# Sauti ya Kweli Kimataifa

(The Voice of Truth International)

Toleo la 95

Mchapaji (Publisher):
**World Evangelism Team**

Nakala ya Kiswahili (Swahili copy):
**Swahili Gospel Team**

Mawasiliano:

+255 (0) 764 792 979
+255 (0) 784 880 470
+255 (0) 765 098 981

Taarifa (Notice):

Kitabu hiki hakiuzwi, kinatolewa bure na kanisa la Kristo kupitia taasisi ya ***World Evangelism Team (WET).***
This book is not for sale, it is freely given by the church of Christ throuth the institution ***World Evangelism Team (WET).***

## Wafanya kazi:

| | | |
|---|---|---|
| Mhariri | : | Louis Rushmore |
| Mhariri Mshirika | : | Jerry Bates |
| Mhariri Mstaaf | : | Byron Nichols |
| Mhariri Mwanzilishi | : | J.C. Choate |
| Meneja wa Ofisi | : | Paula Bates |

## WAANDISHI

George Akpabli
Felix O. Aniamalu
Rex Banks
Wayne Barrier
Paula Bates
Roy Beasley
Mike Benson
Ron Bryant
Charles Burch
Kyle Butt
Frank Chesser
Betty B. Choate
Glenn Colley
Lance Cordle
Sunny David
Hans Dederscheck
David Deffenbaugh
Clarence DeLoach, Jr.
Bill Dillon
Bobby G. Dockery
Hershel Dyer
Earl Edwards
Demar Elam
Raymond Elliott
Reuben Emperado
David Everson
Royce Frederick
Gary C. Hampton
Jack Harriman
Parker Henderson
Gordon Hogan
Wayne Jackson
Ancil Jenkins
Jeff Jenkins
John Kachelman, Jr.
Dayton Keesee
David R. Kenney
Dalton Key
Michael L. King
J. Randal Matheny
Cecil May, Jr.
Wes McAdams
Colin McKee
Stan Mitchell
Kevin L. Moore
Owen D. Olbricht
David Pharr
Neal Pollard
Mark Posey
Steve Reeves
Andy Robison
Martha Rushmore
Rebecca Rushmore
David A. Sargent
Darrell Surrette
David Tarbet
J.J. Turner
Ken Tyler
Allen Webster
R.H. Tex Williams
Nathan Wright

# Mpango wa Mungu wa Ukombozi

## Upande wa Mungu

- **Upendo (Yohana 3:16)**
- **Neema (Waefeso 2:8)**
- **Rehema (Tito 3:5)**
- **Injili (Warumi 1:16)**

## Upande wa Kristo

- **Damu ya Kristo (Ufunuo 1:5)**
- **Mpatanishi Wetu (1 Timotheo 2:5)**

## Upande wa Roho Mtakatifu

- **Ufunuo (2 Petro 1:20-21)**

## Upande wa Mwanadamu

- **Kuiamini Biblia (Yohana 8:24)**
- **Kutubu (Matendo ya mitume 17:30)**
- **Kubatizwa (1 Petro 3:21)**
- **Utii (Waebrania 5:8, 9)**
- **Usafi (Ufunuo 22:14)**
- **Uaminifu (Ufunuo 2:10)**
- **Upendo (1 Yohana 2:10)**
- **Tumaini (Warumi 8:24)**
- **Matendo (Yakobo 2:24)**
- **Uvumilivu (Mathayo 10:22)**
- **Kumkiri Kristo (Warumi 10:9-10)**
- **Kuzaliwa Tena (Yohana 3:3-5)**
- **Kuweka Kando Uovu (Yakobo 1:21)**
- **Kuhubiri (1 Wakorintho 1:18, 21)**
- **Kuliitia Jina la Bwana (Warumi 10:14)**
- **Maarifa ya Maandiko (2 Timotheo 3:15)**



# USHIRIKA KATIKA KANISA

Louis Rushmore

Hayati ndugu T. Pierce Brown aliwahi kuandika kwa kina na kwa usahihi wa kibiblia maelezo: "Ushirika katika kanisa ni zao la wokovu." Baadhi ya watu katika kanisa wanatenganisha kanisa na wokovu, lakini kihalisia, hakuna utengano, Biblia inaunganisha vyote. Hakuna anayeweza kufurahia wokovu bila ya kuwa na ushirika katika kanisa, na hakuna mtu awezaye kuwa mshirika katika kanisa kabla kwanza hajaokolewa kutoka katika maisha yake ya awali ya dhambi. Bila ya kujali mtu binafsi anafikiria nini, ushirika katika kanisa na wokovu vimeunganishwa pamoja kwa kudumu.

Mchakato pekee ambao mtu anaweza kuingia katika wokovu ni mchakato unaotambulika ambao kwa huo mtu huingia katika ushirika wa kanisa. Biblia inasema, ***"…Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."*** (Matendo 2:47).

Mchakato huo hupelekea wokovu na ushirika katika kanisa baada ya kufika katika kilele cha ubatizo (Warumi 6:3-5) kwa ajili ya ondoleo la dhambi (Matendo 2:38, 41). Kinyume na mafundisho ya madhehebu yasemavyo, maji ya ubatizo yanaokoa kutoka katika dhambi (1 Petro 3:20-21). Yesu akitoa muhtasari wa mpango mtukufu wa ukombozi wa mwanadamu katika Marko 16:16 kwamba "imani" jumlisha "ubatizo" sawasawa na "wokovu."

Ikilinganishwa na kitendo cha ubatizo wa kimwili, katika ubatizo, Roho Mtakatifu anamchukua mtu aliyeokoka na kumwingiza katika

mwili wa Kristo (1 Wakorintho 12:13), ambao ni kanisa (Waefeso 1:22-23): Wakolosai 1:18) la Kristo (Warumi 16:16). Hivyo, wokovu na ushirika katika kanisa ni jambo moja. Kwa hiyo, kukataa ushirika katika kanisa ni kukataa wokovu wa mtu. Zaidi sana, kusitisha wajibu wa ushirika wa mtu (Waebrania 10:25) ni kuweka njia panda wokovu wake pia (Waebrania 10:26-31).




Wokovu wa Mkristo pekee unakuwa na afya wakati mtu huyo ni mshirika wa kanisa. Kiwango cha shughuli ambayo mtu huingia katika ushirika katika kanisa ni kiashiria cha afya ya kiroho au wokovu wa mtu huyo. Pamoja na hayo, vifungu vingi vya Agano Jipya vinawahamasisha Wakristo waenende kama Wakristo! ***"Kwa maana zamani ninyi mlikuwa giza, bali sasa mmekuwa nuru katika Bwana; enendeni kama watoto wa nuru."*** (Waefeso 5:8). Kanisa la Bwana linahitajika kuenenda kama mwili wa waliookolewa, kama Mkristo mmoja mmoja na kama kundi kwa pamoja (makusanyiko).





# Amani Ya Uongo

Jerry Bates

Amani ni neno zuri ambalo huleta mawimbi ya ridhaa kupitia mioyo ya watu wengi. Amani ni kitu ambacho kila mtu kutoka katika tamaduni yo yote anaihitaji zaidi kuliko kitu cho chote kile. Tunapenda kuwa na amani na wenzetu, lakini chenye thamani zaidi ya hilo ni kuwa na amani na Muumba wetu, Mungu. Kwa bahati mbaya kulingana na Maandiko, watu wengi hawana hiyo amani (Mathayo 7:13-14). Cha kusikitisha zaidi, wengi wanadhani wanayo hiyo amani, na kumbe wamedanganywa. Kristo alitamka maneno ya kukatisha tamaa katika Mathayo 7:21-23**. *“Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, Sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu.”*** Maneno haya yanapatikana mwishoni mwa Hotuba ya Mlimani, na mara nyingi maneno haya hutumika kupambana na fundisho la uwongo kwamba mtu anaokoka kwa imani pekee. Bila shaka, kifungu hiki kinaonesha kuwa inahitajika zaidi ya imani ya kawaida tu ili kumpendeza Mungu. Hata hivyo, katika muktadha, huo haukuwa msingi uliokusudiwa wa maneno hayo. Lengo lilikuwa ni, tufumbue macho yetu dhidi ya hatari

ya kujidanganya wenyewe juu ya amani ya uongo au kuwa na fikra za ulinzi batili. Humo kuna onyo la hatari kuu: mtu anayeonekana kuwa ni mtu wa dini na yu karibu na Mungu, kihalisia, anaweza kuwa mtu asiyejulikana na Mungu.

Tazama jinsi Yesu alivyowaelezea hawa watu wa kidini. Kwanza, walidhani wana imani sahihi. Kwa ujasiri walimtaja Yesu kama Bwana. Hakuna ubaya wo wote katika ukiri huo. Kwa kweli, sisi sote tunapaswa kukiri imani yetu katika Bwana wetu Yesu Kristo (Warumi 10:9); hata hivyo, maneno pekee hayajalishi kitu. Hata mashetani wanamkiri Yesu kuwa ni Mwana wa Mungu (Luka 4:41). Paulo alisema juu watu baadhi ambao ***"Wanakiri ya kwamba wanamjua Mungu, bali kwa matendo yao wanamkana;.."*** (Tito 1:16). Wengi wanaamini katika imani yao au ya familia zao, pamoja na hayo, kamwe hawajawahi kumtumikia Mungu kutoka moyoni. Zaidi sana, watu hawa wanaonekana kuwa na moyo mkuu wa kidini. Kupayuka "Bwana, Bwana," kuna ashiria shauku na moyo mkuu, lakini kuwa na moyo wa kidini.

Pili, hawa watu walitoa unabii kwa jina la Kristo. Kutoa unabii inamaanisha kufikisha ujumbe wa kiroho. Mwanzoni tunaweza kufikiri kuwa haiwezekani. Hakika mtu anaefundisha ukweli humpendeza Mungu. Hata hivyo, inawezekana kwa mtu kufundisha na kuhubiri ujumbe wa kweli wakati yeye mwenyewe hayupo katika ufalme wa Mungu. Kwa mfano Balaam kwenye Hesabu 22 alizungumza maneno sahihi, lakini Petro alisema kwamba Balaam alipenda fungu la wasio haki (2 Petro 2;15). Paulo aliwazungumzia baadhi ya wahubiri wa kipindi chake waliohubiri ukweli lakini walihubiri kwa husuda, ugomvi, na ubinafsi (Wafilipi 1;15-16). Hii ni hatari ambayo hata wahubiri wengi wa sasa hukumbana nalo. Baada ya kuhubiri ukweli na kubatiza roho nyingi, bado tunaweza kupotea ikiwa hatufanyi hivyo kwa moyo thabiti.

Tatu, watu hawa walidai kutoa mapepo na kufanya miujiza mingine mingi. Yuda Iskariote ni mfano mzuri wa hili. Pale Yesu alipowatuma wanafunzi 70 Yuda akiwa mmoja wao, walikuwa na nguvu ya kweli ya kutoa mapepo (Luka 10;17). Hata hivyo, wote tunakumbuka ya

kwamba Yuda alimsaliti Kristo kwa vipande 30 vya fedha. Badala ya toba ya kweli yeye alienda kujinyonga. Pia, tunasoma kuhusu watoaji pepo wa Kiyahudi kama vile wale watoto saba wa Skewa kutoka katika Matendo ya mitume 19:13-16, ambao walietengeneza madai ya uwongo. Yesu ametuonya kuhusu makristo wa uwongo na manabii wa uwongo ambao wanaweza kutokea na kufanya miujiza mikubwa na kuwalaghai wengi (Mathayo 24:24). Kumekuwa na mjadala kuhusu ishara zile kwamba zilikuwa kweli au la! Lakini kwa malengo yetu hapa, maswali yale sio muhimu. Baadhi ya vitu vinavyovutia hufanywa na watu wa dini mbali mbali, hata sasa miujiza mingi hufanyika. Watu wengi watavutiwa na miujiza hiyo na kukiri kuwa Mungu anapendezwa nao na kuwabariki, lakini hivyo vitu vikubwa haviendani na imani thabiti na mafundisho yao yanakinzana na Maandiko ya Bibilia .

Siku ya hukumu, kutakuwa na mshangao mkubwa. Yesu alisema kwamba wengi watasema vitu hivi katika siku ile. Lugha katika Mathayo 7:21-25 inaonesha majivuno na kujidanganya kwa hawa watu. Mtu anaweza kuwa na taswira ya ufedhuli wanaouonesha kwa msisitizo na kudai Bwana anawakubali. Hata hivyo, Yesu atasema ***''sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu.''*** Hawa sio watu waovu. Ni watu wa kidini waliofanya vitu vingi vizuri katika jina la Mungu. Tatizo lao lilikuwa nini? hawakutii amri za Mungu kwa mioyo ya dhati.

Kinachojalisha ni moyo wa dhati na wa kweli. Wengi hupenda kutilia mkazo katika vitu pekee wanavyovifanya. Na wakati ni vizuri sana kuwa bize kufanya kazi ya Mungu. Pia tunatakiwa kufanya vitu hivyo kwa nia thabiti kutoka moyoni. Bila ya kuhusisha uthabiti wa moyo, shughuli zetu zote hazitakuwa na thamani. Hata hivyo, inatupasa kujua ya kuwa kufanya vitu visivyo sahihi kwa sababu sahihi pia ni kazi bure. Tunaweza kuwa na bidii kwa Mungu, lakini kama hatutofuata au kufundisha kweli, hivyo basi bidii na shauku havitakuwa na thamani. Warumi 10:1-3 Paulo alisema kuwa Wayahudi wanabidii kwa Mungu, lakini haikuwa kulingana na maarifa. Kwa hiyo, bidii yao pekee haikuweza kuwaokoa. Kote huko mpaka katika Hotuba ya Mlimani, tunaona kwamba Yesu alisisitiza uthabiti wa moyo, sasa na

hata mwisho, alisisitiza kuwa hata katika huduma yetu ya kiroho tunatakiwa kutenda kwa sababu sahihi, hiyo ni kutoka moyoni. Kinacho jalisha sio kile tunachokifanya bali ni sababu ya kufanya hivyo. Ni rahisi kudanganya wengine, lakini pia muda mwingine tunajidanganya wenyewe. Pamoja na hayo, Mungu ndiye Hakimu, na si mtu mwingine ye yote, na kamwe hatuwezi kumdanganya, kwa sababu Mungu anajua mioyo (Luka 16:15).

**Yohana 14:27**

"Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo. Msifadhaike mioyoni mwenu, wala msiwe na woga."

**Marko 9:50**

"Chumvi ni njema; lakini chumvi ikiwa si chumvi tena, mtaitia nini ikolee? Mwe na chumvi ndani yenu, mkakae kwa amani ninyi kwa ninyi."

**Luka 2:14**

"Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia."

**Luka 10:5**

"Na nyumba yo yote mtakayoingia, semeni kwanza, Amani iwemo nyumbani humu;"

**Waebrania 12:14**

"Tafuteni kwa bidii kuwa na amani na watu wote, na huo utakatifu, ambao hapana mtu atakayemwona Bwana asipokuwa nao."


1932 - 2008

# Upendo Tunaouhitaji Leo

J.C. Choate

Tumesikia mengi kuhusu upendo wa leo. Tumeambiwa ya kuwa yatupasa kuwapenda ndugu zetu. Imesemwa ya kuwa yatupasa kupendana badala ya kupingana na wenzetu. Huu ni kweli, Hata hivyo, wale wanaohubiri upendo mara nyingi wanaishia kwenye mafarakano na mapambano dhidi ya wale wasiokubaliana nao. Licha ya hayo yote imesemwa kuhusu upendo, inaonekana kwa sasa kuna upungufu wa upendo kuliko wakati mwingine.

Wengi wanaohubiri upendo hufikiria hasa upendo wa kimwili. Ufahamu wao umetawaliwa na raha za kimwili, na wamehitimisha kuwa aina hii ya msisitizo ndio utatuzi wa tatizo la dunia ya sasa. Hata hivyo, jambo hili sio sahihi. Upendo wa kimwili unaongeza matatizo badala ya utatuzi. Tunakumbushwa na maelezo ya mtume Yohana akisema, ***“Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake. Maana kila kilichomo duniani, yaani, tamaa ya mwili, na tamaa ya macho, na kiburi cha uzima, havitokani na Baba, bali vyatokana na dunia. Na dunia inapita, pamoja na tamaa zake, bali yeye afanyaye mapenzi ya Mungu adumu hata milele.”*** (1 Yohana 2:15-17).

## Tafsiri ya upendo kwa Mungu ni tofauti na tafsiri ya dunia

Upendo ni nini? Ni hisia chanya, kivutio, urafiki na kujali mtu mwingine. Inaweza ikawa kimaumbile kwa wakati sahihi, lakini tunafikiria hasa kwa maana ya upendo wa kindugu kwa muda huu. Huu ni upendo tunaotakiwa kuwa nao kwa kila mmoja wetu kama Mkristu na kama binadamu. Upendo unapaswa kuwa msingi wa matendo yetu na mahusiano. Kwa tafsiri zaidi soma **1Wakorintho 13** pale Paulo anatuambia upendo ni nini, nini unafanya na nini haufanyi. ***"Upendo huvumilia, hufadhili; upendo hauhusudu; upendo hautakabari; haujivuni; haukosi kuwa na adabu; hautafuti mambo yake; hauoni uchungu; hauhesabu mabaya; haufurahii udhalimu, bali hufurahi pamoja na kweli; huvumilia yote; huamini yote; hutumaini yote; hustahimili yote. Upendo haupungui neno wakati wo wote; bali ukiwapo unabii utabatilika; zikiwapo lugha, zitakoma; yakiwapo maarifa, yatabatilika."*** ( 1 Wakorintho 13:4-8).

Dunia inahitaji upendo uongezeke. Huu upendo unatakiwa kuwa safi, halisi na wa dhati. Haupaswi kuishia katika mahusiano kati ya mwanamke na mwanaume au katika familia ya mtu, bali unapaswa kuhusisha marafiki, majirani, nchi na dunia. Hata Yesu alisema kwamba tunapaswa kuwapenda maadui zetu. Tumsikilize. ***"lakini mimi nawaambia, Wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi,"*** ( Mthayo 5:44)

## Kile Upendo Usichofanya

Tunapaswa kuelewa, ingawa upendo haupaswi kutufanya tuwe na majadiliano kuhusu ukweli au kuifumbia macho dhambi iliyokaribu yetu. Upendo utatuimarisha kuwasaidia wale tunaowapenda kuishinda dhambi, na madhaifu, kukabiliana na matatizo yao, kuliko kuwaacha na dhambi itakayowapeleka Jehanamu, vinginevyo wafanye toba. Upendo utatuhimiza kwenda kwao badala ya kuwasuburi waje kwa ajili ya kusaidiwa. Pamoja na hayo, upendo utatufanya tuwe wavumilivu zaidi, waelewa na watu wenye kusamehe katika kushughulika na wakosaji na wale wanaohitaji msaada wetu. Hii ni aina ya upendo ambao dunia ina hitaji, sio tu kwa maneno bali kwa vitendo.

Hili ndilo litakalobadilisha ulimwemgu kuwa bora na kufanya mambo yawe mazuri zaidi kuliko sheria na majeshi yawezavyo.

Upendo si ishara ya udhaifu bali ni ya nguvu. Upendo unaozungumziwa hapa unapatikana kwa Mungu na kwa Yesu kristo, Mwanawe. Kama matokeo, tunaletwa kwenye hatua ya kutii mafundisho ya Mungu na kuyatenda mapenzi yake katika maisha yetu. Upendo tulionao kwa Mungu unatuongoza kuwapenda majirani zetu na watu wote ulimwenguni (Mathayo 22:36-39). Kwa sababu tuna mpenda, hivyo tupendane pia.

## Inawezekanaje Kumpenda Adui Yangu?

Shadrack S. Msambaza

***"Lakini mimi nawaambia, wapendeni adui zenu, waombeeni wanaowaudhi,"*** (Mathayo 5:44). Adui kwa tafsiri ya kawaida ni mtu yeyote anayekutendea vibaya kinyume na haki. Watu wanaoudhi katika ayah ii inawarejelea watu watesaji, wanaoshambulia mwili na wakati mwingine kusababisha kifo. Wakristo wa karne ya kwanza walikabiliwa na hatari ya mateso na kifo. Wengi wa Wakristo hawa waliteswa kuuawa kikatili, lakini bado walitakiwa kuwapenda na kuwaombea wale waliokuwa wakiwatendea hayo. Amri hii sit u kwamba Kristo aliiagiza kwa wengine bali kwanza yeye mwenyewe alionesha mfano pindi alipowaombea msamaha wale waliokuwa wakimtesa na kumwua (Luka 23:34). Wakati tunafikiri kuwa hii ni amri ngumu kuitekeleza, Yesu anatuonesha kuwa inawezekana. Mtu mwingine wa kawaida kuliko Yesu aliyeonesha kuwa inawezekana ni, Stefano (Matendo 7:60). Ikiwa bado ni vigumu kwako kung'amua tazama ufafanuzi katika Mathayo 5:45, ***"…maana yeye huwaangazia jua lake waovu na wema, huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki."*** Mungu anachukia dhambi, hawachukii wenye dhambi, ndiomaana mwenye dhambi akitubu anasamehewa. Mtume Paulo anahitimisha hoja hii kwa kuandika: ***"Lakini, Adui yako akiwa na njaa, mlishe; akiwa na kiu, mnyweshe; maana ufanyapo hivyo, utampalia makaa ya moto kichwani pake. Usishindwe na ubaya, bali uushinde ubaya kwa wema."*** (Warumi 12:20-21).



# Dakika 5 Za Kujifunza Biblia

**Paula Bates**

## *Toba*

1. Yohana alitokea, akibatiza nyikani, na ______ubatizo wa ______liletalo ondoleo la dhambi. (Marko 1:4).

2. Yesu aliposikia aliwaambia, Wenye____ hawahitaji tabibu, bali walio hawawezi; sikuja kuwaita wenye___, bali wenye _______. (Marko 2:17).

3. Tokea wakati huo Yesu alianza_____, na kusema, Tubuni; kwa maana_____ wa mbinguni umekaribia. (Mathayo 4:17).

4. Nawaambia, Vivyo hivyo kutakuwa na_____ mbinguni kwa ajili ya mwenye dhambi mmoja____, kuliko kwa ajili ya wenye haki tisini na kenda ambao hawana haja ya kutubu. (Luka 15:7).

5. na kwamba______yote watahubiriwa kwa____lake habari ya toba na_______ la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu. (Luka 24:47).

6. Petro akawaambia,_____ ________ kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio______, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie. (Matendo 2:38-39).

**Majibu:**

1. Kuuhubiri, Toba
2. Afya, haki, dhambi
3. Kuhubiri, ufalme
4. Furaha, atubuye
5. Mataifa, jina, ondoleo,
6. Tubuni, mkabatizwe, mbali

# Yaliyomo


## Mungu

Furaha Pasipo Mungu……………………….Denny Petrillo……………………………………..16
Amani………………………………………………..Andy Robison………………………………………18
Katika Janga Yesu Huleta Tumaini………………….Charles Box…………………………………..21

## Ushahidi

Wazazi Walindeni Watoto Wenu…………………….Carl Mitchell……………………………….24
Toka Nje Ya Uzio: Mageuzi…………………………....Jack Wilkie………………………………….26

## Neno la Mungu

Ufanye Bidii Katika Kusoma……………………………Jimmy Clark……………………………..29
Je! Ni Kweli Biblia Inafundisha Hivyo?................Neal Polland……………………………..31
Kile Biblia Inachofundisha Kuhusu Yenyewe – Ni Hitimisho….Paul Holland…………....33

## Wokovu

Wokovu Wa Kipekee Wa Milele…………………….Owen D. Olbricht…………………………..35
Moyo Usio Na Toba……………………………………….Dwaight Fuqua………………………..37
Mwaliko Wa Mialiko……………………………….Patrick Morrison……………………………..39

## Kanisa

Kazi Ya Kipekee……………………………………..Bob Plunket……………………………………..44
Kundi Moja Na Mchungaji Mmoja…………….Cliff Holmes……………………………………..46
Jambo La Kusisimua………………………………..John Gipson………………………………….…..48

## Fundisho la Kuishi Kwalo

Mfano Wa Kutoa Katika Agano Jipya…………………..Lance Mosher…………………………..50
Imani Na Kuona…………………………………….Joseph Ezenweze…………………………………53

## Ukristo Katika Vitendo

Mamajusi Walikuja Kumtafuta Yesu……………………Sunny David…………………………….56
Agizo Lake Ni Kazi Yetu……………………………...Darrell Surrette……………………………….60
Serikali Na Mkristo: Mtazamo Wa Kanisa Na Utamaduni….Steve Higginbotham……..62

## Ibada

Ukumbusho Kwa Bwana…………………………….Gary C. Hampton……………………………64
Kumwabudu Mungu Katika Nyimbo……………….Mark N. Posey………………………………66
Utuhuishe Tena: Kuna Uhitaji Wa Uamsho Katika Kanisa La Leo…..C. Thompson…….67

## Maisha ya Kila Siku ya Kikristo

Utajiri Na Umaarufu Wa Duniani Hauwezi Kuniingia Kamwe………Don Myers………….74
Biblia Inafundisha Nini Kuhusu Kufunga? Je, Kufunga Ni Kwa Ajili Ya Wakristo?.....Erick Obeng Asant……………………………………………………………………………………….78
Bwana Anawaita Wapiganaji Wote Kufanya Vita Na Shetani, Njooni Nyote Tuvae Silaha Na Twende Vitani…………………………….Dare Hart………………………………………81

## Nyumba ya Kikristo


Waume Tafadhali Someni……………………………….Samuel Matthews………………………..83
Wake!..........................................Betty Burton Choate………………………………………..87
Je, Tunalea Wanamichezo Au Wakristo?....................Wes McAdams…………………..91


## Uchunguzi wa Vifungu


Tubu Au Angamia……………………………………..Dennis Gulledge…………………………………94
Kristo Anakuja Na Watakatifu Wake Wote…………………Kevin L. Moore…………………..96


## Wahusika Katika Biblia


Agizo La Daudi Kwa Sulemani…………………………Therman Hodge…………………………..98
Stefano: Shahidi Mwaminifu Hadi Mwisho………….Brian R. Kenyon……………………..100


## Maswali katika Biblia


Je, Sisi Ni Watetezi?.............................................Mike Riley……………………………104
Kwanini Yesu Alibatizwa?................................Jerry A. Jenkins……………………………105


## Majedwali na Mihtasari


Ukweli Wa Msingi Kuhusu Ubatizo Wa Agano Jipya………Ronald D. Reeves………….107


## Historia ya Kanisa


Ni Changamoto Gani Ambazo Kanisa La Karne Ya Kwanza Lilikabiliana Nazo? Mapambano Dhidi Ya Serikali Na Desturi Za Kidini………….Jeremy W. Barrier………..109


## Makala, Mashairi na Vijazi


Ushirika Katika Kanisa…………………………….Louis Rushmore……………………………….04
Amani Ya Uwongo…………………………………….Jerry Bates…………………………………………..06
Upendo Tunaouhitaji Leo………………………….J.C. Choate…………………………………………..10
Dondoo Za Shadrack………………………………………………………………………12,25,41,45,52,59
Dakika Tano Za Kujifunza Biblia…………………….Paula Bates…………………………………….13
Tafuta Aya……………………………………………..Jerry Bates……………………………………………42
Tafuta Katika Biblia………………………………………Martha Rushmore………………………..49
Rubi Za Robison…………………………………………………………………………………………….54
Maoni Ya Haraka Katika Aya Muhimu……………………………………………………………55
Ni Zipi Alama Za Mfuasi?..............................Therman Hodge………………………………63
Dondoo Za Mwl. Kamatula…………………………………………………69,77,86,90,95,114,120
Je, Unapima Vipi?...........................................................................................70
Ucheshi: Mithali 17:22…………………………….jerry Bates…………………………………………71
Kiasi………………………………………………………Ed Benesh……………………………………………80
Msaka Tonge……………………………………………Rebecca Rushmore………………………97
Kutoka Katika Moyo Wa… Wote Wanakubali………Guy Caskey……………………………115

# Furaha Pasipo Mungu

Denny Petrillo

***"Kwa maana ni nani awezaye kula au kujiburudisha kuliko mimi?"*** (Mhubiri 2:25). Bila shaka watu hula, na kufurahia sana chakula. Watu wa leo ni watu wa burudani, wakifurahia matunda yasiyo sambamba na utajiri. Kwa hiyo, hoja ya Sulemani ilikuwa nini?

Kwanza, katika akili ya kawaida, bila ya Mungu haiwezekani kuwa na furaha ya kweli ya baraka katika maisha. Wakati wengine wanaweza kuhisi kwamba kuwa na pombe katika mlo ni "maisha mazuri," lakini, kihalisia, ni ukosaji na kupungukiwa. Kwa nini? Kwa sababu kwa masikitiko mtu huamini kwamba furaha yake huja kwa sababu ya juhudi zake mwenyewe na kwa uwezo wake mwenyewe. Hivyo, hukosa shukrani. Ni ukosefu wa utambuzi kwamba kama ingekuwa si Mungu kuleta baraka zake kwa wenye haki na wasio haki, wasingekuwa na cho chote (Mathayo 5:44).

Pili, kutambua mkono wa Mungu katika baraka za mtu hurefusha furaha, hata katika baraka za kawaida kabisa. Hatuhitaji kuishi katika majumba, au kuendesha gari zuri au kuvaa nguo za gharama ili kuwa na furaha. Paulo alisema kwamba, ***"ila tukiwa na chakula na nguo tutaridhika na vitu hivyo."*** (1 Timotheo 6:8). Pia aliandika ***"Najua kudhiliwa, tena najua kufanikiwa; katika hali yo yote,"*** Mtu anawezaje kufanya hivyo kwa mafanikio? Siri ni, ***"Nayaweza mambo yote katika yeye anitiaye nguvu."*** (Wafilipi 4:12-13). Sulemani, aliyebarikiwa kwa utajiri mkubwa, alitambua kwamba kuwa na vyote mtu avitakavyo ni (angalia katika orodha yake katika Mhubiri 2:1-11) ***"ubatili na kujilisha upepo"*** Kwa nini? Kwa sababu furaha ya kweli idumuyo, haipatikani katika vitu au katika anasa za dunia.

Kuwa na Mungu katika maisha ya mtu huleta ***"amani ipitayo ufahamu"*** (Wafilipi 4:7), na humfanya kufurahia na kushukuru baraka

zote nzuri za Mungu. Sasa, ni nini jibu la swali letu? Je, mtu anaweza kuwa na furaha pasipo Mungu? Hapana, si furaha ya kweli. Pekee tunapokuwa na Mungu katika maisha yetu ndipo tunapoweza kuwa na furaha zote zinazopatikana katika dunia.

**Denny Petrillo ni raisi wa Taasisi ya Biblia ya Bear Valley huko Denver, Colorado, Marekani.**

**Zaburi 40:8**
"Kuyafanya mapenzi yako, Ee Mungu wangu, ndiyo furaha yangu; Naam, sheria yako imo moyoni mwangu."

**Zaburi 16:11**
"Utanijulisha njia ya uzima; Mbele za uso wako ziko furaha tele; Na katika mkono wako wa kuume Mna mema ya milele."

**Zaburi 4:7**
"Umenitia furaha moyoni mwangu, Kupita yao wanapozidishiwa nafaka na divai."

**Zaburi 51:12**
"Unirudishie furaha ya wokovu wako; Unitegemeze kwa roho ya wepesi."

**Zaburi 97:11**
"Nuru imemzukia mwenye haki, Na furaha wanyofu wa moyo."

**Zaburi 118:15**
"Sauti ya furaha na wokovu Imo hemani mwao wenye haki; Mkono wa kuume wa Bwana hutenda makuu."

**Zaburi 119:92**
"Kama sheria yako isingalikuwa furaha yangu, Hapo ningalipotea katika taabu zangu."

# AMANI

Andy Robison

Yesu alipozaliwa, malaika walikuwa wakisifu "***atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia"*** ( Luka 2:14)!

Miaka mia saba kabla Kristo hajazaliwa , ilitabiriwa kuwa ataitwa ***" Mfalme wa Amani***" (Isaya 9:6). Paulo alisema kuwa Kristo ***" kwa maana yeye ndiye amani yetu…"*** ( Waefeso 2: 14). Hata kwa tazamio la haraka Maandiko yanahusisha jina la Yesu na amani. Hata hivyo, Kristo mwenyewe alisema. ***" Je! mwadhani ya kwamba nimekuja kuleta amani duniani? Nawaambia, La, sivyo bali mafarakano.***" (Luka 12:51).

Kinachovutia zaidi hata katika Maandiko ya Mathayo kuhusu maelezo ya Yesu yanayofanana na hayo, " ***msidhani ya kuwa nimekuja kuleta amani duniani; la! Sikuja kuleta amani, bali upanga."*** ( Mathayo 10:34)

Anawezaje kuwa mwanzilishi wa amani na chanzo cha mgawanyiko kwa wakati mmoja? Kuna watu wanaopinga dini zote, ikiwemo Ukristo, kama mawazo yanayosababisha vurugu. Hili linaweza kuwa kweli? Tafathali zingatia haya mawazo.

## Kristo Pamoja na Mungu Wameleta Amani

Wale wanaomfuata Kristo kwa uaminifu wanaweza kuwa na amani kwa sababu wanazishinda dhambi zao. Hakuna kinachoponda nafsi ya mtu zaidi ya ufahamu wa kufanya makosa. Ingawa wengi hawatakubaliana na hili hata kwa miaka, hatia huleta matatizo. Jamii tangu mwanzo zimekuwa zikitafuta aina fulani ya Mungu kwa ajili ya aina fulani ya ukombozi. Mfumo wa maadili umebadilishwa juu chini na uovu ukaitwa wema, na wema ukaitwa uovu, lakini bado watu

waliendelea kutafuta aina fulani ya msamaha. Mika anaonesha watu waovu wakitahamaki, ni wanyama wangapi watawatoa kwa ajili ya dhambi zao, na hata kuuliza kama itawapasa kuwatoa wazaliwa wao wa kwanza? Haya ni mawazo ya unyenyekevu kwa Mungu (Mika 6:6-8).

Kristo, ingawa ameleta uhuru kwa kila asiye mtauwa, mfumo wa kipagani. Ameleta uhuru hata kutoka kwa kiongozi ( Wagalatia 3:24-25) sheria ya Musa kuhusu dhabihu. Alijitoa yeye mwenyewe ***"..mara moja tu katika patakatifu, akiisha kupata ukombozi wa milele"*** (Waebrania 9:12). Wale waliomtii walipata wokovu (Waebrania 5:9). Elewa ya kwamba, Imani inahususha utii, waraka wa Paulo kwa Warumi 5:1 inafariji " ***basi tukiisha hesabiwa haki itokayo katika Imani, na mwe na amani kwa Mungu, kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo"*** wale Wakristo waliomtwika Mungu fadhaa zao, walipata ***"…amani ya Mungu ipitayo akili zote"***( Wafilipi 4:7)

## Kristo Huleta Amani Baina ya Makundi ya Watu

Wayahudi na mataifa (na kwa upana makabila yote na watu wa madaraja yote) wameletwa pamoja katika kanisa la Kristo (Waefaeso 2:14-17). Wote wamekuwa ***"mmoja katika Kristo Yesu"*** ( Wagalatia 3:28). Kwa hakika, Injili imeundwa ili kila mtu kutoka kila taifa, rangi, na utofauti wa kiuchumi na kijamii wanaweza kukaa pamoja na kuungana katika ufalme wa Mungu. Wamarekani, Warusi, Waafrika, Wairaq na Wachina ni ndugu katika familia ya Mungu (Marko 3:31-35, Waebrania 2:11-12). Pale kanisa



linapofanya kazi kama inavyopaswa, hivyo vikwazo kama rangi, mali, na utaifa zitashindwa kwa damu ya dhamani ya Yesu Kristo.

## Kutokutii kwa Watu Huchochea Mafarakano

Kwa hakika, Kristo huleta faraka katika familia pindi mmoja anapotii na wale wasiotii Injili. Watano katika nyumba moja wanaweza kufarakana, Alifundisha hivyo katika (Luka 12: 52-53). Wakristo hujiletea mateso juu yao wenyewe kwa sababu ya kuishi kwa haki.( 1 Petro 3:13-17; 4:12-16). Mateso ni nini isipokuwa ni mafarakano makali baina ya watu? Wakristo wa awali walijulikana kimakosa kama watu wanaochukia watu kwa sababu hawakukubaliana na maadili mabaya na jamii ya waabudu sanamu. Shitaka hilo lilileta kisasi.

Hakika, kamwe Kristo hakuwahi kuhidhinisha mashambulizi au matumizi yo yote ya vurugu kwa Mkristo mmoja mmoja au kanisa kwa ujumla. Hasa Yeye anahitaji amani, aliwaamuru watu wake waitafute kwa bidii, kwa kadiri ya uwezo wao ( Warumi 12:18; Waebrania 12:14).

## Kanuni za Kristo Zinaleta Amani Zaidi

Hata miongoni mwa wale amabao wanaweza wasiwe Wakristo wa Agano Jipya, maaadam kanuni za Kristo zinatekelezwa, kutakuwa na amani. Amefundisha kutokuwa wabinafsi, bali tuwe watu wa utoaji, upendo wakujitoa, hata kwa adui (Mathayo 5: 43-48). Aliwafundisha watu kuwatendea wengine kama wanavyotaka wao kutendewa (Matheyo 7:12). Hizo kanuni mbili zenyewe huleta amani, amani iliyowakandamiza mno watu wanyenyekevu.

**Andy Robison ni mhubiri wa kanisa la kristo Hillview Terrace pia ni mkurugenzi wa Shule ya Mahubiri ya Virginia ya Magharibi huko Moundsville, Magharibi mwa Virginia, Marekani.**

# Katika Janga Yesu Huleta Tumaini

Charles Box

Dunia yetu imejaa majanga. Watu wamejeruhiwa na kuuawa na mafuliko, moto, vimbunga na ajali. Matetemeko ya ardhi na tufani huja kwa nguvu zao za maangamizi. Magonjwa hufanya kazi na nguvu za kifo. Hata hivyo, katika janga Yesu anaweza kuleta tumaini.

## Mtoto Alikuwa na Miaka 12

Daima imekuwa ni jambo la kuhuzunisha kuhusu ugonjwa au kifo cha mtoto. Binti wa miaka 12 alikuwa anaugua sana. Marko 5:22-23 inaonesha jinsi baba wa mtoto alivyomwendea Yesu. ***"Akaja mtu mmoja katika wakuu wa sinagogi, jina lake Yairo; hata alipomwona, akaanguka miguuni pake, akimsihi sana, akisema, Binti yangu mdogo yu katika kufa; nakuomba uje, uweke mkono wako juu yake, apate kupona, na kuishi."*** Janga la kuugua kwa mtoto lilimfanya huyu kiongozi wa Sinagogi kupiga magoti. Watu wengi waliokuwa upande wa Yairo walikuwa wakimpinga Yesu. Inawezekana pia hata yeye mwenyewe alikuwa akimpinga Bwana wetu vilevile, lakini hayo yote yalisahaulika pindi alipomwendea Yesu kumwomba msaada na tumaini. Wengi wetu hupenda kuendesha maisha yetu wenyewe, lakini ebu tuwe wanyenyejevu vya kutosha tukitambua ya kwmba msaada wetu pekee na tumaini ni katika Kristo. Kwa hili, Yairo alijifunza, na kwa kujifunza huko binti yake alipata afya.

## Tumaini la Mwisho la Mwanamke

Wakati Yesu na Yairo wakiondoka, mwanamke kutoka katika umati alimjia na kuligusa vazi lake. ***"Akaenda pamoja naye; mkutano mkuu wakamfuata, wakimsonga-songa. Na mwanamke mmoja mwenye kutoka damu muda wa miaka kumi na miwili, na kuteswa mengi kwa***

***mikono ya matabibu wengi, amegharimiwa vitu vyote alivyo navyo, kusimfae hata kidogo, bali hali yake ilizidi kuwa mbaya aliposikia habari za Yesu, alipita katika mkutano kwa nyuma, akaligusa vazi lake; maana alisema, Nikiyagusa mavazi yake tu, nitapona. Mara chemchemi ya damu yake ikakauka, naye akafahamu mwilini mwake kwamba amepona msiba ule."*** (Marko 5:24-29).

Masikini mwanamke yule aliteseka kwa miaka kumi na mbili, akitumia fedha zake zote kwa matabibu lakini hali ilizidi kuwa mbaya. Matabibu wana nafasi yao, lakini hawakufanikiwa kumsaidia yule mwanamke. Alimwendea Yesu kama nafasi yake ya mwisho. Je! Si jambo la kustahajabisha kuwa watu wengi wanafanya jambo kama hilo? Wanajaribu kila njia, hatimaye, wanaamua kujaribu kwa Yesu. Na tujifunze kwamba Bwana Yesu ni msaada uliopo katika nyakati za shida.

## Mwanamke Aliyeponywa

Wakati uponyaji ulipotokea, kuna kitu kilimtoka Yesu, ***"aliposikia habari za Yesu, alipita katika mkutano kwa nyuma, akaligusa vazi lake; maana alisema, Nikiyagusa mavazi yake tu, nitapona. Mara chemchemi ya damu yake ikakauka, naye akafahamu mwilini mwake kwamba amepona msiba ule. Mara Yesu, hali akifahamu nafsini mwake kwamba nguvu zimemtoka, akageuka kati ya mkutano, akasema, Ni nani aliyenigusa mavazi yangu?"*** (Marko 5:27-30). Kuna mambo makuu hufanikishwa pindi tu mtu anapoamua kuweka maisha yake katika hilo. Huu ulikuwa ni ukweli kwa Yesu, na hata kwetu na kazi zetu. Yesu alikuwa Mkuu kwa sababu alikuwa tayari kujitoa ili awahudumie wengine. Wanafunzi hawakuweza kuelewa ni kwa jinsi gani Yesu aliweza kujua mtu aliyemgusa kutoka katika umati. Mara nyingi, tumekuwa kama wanafunzi wale, tumeshindwa kuelewa dhabihu iliyotolewa na wengine kuwahudumia watu. Sehemu hii ya Maandiko inatufundisha somo kubwa kutoka kwa yule mwanamke. ***"Na yule mwanamke akaingiwa na hofu na kutetemeka, akijua lililompata, akaja akamwangukia, akamweleza kweli yote."*** (Marko

5:33). Kwa ufupi alimwambia Yesu ***"ukweli wote"*** na matokeo yalikuwa mazuri. ***"Akamwambia, Binti, imani yako imekuponya, enenda zako kwa amani, uwe mzima, usiwe na msiba wako tena."*** (Marko 5:34).

## Kukata Tamaa Kumegeuka Kuwa Tumaini

Neno lilikuja ambalo lilisababisha kukata tama. ***"…binti yako amekwisha kufa; kwani kuzidi kumsumbua Mwalimu?"*** (Marko 5:35). Kuna nguvu iliyokinyume na waombolezaji waliokata tamaa na tumaini lililo katika Yesu. Sauti ya matumaini ilisikika ikisema, ***"…Mbona mnafanya ghasia na kulia? Kijana hakufa, bali amelala tu."*** (Marko 5:39). Mara nyingi wasio wacha-Mungu "hucheka kwa zihaka", wale wanaolichukua neno la Yesu. Kwa upole na nguvu ya maneno, Yesu alinyamazisha vicheko vyao. ***"Akamshika mkono kijana, akamwambia, Talitha, kumi; tafsiri yake, Msichana, nakuambia, Inuka. Mara akasimama yule kijana, akaenda; maana alikuwa amepata umri wa miaka kumi na miwili. Mara wakashangaa mshangao mkuu."*** (Marko 5:41-42). Katika Siku ya Hukumu, wengi, waliotuzihaki, Wakristo wa Agano Jipya, watasimama kimya, wakiwa wameduwaa.

Kutoka katika Marko 5:21-43 na tujifunze: (1) Watu hukabiliwa na majanga mengi katika maisha haya. (2) Magonjwa huwapata wakubwa kwa wadogo. (3) Yesu ni kweli anajali pindi watu wanapoteseka. (4) Yesu ana uwezo wa kugeuza huzuni kuwa tumaini. (5) Wale wanaouzihaki Ukristo watafumbwa midomo. (6) Yesu ndiye tumaini letu pekee. (7) Ikiwa tutamruhusu Kristo kutawala maisha yetu, hivyo, **maisha ya sasa na yale yajayo** yatakuwa yetu (Warumi 6:1-6; Matendo 3:36-41; Yohana 10:10).

**Charles Box ni mhubiri wa kanisa la Kristo Mtaa wa Walnut huko Greenville, Alabama, Marekani.**

# Wazazi, Walindeni Watoto Wenu!

Carl Mitchell

Katika maelezo mazuri ya ushairi katika Zaburi, twasoma, ***"Fadhili na kweli zimekutana, Haki na amani zimehusiana."*** (85:10. Wazo linalozungumziwa hapo ni kwamba ubora wa mambo haya mawili huenda pamoja. Nina amini hiyo ndiyo asili ya Neno la Mungu kama vile mshikamano unaoishi miungoni mwa fadhili zake kuu ambapo moja wapo kwa aslili huonekana kuongoza wengine katika uzani endelevu.

Huu ni ukweli pia katika uovu. Tunaweza pia kuhusisha kanuni hii katika siku za leo.

Falsafa za Shetani ziko kila mahali karibu yetu. Zinasafiri vizuri kwa pamoja, si kwamba zinafanana katika maudhui yao yote, lakini zina uwiano mkubwa katika msingi wa nia kuelekea katika ukosefu wa ukweli halisi, vituo vyao ni katika mtu mmoja mmoja na si kwa Mungu ambaye ni kiti cha mamlaka na katika zihaka zao hatimaye zitawapeleka hukumuni kulingana na Maandiko Matakatifu.

Wazazi wanapaswa kuwa macho dhidi ya misingi mikuu ambayo ipo katika mitindo tofauti itolewayo na vyombo vya habari. **Kiwanda cha filamu, runinga, majarida maarufu na vitabu visivyo vitakatifu.**

Kama unadhani vinavyosukuma falsafa za "Nyakati Mpya" viko kimya, basi nenda katika duka la vitabu uone chaguzi nyingi za vitabu vyenye ujumbe kutoka kwa; malaika, michoro au picha elekezi, tafakuri, faida za maruwe-ruwe zitokanazo na madawa, nguvu za giza na mengine mengi. Chakufanya, jihusishe na vyanzo vya taarifa vinavyoonesha athari zilizopo katika harakati hizi, kwa mfano vitabu vinavyozungumzia mafundisho ya Yesu dhidi ya falsafa au mafundisho ya kidunia.

Wazazi wanaweza kufanya nini ili kuwalinda na mitazamo ya kidunia? Kwanza, tunatakiwa kujua kwamba tunaweza kumtegemea Mungu ili abariki juhudi zetu. Pili, tunatakiwa kufahamu kwamba utamaduni wetu unabadilika kwa kasi kwa sababu ya ushawishi wa kidunia. Takwimu zinaonesha, watu wengi wanaamini katika falsafa za kidunia kuliko uhalisia wa Maandiko Matakatifu.

Wazazi wanapaswa kuwaelimisha watoto wao ukweli wa Biblia, mpango wa Mungu kumtuma Yesu, jinsi alivyochukua umbo la kibinadamu, maisha yake, mafundisho yake, dhabihu yake ya ukombozi na kufufuka kwake. Wanapaswa kuwafundisha maisha ya Kikristo, msaada wa Kiungu, Ujio wa Mara ya pili, Hukumu, Mbingu na Jehanamu.

Katika mazungumzo yao wanapaswa kuwashirikisha hadithi zijengazo. Wanapaswa kujua kwamba **tupo katika mapambano kati ya kifo na uzima dhidi ya Shetani kwa ajili ya hatima ya watoto wetu**, na hivyo ni hatari sana kutegemea peke yake madarasa ya Jumapili, au shule za Kikristo, au shule ya Biblia kwa njia ya video, kambi za muda mfupi ili kuwakamilisha katika mapambano haya. Wazazi wanatakiwa kujitoa kwa kadiri wawezavyo ili kuongoza roho za watoto wao kwa Mungu ambaye aliwaumba, na matamanio yake ni kuishi pamoja nao milele.

**Carl Mitchell anatumika kama Profesa wa Biblia katika chuo kikuu cha Harding huko Searcy, Arkansas, Marekani.**

## Swali la Kujiuliza: Kwa nini Farao Alitaka Kubaki na Watoto?

Shadrack S. Msambaza

***"Sivyo, endeni ninyi mlio watu wazima, mkamtumikie Bwana; kwa kuwa ndilo jambo mtakalo. Nao walifukuzwa usoni pa Farao."*** (Kutoka 10:11). Farao hakutaka watoto wafunzwe kumtumikia BWANA bali alitaka wafundishwe kumtumikia yeye na hivyo, waendelee kuwa watumwa wake daima. Hivi ndivyo Shetani atakavyo hata leo. Kama kweli tunataka kuwalinda watoto wetu, basi ni lazima tuchunguze aina ya elimu wanayoipata katika maisha yao ya kila siku.

# Toka Nje ya Uzio: Mageuzi

Jack Wilkie

Wakristo wengi wanajaribu "kuuendesha uzio" katika dunia ya leo. wanajikuta wamenaswa katikati baina ya mafundisho ya kibiblia yaliyo bayana na kile utamaduni unachowashinikiza kuamini, na kwa hiyo, wanajaribu kutafuta aina fulani ya muafaka. Jambo kama hilo lilitokea mara nyingi katika Biblia, moja ya mfano unatoka katika kipindi cha changamoto ya Eliya dhidi ya manabii wa Baali. Katika 1 Wafalme 18:21, watu walipokusanyika karibu ili waone nani ambaye angeshinda kati ya Mungu na Baali, Eliya akawapa changamoto kila mmoja wao: ***"Naye Eliya akawakaribia watu wote, akanena, Mtasita-sita katikati ya mawazo mawili hata lini? Bwana akiwa ndiye Mungu, mfuateni; bali ikiwa Baali ni Mungu, haya! Mfuateni yeye. Wale watu hawakumjibu neno."***

Ni wakati wa Wakristo kuwapa changamoto wale wanaotembea katika uzio na kuwauliza, "Hata lini mtasita-sita katikati ya mawzo mawili?"

"Ndiyo, mimi ni Mkristo, lakini pia ninaiamini sayansi, kwa hiyo sikani (falsafa ya) mageuzi." Wazo pendekezwa la kawaida ambalo mtu hawezi kushikilia maelezo ya uumbaji katika kitabu cha Mwanzo na bado kuendelea kuamini sayansi imepelekea Wakristo wengi kutamka maelezo hayo, lakini je, wanapaswa? Je! Tunalazimika kubaki katika uzio baina ya kuamini katika Biblia na mafundisho ya Mageuzi (revolution)? Bila shaka hapana.

## Toka Nje ya Uzio Kwa Sababu Ushahidi Upo Upande wa Mungu

Daima ujumbe huonekana kuwa ni kitu fulani kinachoambatana na, "Tunapaswa kuwa katika upande ambao wanasayansi

wanatuambia tuwe au vinginevyo ulimwengu utatuona kuwa hatuko sawa." Sawa, unajua nini, kamwe Biblia haijawahi kukubalika na jamii. Yesu alituambia tutarajie hilo (Yohana 15:18-25). Mbaya zaidi, ni kuikosea heshima elimu kwa watu kuendelea kueneza ushindani kati ya simulizi za "sayansi dhidi ya Biblia." Sayansi haina upendeleo, na kwa sababu hiyo haichagui upande. Hata hivyo, wanasayansi wana upendeleo, na hilo ndilo mara nyingi usahaulika. Waundaji na Wanamageuzi huletewa ushahidi mmoja na sayansi. Pekee wanapotofautiana ni katika tafsiri, na watu bado wataona kile tu ambacho wao wanataka waone. Ushahidi, ingawa, unabaki katika uhalisia, na kuna sababu nyingi za kuamini kwamba ushahidi upo upande wa mafundisho ya Biblia.

Hata hivyo, kwa nini tuwe na wasiwasi juu ya mawazo ya watu ambao hawana maelezo yo yote juu ya wapi ulimwengu ulitokea? Kwa nini tuwe na wasiwasi juu ya mawazo ya watu waliogoma kusogea katika tarehe ya mjusi mkubwa (dainaso) wakati ambapo ushahidi unaendelea kujitokeza kwamba walikuwa wakiishi si muda mrefu sana kuliko wazo la awali lisemavyo? Kwa nini tuwe na wasiwasi na mawazo ya watu ambao maelezo yao katika kila kitu ni kwamba hakuna kilicholipuka na kuumba ulimwengu usiowezekana katika utatanishi? Watu hawa hawawezi hata kujua ni kwa muda gani mwanadamu amekuwepo. Kwa kweli sijali kama watu wanaoegemea katika jambo hilo la kipuuzi wataniona kuwa sina akili kwa sababu ya kutokukubaliana nao.

## Toka Nje ya Uzio Kwa Sababu Biblia Haiambatani na Mawazo Yote Mawili

Kama unakataa maelezo ya kwamba Adamu ndiye wa kwanza kuumbwa, basi utakuwa unaweka hoja nzito. Utakuwa unasema kwamba Yesu na waandishi wa Biblia waliovuviwa wote walikosea pindi walipomrejelea Adamu na uumbaji katika vitabu. Kama una amini kuwa Yesu ni Mungu aliyevaa mwili na ya kwamba Maandiko yamevuviwa na Mungu, na kwa wakati huohuo unasema kwamba

uumbaji ni hadithi ya kutunga tu, utakuwa unamaanisha kwamba Mungu hakuwa anaelewa kwamba kitabu cha Mwanzo 1-3 ilikuwa ni hadithi tu. Nyongeza, utakuwa unasema kwamba Adamu na Hawa hawakutambulisha dhambi na kifo katika dunia, na kwa hiyo kifo kilisababishwa na sheria za asili muda mrefu uliopita hata kabla ya binadamu kuwepo. Hiyo inamaanisha kwamba Mungu, na sio mwanadamu, ndiye msababishi wa kifo na mateso, kitu ambacho kwa hakika kinasambaratisha Injili. Je, unaona sasa jinsi ambavyo hayo mawazo yanaweza kuathiri msingi wa imani yetu na kujeruhi ushawishi wa kanisa? Inakupasa kuchagua upande mmoja wa uzio au mwingine.

Sisemi kwamba Mkristo hawezi kwenda Mbinguni kama anaamini katika dhana ya mageuzi, bali wale wanaofanya biashara na maelezo yaliyotolewa katika kitabu cha Mwanzo na kuungwa mkono na Yesu na kuyachanganya na viwango vya dunia inayotuambia kwamba tunapaswa kuamini hivyo, watakuwa wakipita katika njia hatarishi. Hatuwezi kuwaacha wale wanaokataa uwepo wa Mungu watutafsirie Biblia, hususani pale ambapo hata ushahidi wa kisayansi haupo upande wao. Kanisa halikusaidiwa na wale waghushio Biblia.

Usiamini wazo ya kwamba Biblia na sayansi hazipatani. “Toka Nje ya Uzio” katika fundisho hili la mageuzi halimaanishi kuwe na uchaguzi kati ya Biblia na sayansi; inamaanisha kuchagua ushahidi wa kisayansi katika Biblia na usumbufu usio na ushahidi wa kisayansi katika dhana ya mageuzi. Fanya utafiti kwa moyo mkunjufu na akili iliyofunguka, utagundua kuwa Maandiko yaliyovuviwa katika kitabu cha Mwanzo yamesharabu na kuthibitishwa katika sayansi katika njia tofauti tofauti, na kuona ushahidi zaidi ulikuwepo kwa wakati wote. Angalia usinaswe umeketi katikati ya uzio baina ya Mungu na dhana ya mageuzi.

**Jack Wilkie anafanyakazi kama mmoja wa wahariri wa Jarida la “Think”, lililochapishwa na Focus Press huko Franklin, Tennessee, Marekani. Makala hii hapo mwanzoni ilichapichwa katika jarida hilo.**

# Ufanye Bidii Katika Kusoma

Jimmy Clark

***"…hata nitakapokuja, ufanye bidii katika kusoma…"*** (1Timotheo 4:13). Hii nasaha fupi inavutia kutafakari. Paulo hakueleza bayana nini hasa cha kusoma. Ingawa hilo linaweza kuongozwa na kanuni ya Mungu ya haki na maadili. Kusoma kunaunganisha maneno ***"kuonya"*** na ***"mafundisho"*** ( 1Timotheo 4:13). Zingatia baadhi ya mawazo kuhusu kusoma, hasa inavyohusiana na Biblia

**Mawasiliano Yaliyoandikwa Ni Faida**

Ni kweli kwamba matakwa ya Mungu yapo katika mfumo wa maandishi ambao una umuhimu mkubwa katika kuonya na kufanya bidii katika kusoma. Paulo alimwandikia Timotheo katika barua nyingine ***"kila andiko, lenye pumzi ya Mungu , lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema"*** (2 Timotheo 3:16-17). Paulo aliwaandikia ndugu wa Efeso ***"ya kwamba kwa kufunuliwa nalijulishwa siri hiyo, kama nilivyotangulia kuandika kwa maneno machache. Kwa hayo myasomapo, mtaweza kuutambua ufahamu wangu katika siri yake Kristo."*** (Waefeso 3:3-4).

Ni hakika kwamba jambo lililo katika rekodi ya kimaandishi linafaida sana hasa tukiangalia maisha ya Mordekai . ***"usiku ule mfalme hakupata usingizi; akaamuru aletewe kitabu cha maandiko ya taarifa, nayo yakasomwa mbele ya mfalme. Ikaonekana kuwa imeandikwa ya kwamba mordekai aliwachongea Bigthana na Tereshi, wasimamizi wawili wa mfalme, katika hao waliolinda mlango, waliotaka kumtia mikono mfalme Ahasuero".*** ( Esta 6: 1-2).

## Mawasiliano Yaliyoandikwa Ni Ya Kuhakikika

Pindi maneno yanapokuwa yamewekwa kwenye karatasi, kuna kuwa na uwezekano wa kurejea katika mawasiliano hayo halisi kama kukiwepo na changamoto. Watu wa Samaria walipingwa vikali kushiriki ujenzi mpya wa hekalu ndani ya Yerusalemu katika kipindi cha Zerubabeli. Baada ya kazi kusimamishwa kwa amri ya waraka wa mfalme Artashasta ( Ezra 4:23) na manabii Hagai na Zekaria walitabiri kwa Wayahudi kuendelea na kazi ( Ezra 5:1), kuliibuka upinzani juu ya kuendelea kufanya kazi (Ezra 5:3-5). Wakati uchunguzi ulipohitajika kwa ajili ya kuangalia madai kwamba Dario aliamuru kuendelea kwa kazi ya ujenzi, rekodi ya maandishi ilipatikana iliyoonesha amri iliyowekwa na Dario. Maelekezo yakawa ***"iacheni kazi hii ya nyumba ya Mungu, msiizuie, waacheni liwali wa Wayahudi, na wazee wa Wayahudi, waijenge nyumba hii ya Mungu mahali pake."*** (Ezra 6:7). Mawasiliano ya kimaandishi yalitoa uthibitisho wa ukweli kuonekana. Hivyo, inapaswa kuchunguza katika kusoma Maandiko ya Mungu kwa madai yote yanayotolewa na watu (Matendo 17:11). Mungu anawataka watu kuthibitisha mambo yote ( 1 Watheselonike 5:21).

## Mawasiliano ya Kimaandishi ni Nguvu

***"maana neno la Mungu li hai, tena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo"*** (Waebrania 4:12). Petro aliandika ***"walakini nitajitahidi, kwamba kila wakati baada ya kufariki kwangu mpate kuyakumbuka mambo hayo"*** (2 Petro 1:15). Rekodi ya kimaandishi huishi hata mtu akifa. Yesu alitumia Maandiko kupingana na majaribu ya Shetani (Mathayo 4:4,7,10). Shetani anajua nguvu ya Maandiko ya Bwana ***"…lenye uzima, lidumulo hata milele"*** (1 Petro 1:23). Litafariji moyo wenye huzuni ( 1 Wathesalonike 4:18). Litatekeleza matakwa ya Mungu ( Isaya 55:11).

**Jimmy Clark ni Mhuburi wa Kanisa la Kristo la Bethel ndani ya Athens, Alabama, Marekani.**

# Je! Ni Kweli Biblia Inafundisha Hivyo?

Neal Pollard

Huenda ushawahi kuwa na kicheko cha chinichini juu ya **Maandiko ya kidohani,** hayo mambo yanaonekana kama vile au tunafikiri kwamba yapo ndani ya Biblia lakini hayapo (Kwa mfano., "fanya dhamiri yako iwe mwongozo wako," " kukiri ni kuzuri kwa ajili ya nafsi" au kazi nzuri kwa njia ya ajabu"). Si jambo la kufurahisha pindi mioyo yetu na akili zetu inapokuwa haijalindwa sawasawa dhidi ya mwalimu au mhubiri ambaye anatangaza jambo fulani kama ni la kibiblia na kumbe sio. Inaweza kuwa mtu fulani ambaye anatangaza kitu kinachoonekana kukubalika na Mungu ambacho Biblia inafundisha kuwa hakikubaliki na Mungu. Inaweza ikawa mtu fulani anatetea kwamba kitu fulani lazima kiaminiwe au kifanyike, na wakati Biblia haikubaliani nacho.

Hata hivyo, Mungu amemfanya kila mmoja wetu kuwa na wajibu wa kujua mapenzi yake (Mungu). Tunajidanganya wenyewe na nafsi zetu hasa pale tunapo mruhusu mwalimu au mhubiri kutulazimisha jinsi gani tunapaswa kuhisi au kufikiri kuhusu mada iliyotolewa. Sisemi kuwa tunapaswa kuwa watu wa kushuku au tusioamini. Badala yake nasema tuwe kama Waberoya. Moja kati ya vitu vyenye guvu sana, maelezo chanya yaliyotolewa na kundi la watu inasemwa kuhusu wao katika Matendo 17:11 ***"watu hawa walikuwa waungwana kuliko wale wa Thesalonike, kwakuwa walilipokea lile neno kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo."*** Bila shaka umewahi kusoma kifungu hicho, lakini Roho Mtakatifu alisema nini kuhusu wao?

## Walisifika Kwa Uzuri

Walikuwa waungwana. Angalia ilianzia hapa. Yote mazuri yaliyosemwa kuhusu wao yaliaanza na mtazamo wao chanya. Yesu

aliwasifu watu wenye njaa na kiu ya haki (Mathayo 5:6). Hawa watu walijaliwa kulipokea Neno la Mungu.

## Walisifika Kwa Kuwa Na Shauku

Kinyume cha hili ni hali ya kutojali na kuwa tofauti. Waberoya walikuwa ni **wapokeaji wa Neno**. Walikuwa watu wa kushika, na wenye shauku ya kujua Neno la Mungu. Biblia, kutoka ukurasa hadi ukurasa. Inajitangaza kuwa ni ujumbe wa wokovu. Je, haistahili kuwa shauku yetu kubwa?

## Walisifika Kwa Uchunguzi

Waberoya hawakuwa wakosoaji, sio wanafunzi wajinga. Walikuwa wakimsikiliza mmoja kati ya Wakristo mashuhuli kihistoria, lakini bado waliendelea kuchunguza Maandiko na kile alichokisema. Kila mtu anayedai kuwa ni mhuburi wa Neno la Mungu anastahili kuhakikiwa kwa kiwango kama hicho.

## Walisifika Kwa Kujitoa Kila Siku

Waberoya hawakuridhika kusubiria darasa lingine la Biblia au hotuba. Kila siku walijitoa katika kutafakari maneno Matakatifu ya Mungu! Je, hakuna mambo unayohisi kulazimika kuyafanya kila siku (kula, kulala, kuswaki, kuangalia mitandao ya kijamiii kama vile facebook)? Tunathibitisha kwa Mungu kuwa tunajali kuhusu baraka ya kuwa na uhusiano pamoja naye kwa kutokuacha kumhusisha kwa uaminifu, akili yake iliyofunuliwa na shauku ambayo pekee tunaipata katika Neno lake!

Tunawezaje kujua kama jambo fulani ni imani tu ya mtu au ni amri ya Mungu? Tunajuaje kwamba fundisho jipya ni la kweli au la uwongo? Usitosheke kumfanya mtu fulani awe ndiye chanzo chako pekee cha kupima hilo! Kuwa Mberoya! (Waefeso 4:14).

**Neal Pollard ni Mhubiri wa Kanisa la Krist la Bear-valley huko Denver, Colorado, Marekani.**

# Kile Biblia Inachofundisha Kuhusu Yenyewe – Ni Hitimisho

Paul Holland

Paulo na Sila walipokuwa wakisafiri katika safari ya pili ya Paulo ya umisheni, walipita Thesalonike (Matendo 17) mpaka katika mji wa Beroya. Wakati akiwa Thesalonike, Paulo aliwafundisha Wayahudi, kwamba Yesu ndiye Masihi aliyeahidiwa, akihojiana nao ***"…kwa maneno ya maandiko sabato tatu, akiyafunua na kuwaeleza ya kwamba ilimpasa Kristo kuteswa, na kufufuka katika wafu; na ya kwamba, Yesu huyu ninayewapasha ninyi habari zake ndiye Kristo."*** (17:2-3). Paulo alijua kwamba Wayahudi waliwekeza sana katika Biblia yao (kwetu Agano la Kale), alihitaji kuonesha kwa usahihi kuwa Yesu ndiye Mwokozi.

Paulo alikuwa na mafanikio kwa kiwango fulani huko Thesalonike miungoni mwa Wayahudi na Mataifa, lakini Wayahudi, kama kikwazo, walikuwa na wivu (angalia mwitikio wao haukujikita katika Maandiko wala katika hoja) na kuishia kuwatoa nje ya mji Paulo na Sila. Kufikia hatua hiyo, wakaenda Beroya.

Luka aliandika kwamba Wayahudi wa Beroya walikuwa ***"waungwana"*** sana kuliko Wayahudi wa Thesalonike. Kitenzi kilichotafsiriwa "waungwana" kinamaanisha, "utayari wa kujifunza na kuthamini jambo fulani kwa haki" (Louw-Nida). Nadhani kwamba Paulo alichokifanya Beroya kilikuwa kitu kile kile alichokifanya Thesalonike (aya ya 2 – 3), lakini Wayahudi wa Beroya walikuwa tayari kufunua Biblia zao ***"kwa uelekevu wa moyo, wakayachunguza maandiko kila siku, waone kwamba mambo hayo ndivyo yalivyo."*** (mst. 11).

Kwa bahati, ikiwa sisi, kama wahubiri, tunataka makusanyiko yetu yawe kama waungwana hawa, basi tunahitajika kuwatia moyo, kuwaruhusu, na kusisitiza kwamba wayachunguze Maandiko ili waone

kama kile tunachokisema ni sahihi. Kwa maneno mengine, unapohubiri usitamke haraka-haraka kiasi kwamba wasikilizaji hawawezi kuandika somo hilo. Usinukuu vifungu vingi kiasi ambacho wasikilizaji wetu wakachanganyikiwa, tunatakiwa kutafsiri vifungu sawasawa kutoka katika muktadha wake. Katika hotuba yako wafanye wafunue Maandiko na waruhusu waone na kusoma vifungu wao wenyewe.

Kwa nini? Kwa sababu Biblia inafundisha, kama Wayahudi na Paulo walivyoonesha, kwamba yenyewe ina Neno la mwisho katika dini yo yote au mhusika ye yote wa kiroho. Kevin DeYoung, katika kitabu chake *Taking God at His Word* (Mpeleke Mungu katika Neno Lake), aliandika kwamba, Waberoya walikuwa waungwana kwa sababu, "walikuwa wanyenyekevu katika Maandiko. Wangeweza kukubali jambo jipya kama jambo hilo lingeungwa mkono na Maandiko. Walikuwa tayari kumfuata Kristo katika maisha yao yote, ingawa walikuwa katika mchakato wa kuyatii Maandiko." (uk. 75). Wamekuwa ni kielelezo bora na kinachotufaa leo!

Kuna utengano na utofauti miungoni mwa wanaojiita Wakristo, Wakatoliki na Waothodoksi, Waprotestanti wenye msimamo wa wastani na wale wanoitwa Waprotestanti wenye msimamo mkali. Kisha wapo Wakristo wanaolifuata Agano Jipya. Msingi wa utofauti wa imani zao ni imani yao na wanavyoyatumia Maandiko. Mamlaka yako yapo wapi? Je! Ni Papa? Wahenga? Utamaduni wa leo? Itikadi yenye kuheshimika? Au ni Agano Jipya la Yesu Kristo pekee?

Neno la Mungu lipo namna hiyo, ni **Neno la Mungu**. Tunawezaje kulipuuzia? Kuongeza? Kulibadilisha? Kupunguza? Tutahukumiwa kwa Neno la Kristo (Yohana 12:48), na hilo ndilo la mwisho!

**Paul Holland ni mhubiri wa Injili, anafanya kazi na Kanisa la Kristo Swartz Creek huko Swartz Creek, Michigan, Marekani.**

# Wokovu Wa Kipekee Wa Milele

Owen D. Olbricht

"Nimeokolewa; nimetakaswa, na sitaweza kupotea. Siendi kanisani!" Haya yalikuwa majibu aliyonipa kijana niliyemwalika kunisikiliza nikiongea katika kanisa la Kristo wakati wa kampeni huko Finger, Tennessee. Hakika aliwaza kwamba ameokolewa na hatoweza kupotea.

## Kwa nini Aliamini Hivyo?

Inaweza ikawa aliamini mafundisho "ukiokolewa, daima umeokolewa" kwa sababu alisikia mafundisho haya mara nyingi. Wahubiri wanaoshawishi hili wamekita fundisho lao katika aya mbali mbali za Biblia, kama vile Yohana 10:28. Yesu alisema kwamba wala hakuna mtu atakayewapokonya katika mkono wangu au katika ***"mkono wa Baba."*** Hii ni kweli, lakini Yesu hakusema **hatuwezi kuondoka mikononi mwao,** ila tu hakuna anayeweza kutupokonya mikononi mwao.

Paulo alifundisha kuwa vitu vingi hatarishi ***"havitaweza kututenga na upendo wa Mungu ulio katika Kristo Yesu Bwana wetu"*** (Warumi 8:35-39). Hili pia ni kweli, lakini Paulo hakuandika kwamba **hatutoweza kujitenga** na upendo wa Mungu.

Yuda aliwaandikia Wakristo, ***"jilindeni katika upendo wa Mungu"*** (Yuda 1:21), ikiwa na maana inatulazimu kufanya kitu fulani ili tubakie kwenye upendo wa Mungu. Yesu alisema ***"…kaeni katika pendo langu. Mkizishika amri zangu, mtakaa katika pendo langu;"*** ( Yohana 15:9-10). Yesu alifundisha kuwa upendo wa Mungu una masharti. Tutabakia katika pendo lake kama tutafuata amri zake.

Walio waovu na wasiomtii Mungu wanachukiwa na Mungu (Zaburi 5:5; 11:5), na ***"hatawapenda tena"*** (Hosea 9:15). Katika desturi inayofanana tunapenda ndizi lakini sio iliyoharibika, Mungu

anawapenda watu wote, isipokuwa walioharibika ambao hawatatenda mapenzi yake (Mathayo 7:21).

## Tawi Ndani Ya Yesu

Yesu alifundisha kwamba Yeye ni mzabibu na wafuasi wake ni matawi (Yohana 15:5). Ili sisi tuwe na maisha ya kiroho na kuzaa, lazima tubaki kwenye mzabibu ambao unamwakilisha Kristo. ***"kila tawi ndani yangu lisilozaa huliondoa"*** *(*Yohana 15:2). ***"Mtu asipo kaa ndani yangu, hutupwa nje kama tawi na kunyauka; watu huyakusanya na kuyatupa motoni yakateketea."*** ( Yohana 15:6).
Yesu ni mzabibu na uzima wa milele (1 Yohana 5:11). Ili tuwe na uzima wa milele katika Kristo (1 Yohana 5:11), Mtu lazima abatizwe katika Yeye (Warumi 6:4; Wagalatia 3:26-27), na kukaa ndani yake na kuzaa matunda.

Mtu aliye ndani ya Kristo ambaye hazai matunda atatupwa nje na Baba, inamaana atanyauka na kufa bila ya kuwa na maisha ya mzabibu (Yohana 15:2). Ikiwa mtu ye yote aliye ndani ya Kristo lakini hazai matunda hutupwa nje na kunyauka na kutupwa katika moto na kuteketea. Tawi (mtu) katika mzabibu (Yesu) linaweza kuondolewa katika uzima wa milele ulio katika Yesu na matokeo yake ni kunyauka na kutupwa katika moto na kuteketea.

## Uzima Wa Milele Katika Yesu

Tunao uzima wa milele katika Yesu (1 Yohan. 5:11) kama tukiingia kupitia Yeye na kuendelea kumwamini Yeye na kubaki kwakwe. Ikiwa hatutobaki kwake na kuzaa matunda tutatupwa katika moto na kuteketea. Mara baada ya kuokolewa, "daima umeokolewa" usemi huu utakuwa kweli ikiwa tu tutabaki katika Kristo na kuendelea kumtii ( Yohana 15:9-10).

**Owen D. Olbricht ni Mhubiri na mwandishi anaishi Sherwood, Arkansas, Marekani.**

# *Moyo Usio Na Toba*

Dwaight Fuqua

Akiwahubiria mataifa waliohitaji Injili, Paulo alizungumza kuhusu mioyo yao isiyoamini (Warumi 1:21, 28). Akiwahubiria Wayahudi waliohitaji Injili, alizungumza **“moyo usio na toba.”** Aliandika ***“bali kwa kadiri ya ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, wajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu”*** (Warumi 2:5).

“Wasiotubu” ina maana gani? Kutokana na mzabibu, neno alilolitumia Paulo (*amenanoetos*) likiwa na maana **“bila kubadili akili”**. Likimaanisha kutokuwa na hisia ya kujutia kuhusu dhambi zako. Lina matokeo mabaya kwa sababu “kutubu” (metanoeo) kunahusisha kubadili akili. Moyo mgumu matokeo yake ni akili isiyo na toba! Akili isiyo na toba matokeo yake ni maisha ya kutokujutia! Maisha ya kutokujuta matokeo yake ni hukumu! Paulo aliwambia wasiotubu, ***“wanajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira…”***

Ayubu akihubiri kutokutubu kwa mtu. Alisema ***“hawa ni katika hao waliouasi mwanga; Hawazijui njia zake, wala hawakai katika mapito yake.”*** (Ayubu 24:13). Mtazamo unaokubalika! Aliuliza, ***“… ni nani aliyejifanya kuwa mgumu juu yake, naye akafanikiwa?”*** (Ayubu 9:4). Swali linalokubalika!

Daudi akihubiri kuhusu kutokutubu kwa mtu. Alisema ***“Mungu ni mwamuzi mwenye haki, Naam, Mungu aghadhibikaye kila siku. Mtu asiporejea atauona upanga wake; Ameupinda uta wake na kuuweka tayari;”*** (Zaburi 7:11-12). Aliwauliza wasiotubu, ***“kwa nini kujisifia uovu, Ewe Jabari?”*** (Zaburi 52:1).

Sulemani akihubiri kuhusu kutokutubu kwa mtu. Aliwasilisha uhalisia wa kutisha. ***“Kwa kuwa nimeita, nanyi mkakataa; Nimeunyosha mkono wangu, asiangalie mtu; Bali mmebatilisha shauri langu, Wala hamkutaka maonyo yangu; Mimi nami nitacheka siku ya msiba wenu, Nitadhihaki hofu yenu ifikapo;Hofu yenu ifikapo***

***kama tufani, Na msiba wenu ufikapo kama kisulisuli, Dhiki na taabu zitakapowafikia. Ndipo watakaponiita, lakini sitaitika; Watanitafuta kwa bidii, wasinione. Kwa kuwa walichukia maarifa, Wala hawakuchagua kumcha Bwana. Hawakukubali mashauri yangu, Wakayadharau maonyo yangu yote. Kwa hiyo watakula matunda ya njia yao, Watashiba mashauri yao wenyewe."*** (Mithali 1: 24-34).

Sulemani alikuwa anaonesha kwamba "***ukaidi wao wenye fitina utawaangamiza.***" (Methali 11:3).

Isaya alihubiri kutokutubu kwa mtu. Alizungumzia jinsi gani Bwana aliwaita wale waliochoka wakapumzike, lakini hawakutaka kusikia. Aliwaita ***"mlio na moyo mshupavu"*** (Isaya 46:12) na **"ukaidi"** *(Isaya 48:4).* Pale alipowaita hawakuitika, na aliponena hawakusikia; bali waliendelea kutenda mabaya (Isaya 65:12).

Cha kusikitisha, siku hizi wengi hawajutii! Kama Esau, maana ***"hakuona nafasi ya kutubu"*** (Waebrania 12:17). Kama wale wa siku za Isaya (Isaya 6:9-10) na siku za Yesu (Mathayo 13:14-15). Hawakuelewa kwa mioyo yao, hawakuona kwa macho yao na hawakusikia kwa masikio yao ***"Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu, ukayafanye matendo ya kwanza. Lakini, usipofanya hivyo, naja kwako, nami nitakiondoa kinara chako katika mahali pake, usipotubu."*** (Ufunuo 2:5).

Mungu anawahurumia wale wasiotubu! ***"Sikilizeni neno hili, enyi watu wajinga msio na ufahamu; mlio na macho ila hamwoni; mlio na masikio ila hamsikii Je! Hamniogopi mimi? Asema Bwana;"*** (Yeremia 5:21-22, 23-25). ***"Au waudharau wingi wa wema wake na ustahimili wake na uvumilivu wake, usijue ya kuwa wema wa Mungu wakuvuta upate kutubu? Bali kwa kadiri ya ugumu wako, na kwa moyo wako usio na toba, wajiwekea akiba ya hasira kwa siku ile ya hasira na ufunuo wa hukumu ya haki ya Mungu,"*** (Warumi 2:4-5).

**Dwight Fuqua anatoa huduma ya Bwana kama Mhubiri kutoka Kanisa la Kristo la Findlay huko Sparta, Tennessee, Marekani.**

# Mwaliko Wa Mialiko

Patrick Morrison

Rafiki yangu mkubwa na mhubiri mwenzangu, ndugu Glenn Hitchcock, aliweka picha ya kuvutia ya chakula kidogo chenye radha katika ukurasa wake wa Facebook, siku moja nikaona kwamba inastahili na mimi kuishiriki. Wakati mmoja, kuna mtu alimwandikia Emily Post, huenda ni moja kati ya wataalam maarufu na mashuhuri wa dunia katika somo la tabia njema. Muhitaji aliuliza swali hili: “Ikiwa mtu alitakiwa kupokea mwaliko kutoka Ikulu, lakini alikuwa na jukumu hapo nyuma kidogo, je, kuna hatua gani za kuchukua ili kushughulika na hilo?” Mrs. Post alijibu, “Kwa kawaida mwaliko wa Ikulu huvunja shughuli zingine zote.” Unaweza kupata picha ya kupata mwaliko wa Ikulu ili kuhudhuria tukio fulani? Nadhani wengi wetu, bila ya kujali uhusiano wa kisiasa, tungechukulia kuwa ni moja kati ya heshima ya juu katika maisha yetu kupokea mwaliko wa namna hiyo! Nabashiri kwamba tungefanya kila kitu ili kuweka sawa kalenda zetu na kupanga upya mipango yetu ili tu tuweze kuufanikisha mwaliko huo. Bila shaka Mrs. Post alichomaanisha ni, mtu ye yote asingeihesabu shughuli yake aliyokuwa nayo kuwa ni muhimu kuliko kukubali mwaliko wa Ikulu!

Mwaliko wa Ikulu hautoshi kulinganisha na mwaliko tulioupokea kutoka kwa Bwana wetu Yesu Kristo. Muumba wa vitu vyote tunavyoviona na sisi sote, Mpaji wa roho zetu, na anayetufanya tunaishi, Naye ndiye Dhabihu kwa dhambi zetu, Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana, Tumani la uzima baada ya maisha haya na Mhukumu wa dunia yote ametualika katika meza yake ya chakula! Nani awezaye kuona kuwa shughuli yake ni muhimu kuliko mwaliko huu? Lakini bado, wapo watu ambao hutoa kila aina ya visingizio kwa nini hawawezi kuhudhuria.

***“Akamwambia, Mtu mmoja alifanya karamu kubwa akaalika watu wengi, akamtuma mtumwa wake saa ya chakula awaambie wale walioalikwa, Njoni, kwa kuwa vitu vyote vimekwisha kuwekwa***

***tayari. Wakaanza wote kutoa udhuru kwa nia moja. Wa kwanza alimwambia, Nimenunua shamba, sharti niende nikalitazame; tafadhali unisamehe. Mwingine akasema, Nimenunua ng'ombe jozi tano, ninakwenda kuwajaribu; tafadhali unisamehe. Mwingine akasema, Nimeoa mke, na kwa sababu hiyo siwezi kuja. Yule mtumwa akaenda, akampa bwana wake habari ya mambo hayo. Basi, yule mwenye nyumba akakasirika, akamwambia mtumwa wake, Toka upesi, uende katika njia kuu na vichochoro vya mji, ukawalete hapa maskini, na vilema, na vipofu, na viwete. Mtumwa akasema, Bwana, hayo uliyoagiza yamekwisha tendeka, na hata sasa ingaliko nafasi. Bwana akamwambia mtumwa, Toka nje uende barabarani na mipakani, ukawashurutishe kuingia ndani, nyumba yangu ipate kujaa. Maana nawaambia ya kwamba katika wale walioalikwa, hapana hata mmoja atakayeionja karamu yangu.”*** (Luka 14:16-24).

Mwaliko wa Yesu unataka mwitikio wa haraka. Unataka kwamba tuwe na muda kwa ajili ya bufee aliyoiandaa kwa ajili ya wote watakao mjia. Hakuna kitu cho chote hapa duniani kilicho cha muhimu au cha dharula kuliko kuitikia mwaliko wa Mbinguni! Lakini bado, watu wengi wanauchukulia mwaliko huu kama jambo lisilo na umuhimu. Utafutaji wa pesa na vitu vingine kumeteka sana mioyo ya watu wengi kiasi kwamba wako tayari kuachana na mwaliko wa kuketi pamoja na Yesu! Wengine wanauchukulia mwaliko huu kuwa ni muhimu, lakini si muhimu vya kutosha kiasi cha kuutendea kazi kwa haraka. Wengine wanaonekana kuutazamia mwaliko wa Yesu kama jambo fulani bora lijalo. Wengine wanadhani kwamba mwaliko huu unaweza kuitikiwa muda wo wote, kwamba siku zote bufee litakuwa limeandaliwa kwa hiyo wanaweza kuja wakati wo wote.

Utafika wakati ambapo dirisha la fursa kwa ajili ya kalamu kubwa iliyoandaliwa na Bwana litafungwa.  Hii haimaanishi tu kukosa fursa ya kuketi katika meza ya Yesu; inamaanisha kuishi maisha yote ya umilele mbali na mtu aliyetununua ili tuje kushereheka pamoja naye katika maisha ya umilele! Mwaliko wako tayari umetumwa. Hakuna mtu

awezaye kuukubali au kuukataa kwa niaba yako. Nina kusihi uukubali mwaliko huu haraka sana, kwa maana unaweza usiwe na fursa nyingine!

**Patrick Morrison ni mhubiri wa kanisa la Kristo Sixth Avenue huko Jasper, Alabama, Marekani.**

# Maandiko ya Kutafakari

Shadrack S. Msambaza

**(Mhubiri 1:1-2, 14)**"Mhubiri asema, Ubatili mtupu, ubatili mtupu, mambo yote ni ubatili. Mtu ana faida gani ya kazi yake yote aifanyayo chini ya jua? **14** Nimeziona kazi zote zifanywazo chini ya jua; na, tazama, mambo yote ni ubatili na kujilisha upepo." (**Mhubiri 2:1-11)** "Nikauambia moyo wangu, Haya, nitakujaribu kwa njia ya furaha basi ujifurahishe kwa anasa. Na tazama, hayo nayo yakawa ubatili. Nikasema juu ya kicheko, Ni wazimu; na juu ya furaha, Yafaa nini? Moyoni mwangu nikapeleleza jinsi ya kuuburudisha mwili kwa mvinyo, na (moyo wangu ukali ukiniongoza kwa hekima) jinsi ya kushikana na upumbavu, hata niyaone yaliyo mema ya kuwafaa wanadamu, ili wayafanye hayo chini ya mbingu siku zote za maisha yao. Nikajifanyizia kazi zilizo kubwa; nikajijengea nyumba; nikajipandia mashamba ya mizabibu; nikajifanyizia bustani na viunga, na kuipanda humo miti yenye matunda ya kila namna; nikajifanyizia birika za maji, ya kuunyweshea mwitu mlimopandwa miti michanga. Nami nikanunua watumwa na wajakazi, nikawa na wazalia nyumbani mwangu; tena nikawa na mali nyingi za ng'ombe na kondoo, kupita wote walionitangulia katika Yerusalemu; tena nikajikusanyia fedha na dhahabu, na tunu za kifalme na za kutoka katika majimbo. Nikajipatia waimbaji, waume kwa wake, nao wale ambao wanadamu wanawatunuka, masuria wengi sana. Basi nikawa mkuu, nikaongezeka kupita wote walionitangulia katika Yerusalemu; pia hekima yangu nikakaa nayo. Wala sikuyanyima macho yangu cho chote yalichokitamani; wala sikuuzuia moyo wangu katika furaha yo yote; maana moyo wangu ulifurahi kwa sababu ya kazi yangu yote, na hii ilikuwa sehemu yangu katika kazi yangu yote. Kisha nikaziangalia kazi zote zilizofanywa kwa mikono yangu, na taabu yote niliyotaabika katika kuzitenda; na tazama, yote ni ubatili na kujilisha upepo, wala faida hakuna chini ya jua." **(Mathayo 16:26)** "Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? Au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake?"

# Tafuta Aya




1. Paulo alisema kwamba alikuwa____________kwa wote.( mst.19)
2. Kwa nini alifanya kile alichofanya kwenya swali la kwanza? (mst. 19)
3. Kwa Wayahudi, Paulo alikuwa________Kwa wale walio chini ya sheria, alikuwa kama chini ya________kwa wale wasio na sheria, alikuwa kama ___________(mst.20-21)
4. Je, Paulo alikuwa hana sheria? (mst. 21)
5. Paulo alisema yupo chini ya sheria ipi? (mst.21)
6. Paulo alisema kwamba alikuwa hali zote kwa watu wote. Kwa nini? (mst. 22)
7. Alifanya mambo yote kwa ajili ya_________( mst. 23)
8. Ni watu wangapi hupokea tuzo kwenye mbio? ( mst. 24)
9. Na kila ashindanaye katika michezo ni_____katika yote. Kwanini?(mst.25)
10. Kuna tofauti gani kati ya taji tunalolitafuta na taji wanalolitafuta wanariadha? (mst. 25)
11. Ni kwa jinsi gani Paulo alisema tunahitaji kukimbia? (Mst. 26)
12. Paulo aliutendea nini mwili wake? (mst.27)
13. Paulo alisema kwamba hata kama nimewahubiria wengine, kulikuwa bado na uwezekano wa yeye kupotea**.** **Kweli** au **Si kweli**. (mst. 27)

**(Angalia jalada la nyuma kwa majibu)**

“**19** Maana, ingawa nimekuwa huru kwa watu wote, nalijifanya mtumwa wa wote, ili nipate watu wengi zaidi. **20** Nalikuwa kama Myahudi kwa Wayahudi, ili niwapate Wayahudi; kwa wale walio chini ya sheria, nalikuwa kama chini ya sheria, (ingawa mimi mwenyewe si chini ya sheria), ili niwapate walio chini ya sheria. **21** Kwa wale wasio na sheria nalikuwa kama sina sheria, (si kwamba sina sheria mbele za Mungu, bali mwenye sheria mbele za Kristo), ili niwapate hao wasio na sheria. **22** Kwa wanyonge nalikuwa mnyonge, ili niwapate wanyonge. Nimekuwa hali zote kwa watu wote, ili kwa njia zote nipate kuwaokoa watu. **23** Nami nafanya mambo yote kwa ajili ya Injili ili kuishiriki pamoja na wengine. **24** Je! Hamjui, ya kuwa wale washindanao kwa kupiga mbio, hupiga mbio wote, lakini apokeaye tuzo ni mmoja? Pigeni mbio namna hiyo, ili mpate. **25** Na kila ashindanaye katika michezo hujizuia katika yote; basi hao hufanya hivyo kusudi wapokee taji iharibikayo; bali sisi tupokee taji isiyoharibika. **26** Hata mimi napiga mbio vivyo hivyo, si kama asitaye; napigana ngumi vivyo hivyo, si kama apigaye hewa; **27** bali nautesa mwili wangu na kuutumikisha; isiwe, nikiisha kuwahubiri wengine, mwenyewe niwe mtu wa kukataliwa.”

**KUMBUKA:** Katika aya hizi, tunaweza kasema Paulo aliweka kwanza miongozo kwaajili ya huduma yake. Falsafa yake ilikuwa ni kuitanguliza Injili kuliko mambo yake binafsi.Alikuwa tayari kubadili matamanio yake binafsi na kufutana desturi ya wengine ili awalete kwa Kristo. Hata hivyo, hiyo haimaanishi kwamba alifanya chochote ili afanane na wale aliokuwa anawafundisha. Kama jinsi sisi tulivyo daima alikuwa chini ya sheria ya Kristo. Muda mwingine watu wanatumia vibaya mistari hii kutetea matendo yao kwakudai kuendana na wale wanaojaribu kuwafundisha. Ingawa dhamira inaweza ikawa njema, siku zote lazima tukumbuke ya kuwa tupo chini ya sheria ya Kristo na kamwe usitafute kisingizio kwa sababu yeyote. Maisha yetu lazima mara zote yafuate sheria ya Kristo, na sio vinginevyo.

Mstari wa 27 ni mstari muhumu. Watu wengi wanaamini kwamba mara mtu anapokuwa ameokolewa, daima ameokolewa, bila kujali nini anaweza kufanya. Paulo kwa uwazi ameonesha kwamba hiyo Imani siyo sahihi. Paulo alihakikisha kwamba aliunidhamisha mwili wake na kuutiisha chini ya Kristo, kwasababu kama asingefanya hivyo basi angeweza kupoteza tunzo yake.matendo yake yote mema ambayo aliyafanya hakuweza kuishi katika mtindo wa Maisha ya uovu. Inaonekana baadhi ya watu leo hii wanafikiria kinyume. Maisha yao kwa uwazi hayafuati amri za Kristo, lakini bado wanaedelea kuhubiri au kufanya matendo mengine mema ya kikristo ambayo wanadhani diyo kuthibitisha wokovu wao. Ili tuvikwe taji, lazima tufuate sheria; hiyo ni kutii amri za Kristo. Kwakutembea katika nuruni, damu ya Kristo inaosha dhambi zetu (1 John 1:7).

# Kazi Ya Kipekee

Bob Plunket

Mtu mmoja alisema kwamba Alexander aliendelea zaidi na kutawala dunia. Kaisari alisonga mbele na kuwashinda maadui zake. Plato na Socrates walienda mbali wakitafuta maarifa. Columbas alienda mbali ili kugundua dunia mpya. Stanley alienda mbali kuipeleleza Afrika. Mashujaa wamekwenda mbali kuwatafuta maadui zao, huku wakikabiliwa na taabu, na kifo. Safari iliendelea kwa kuchunguza mikoa ya mbali ili kuona maajabu ya asili na mwonekano wa kazi za sanaa. Wahisani wameenda mbali katika ujumbe wa huruma.

Watu wa enzi hizi wameenda mbali na kupeleleza mwezi na kufika sehemu ya mbali nje ya dunia. Watu wamegundua mafuta chini ya bahari. Sasa hivi wameenda kwenye dunia ya hadubini kwa ajili ya gene na vinasaba

Hata hivyo, mgeni wa kipekee alitajwa katika mstari mmoja mfupi***:*** ***"… mwana wa Adamu alikuja kutafuta na kuokoa kile kilichopotea"*** (Luka 19:10). Hakuja kuitawala dunia bali kuiokoa. Hakuja kutafuta maarifa bali kugawa maarifa. Hakuja kutafuta dunia mpya, bali kugawa Maisha mapya. Hakuja kuwashinda maadui bali kuwavunja. Hakuja kutafuta hazina, bali kutujulisha sisi wapi tuwekeze hazina yetu. Hakuja kuilaani dunia, bali kuikomboa. Hakuja kuiharibu ardhi, bali kulijenga kanisa lake juu ya ardhi.

Ipi inapaswa kuwa kazi ya kanisa la Kristo la leo? Haipaswi kuwa kuwatafuta na kuwaokoa waliopotea? Kazi yetu sio kumpatanisha Kristo na ulimwengu, bali kuipatanisha dunia yetu na Kristo. Kazi yetu wala si kazi ya kukusanya tu maarifa ya kidini, bali badala yake ni kuitangaza Injili ya Kristo kwa walimwengu. Kanisa, kama Yesu, linapaswa kuwalisha walio na njaa, kuwasaidia wagonjwa na kuwatunza wajane na yatima, lakini lazima tusisahau kamwe ya

kwamba hili lilikuwa kwa ajili ya Kristo, na inapaswa kuwa na kwetu pia, kuwe na njia ya kuwaokoa waliopotea**. Mara nyingi, kanisa limekuwa likikwamishwa na ajenda ya kijamii na watu waliokufa kikamilifu, wamevikwa vizuri, lakini wamepotea**. Ikiwa kanisa halijihusishi na mahitaji ya kiroho ya walimwengu, nani atafanya? Kazi yake ni kazi yetu, ***"kutafuta na kuokoa kile kilichopotea"***

**Bob Plunket anahubiri katika kanisa kusanyiko la Colbert Heights huko Tuscumbia, Alabama, Marekani.**

## Onyo Kwa Mtume Tu Au Kwa Wakristo Wote?

Shadrack S. Msambaza

***"Maana, ijapokuwa naihubiri Injili, sina la kujisifia; maana nimewekewa sharti; tena ole wangu nisipoihubiri Injili!"*** (1 Wakorintho 9:16). Hapa inaonekana ni kana kwamba onyo hili lilimhusu mtume Paule peke yake, lakini je, Wakristo hawahusiki katika utumishi huu? Pengine mtu anaweza kusema kuwa si kila Mkristo mwenye uwezo wa kuhubiri. Hilo ni kweli, lakini je, hiyo inamaanisha kuwa hawezi kuhusika? Ieleweke ya kwamba, kazi ya kuhubiri Injili si ya mtu, bali ni kazi ya kanisa, ***"ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho; kwa kadiri ya kusudi la milele alilolikusudia katika Kristo Yesu Bwana wetu."*** (Waefeso 3:10-11). Je! Hii inaonekana kama ni kazi ya mtu mmoja?

Kanisa linapaswa kukaa na kupanga mikakati ya namna ya kutekeleza agizo hilo, likisha pata njia ndipo huenda hatua ya pili ya kutuma mtu au watu kwa niaba ya wote. Hivyo, kanisa hilo litawajibika kumhudumia au kuwahudumia watu hao kwa muda wote wa kazi hiyo (Warumi 10:14-15; 1 Wakorinth 9:7-14). Kwa hiyo, onyo lile halikuwa kwa mtume peke yake bali kwa kanisa zima.

### KanIsa

# Kundi Moja na Mchungaji Mmoja

Cliff Holmes

***"Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja."*** (Yohana 10:16). Kuna hoja bora nne katika Maandiko.

## Kondoo Wengine, Ambao si wa Zizi Hili

Nani alikuwa kondoo katika zizi la Yesu Kristo, Mchungaji Mwema? Wanafunzi wake, mitume na wote waliokuja kwake kutafuta wokovu kwa ajili ya dhambi, huzuni, majaribu, na dhiki. Kuna wengine wengi waliohitaji kuingizwa katika zizi la kondoo. Mataifa kumi na mbili au zaidi waliorodheshwa kama wasikilizaji wa hotuba ya Petro siku ya Pentekoste, mbali na Wayahudi, Wagiriki, Mataifa, Warumi, na pia kwa ujumla na mataifa ya kipagani. Leo hii kuna makundi 34,000 na madhehebu ambao wanadai kuwa na aina fulani ya muungano na Kristo. Wameunda makusanyiko million 3.5, na kudai kuwa na waumini billion 1.9. Kuna vikundi vinafundisha mafundisho mabaya ambayo kamwe Kristo asingeyakubali. Mamillioni bado wanaabudu miungu ya uwongo, au hata Shetani mwenyewe, lakini Yesu anasema ***"na hao nao imenipasa kuwaleta"***

## Na hao nao imenipasa kuwaleta

Yesu aliposema ***"na hao nao imenipasa kuwaleta"*** je, ni mtu ye yote? Ndiyo, ni mapenzi yake kwamba watu wote watubu na kuokolewa na dhambi zao. Hii ni njia ya pekee ya hili kutokea ni kama wao ***"watasikiliza sauti yangu"*** alisema Yesu. Jinsi gani watamwamini yeye ambaye hawakuwahi kumsikia, watasikiaje bila mhubiri, na itakuwaje kama mhubiri hata kuja kuhubiri? Watasikilizaje sauti yake (Warumi 10:13-15)?

## Sauti Yangu Wataisikia

Mmoja lazima aje kuwa hiyo sauti. Katika Agizo lenye mpaka, Yesu aliwatuma watu kwa watu walipotea wa nyumba ya Israeli. Walienda, wakifundisha na kufanya miujiza mingi kama wasemaji (sauti ya Mchungaji), na wengi waliamini wakatubu. Baadaye, Yesu aliwapa wanafunzi wake Agizo Kuu, na upana wake kwetu sisi pia ***"enendeni ulimwenguni mwote, mkaihubiri Injili kwa kila kiumbe"*** (Marko 16:15). Nasi pia, tumeitwa, "kuisikiliza sauti yake" hii haikuwa tu ujumbe kutoka kwa Yesu; bali ilikuwa ni amri inayotakiwa kutekelezwa na Wakristo hata wa siku hizi.

## Kutakuwa na Kundi Moja na Mchungaji Mmoja

Tutakapoitikia wito, itatulazimu sisi sote **kufanya kazi na kufanya kazi vizuri.** Si tu **kamba** tutakuwa tumeifanya kazi hii vizuri, bali sisi sote tutakuwa kundi moja na Yesu atakuwa Ndiye Mchungaji Mmoja.

**Cliff Holmes ametumika kama mhubiri katika maeneo mbali mbali kwa miaka kadhaa, shemasi na kiongozi wa nyimbo huko Anakaa huko Decatur, Alabama, Marekani.**

Yohana 10:14-16

**"Mimi ndimi mchungaji mwema; nao walio wangu nawajua; nao walio wangu wanijua mimi; kama vile Baba anijuavyo, nami nimjuavyo Baba. Nami nautoa uhai wangu kwa ajili ya kondoo. Na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili; na hao nao imenipasa kuwaleta; na sauti yangu wataisikia; kisha kutakuwako kundi moja na mchungaji mmoja."**

Yohana 10:9

**"Mimi ndimi mlango; mtu akiingia kwa mimi, ataokoka; ataingia na kutoka, naye atapata malisho."**

# Jambo La Kusisimua

John Gipson

Nikiwa kijana, nilisikiliza hotuba za Winston Churchill katika redio katika kipindi cha Vita Kuu ya Pili ya Dunia, na nilivutiwa sana na hotuba hizo. Baadaye, nikahitaji zaidi kanda za hotuba zake maarufu, kwa mara nyingine, nilivutiwa sana. Mtu yule alijua jinsi ya kuwashikiria wasikilizaji bila ya kamba. Alitumia maneno kama jenelali anavyotumia vikosi vyake katika uwanja wa vita. Ilikuwa ni jambo lenye nguvu.

Ilikuwa hivyo hadi niliposoma wasifu wa Winston Spencer Churchill kutoka kwa William Manchester ambapo nilijifunza kuhusu wakili Mmarekani wa Kiairishi na mbunge wa bunge la Marekani Bourke Cockran, na hotuba zake zilizokuwa na msukumo kwa Churchill. Cockran alimshauri Churchill kwamba ajiepushe na kashfa, na kukuza mambo. Alisema “Watu wanachotaka kusikia ni ukweli, ni jambo la kusisimua, zungumza ukweli mrahisi.” Plato, karne nyingi kabla Cockran, alisema, “Hakuna jambo la kupendeza kama kusikia au kuzungumza ukweli.”

Yesu alikuja ulimwenguni akinena juu ya kweli, na watu walimsikia vizuri. Hata Maafisa waliotumwa kumkamata walirudi bila ya kutimiza kazi yao. Walieleza nini? ***“…Hajanena kamwe mtu ye yote kama huyu anavyonena.”*** (Yohana 7:46).

Baadaye, mitume wa Yesu walishitakiwa kwa kuipindua dunia. Jambo hili lilifanikishwaje? Si kwa nguvu za kijeshi, akili za kisomi au ujanja wa kisiasa, bali kwa njia ya ukweli, ukweli rahisi. Katika dunia yetu, kuna kulaghaika sana na mianga, uzuri, makelele na mijongeo, lakini hakuna kilicho cha kusisimua kuliko kuzungumza ukweli. ***“Tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.”*** (Yohana 8:32).

**John Gipson anafanya kazi na kanisa la Kristo Windson huko Little Rock, Arkansas, Marekani.**



# Tafuta Katika Biblia

Martha Rushmore

## Vuka

1. Mke wa Lutu aligeuka nguzo ya nini kwa kugeuka nyuma? (Mwanzo 19:26).
2. Jina gani ambalo Ibrahimu na Sarah walimpa mtoto wao? (Mwanzo 17:19).
3. Ni watu wangapi walioondoka katika miji ile miwili? (Mwanzo 19:15).
4. Mtoto wa kwanza wa Ibrahimu aliitwa nani? (Mwanzo 16:11).
5. Familia ya Lutu waliambiwa wasiangalie wapi? (Mwanzo 19:17).
6. Mungu aliangamiza Sodoma na Gomora kwa dhambi gani? (Mwanzo 19:5).
7. Sarah alikuwa wapi wakati wanaume watatu walipokuwa wakimwambia Ibrahimu kuwa Sara atapata mwana? (Mwanzo 18:9)
8. Sarah angekuwa mama wa kitu gani? (Mwanzo 17:16)
9. Abramu alipewa jina gani jipya na Mungu? (Mwanzo 17:5)
10. Sarai alipewa jina gani jipya na Mungu? (Mwanzo 17:15)
11. Mungu alianzisha nini baina Yake na Ibrahimu (Mwanzo 17:7)
12. Ibrahimu alifanya nini pindi Mungu alipomwambia kuwa atakuwa baba? (Mwanzo 17:17)
13. Ni wanaume wangapi waliomtembelea Ibrahimu? (Mwanzo 18:2)
14. Mpwa wa Ibrahimu aliitwa nani? (Mwanzo 12:5)

# Mfano wa Kutoa katika Agano Jipya

Lance Mosher

Nimekutana na watu wengi ambao wamekatishwa tamaa na viongozi wao wa kidini na mkazo wa **"zaka"** katika makanisa yao. Nadhani hata mimi ningekatishwa tamaa pia, kama ningekuwa chini ya viongozi wa kidini ambao wanasisitiza kielelezo cha zaka, kwa kuwa zaka chini ya Kristo haipo.

Taifa la Israel lilipotolewa katika utumwa wa Misri kwa nguvu za Mungu, baada ya muda wakiwa jangwani, walipewa zawadi ya Nchi ya Ahadi. Baada ya kumiliki, kila kabila la wana wa Israeli walipewa urithi wa ardhi, isipokuwa kabila la Lawi. Kwa urithi huo wa ardhi ukaleta kazi za mavuno na kufuga wanyama. Badala ya urithi, Mungu aliwapa Walawi kazi ya msingi kabisa katika taifa, kuwahudumia Waisraeli kwa njia ya ukuhani. Wakiwa na kazi hiyo muhimu, hawakuwa na muda wa kushughulika na ardhi. Kwa hiyo, wakalazimika kulitegemea taifa zima kwa ajili ya kuishi kwao, ambapo kulitokana na mfumo wa zaka aliouweka Mungu (Hesabu 18:21-24).

Leo viongozi wengi wa kidini wanafundisha kuhusu zaka. Pamoja na hayo, inahitajika tutambue mambo mawili ya msingi kuhusu zaka kwa mujibu wa Biblia. (1) Zaka ya Kiisraeli haikuhusu pesa, ilihusu mazao ya chakula. (2) Amri ya zaka ilitolewa na kuwahusu taifa la wana wa Israeli pekee chini ya sheria ya Musa. Mambo ya Walawi 27:30-34 tunasoma; ***"Tena zaka yote ya nchi, kama ni mbegu ya nchi, au kama ni matunda ya nchi, ni ya Bwana; ni takatifu kwa Bwana. Na kama mtu akitaka kukomboa cho chote cha zaka yake, ataongeza sehemu yake ya tano juu yake. Tena zaka yote ya ng'ombe, au ya kondoo, kila apitaye chini ya fimbo; sehemu ya kumi watakuwa ni watakatifu kwa Bwana. Hataangalia kwamba ni mwema au kwamba ni mbaya, wala hatambadili; na kama akimbadili na yo yote, ndipo wote wawili, huyo na huyo waliobadiliwa watakuwa ni watakatifu; hatakombolewa. Haya ndiyo maagizo, Bwana aliyomwagiza Musa kwa ajili ya wana wa Israeli katika mlima wa Sinai."***

Hizi ndizo amri ambazo Bwana alimwamuru Musa kwa ajili ya wana wa Israeli katika Mlima Sinai.

Maadam ukuhani wa Kilawi bado ulikuwa hai, sheria ya zaka bado ilikuwa hai. Hata hivyo, Kristo alikuja na Agano Jipya, ambalo lilifanya Agano la kwanza kuwa kuukuu (Waebrania 8:6-13). Sasa, Kristo anatumika kama Kuhani Mkuu, sio kulingana na utaratibu wa Haruni na Walawi, bali kulingana na utaratibu wa Melkizedeki (Waebrania 5 – 7). Waebrania 7:12, inasema, ***"Maana ukuhani ule ukibadilika, hapana budi sheria nayo ibadilike."*** Kwa kuwa Wakristo hawapo chini ya ukuhani wa Kilawi, hakuna sababu ya mfumo wa zaka kuendelea kuwepo. Badalayake, sheria ya utoaji imebadilika na mabadiliko ya ukuhani. Kristo anatumika kama Kuhani Mkuu, na kila Mkristo anatumika kama kuhani katika taifa la kiroho la Mungu (1 Petro 2:4-10).

Kristo alikuja duniani na akaleta kila kitu (Marko 10:41-45). Sisi tunaotaka kuwa kama Kristo ni lazima tuwe na nia ileile, kwa kuwa tunafahamu kwaba, baraka yo yote tunaipokea kutoka kwa Mungu (Yakobo 1:16-18). Sababu ya Mungu kutubariki sana ni ili tuwe ***"…na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema;"*** (2 Wakorintho 9:8). Hilo linahusiana vipi na kutoa? Rafiki aliuliza kuhusu hilo kwa mtindo huu, "Kwa nini Mungu anahitaji pesa?" Ukweli ni kwamba haitaji! Hata hivyo, amewaagiza watu wake ***"Enendeni ulimwenguni pote mkahubiri Injili kwa kila kiumbe."*** (Marko 16:15). Mungu haitaji pesa, lakini watu wake wanahitaji pesa ili waweze kuieneza Injili (1 Wakorintho 9:9-14). 1 Wakorintho 9:14 inasema, ***"Na Bwana vivyo hivyo ameamuru kwamba wale waihubirio Injili wapate riziki kwa hiyo Injili."***

Nyongeza katika kutoa michango ni ili kueneza Injili, pia Wakristo wanatakiwa kutoa michango kwa ajili ya wahitaji. Matendo 11:27-30 inasema; ***"Siku zizo hizo manabii walitelemka kutoka Yerusalemu hata Antiokia. Na tulipokusanyika akasimama mmoja wao, jina lake Agabo, akaonyesha kwa uweza wa Roho Mtakatifu kwamba njaa kubwa itakuja karibu katika dunia nzima, nayo ikatukia katika siku za Klaudio. Na wale wanafunzi, kila mtu kwa kadiri ya alivyofanikiwa, wakaazimu kupeleka msaada kwa ndugu zao waliokaa Uyahudi. Wakafanya hivyo, wakawapelekea wazee kwa mikono ya Barnaba na Sauli."***

Kwa wale walio katika Agano Jipya, wakimfuata Roho wa Kristo, kutoa kulikuwa ni baraka. Kwa hiyo inapaswa kuwa hivyo kwa Wakristo wa leo pia. Angalia, kile ambacho 1 Wakorintho 16:1-2 inasema, ***"Kwa habari ya ile changizo kwa ajili ya watakatifu, kama vile nilivyoamuru makanisa ya Galatia, nanyi fanyeni vivyo. Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake; ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja;"*** ongeza 2 Wakorintho 9:6-8, twasoma, ***"Lakini nasema neno hili, Apandaye haba atavuna haba; apandaye kwa ukarimu atavuna kwa ukarimu. Kila mtu na atende kama alivyokusudia moyoni mwake, si kwa huzuni, wala si kwa lazima; maana Mungu humpenda yeye atoaye kwa moyo wa ukunjufu. Na Mungu aweza kuwajaza kila neema kwa wingi, ili ninyi, mkiwa na riziki za kila namna siku zote, mpate kuzidi sana katika kila tendo jema;"***

Katika Agano la Kale zaka, iliwekwa bayana kuwa ni moja ya kumi ya chakula. Utoaji katika Agano Jipya, zaka haipo. Badalayake, ukichanganya haya yote kwa pamoja, Wakristo wanatakiwa kutoa kwa kadiri ya kufanikiwa kwao, na kama walivyokusudia mioyoni mwao, kila siku ya kwanza ya juma, kwa ukarimu, kwa moyo mkunjufu, sio kwa huzuni na wala si kwa lazima. Ni baraka kutoa pindi tunapotambua kuwa mali zetu ni za Bwana, ukiachana na hilo, tunapotoa zaidi ndivyo Injili inavyohubiriwa zaidi. Tunaweza kujifunza kutoka kwa Wakristo mafukara wa Makedonia, ambao waliweza kutoa sana, kwa sababu, ***"…kwanza walijitoa nafsi zao kwa Bwana;"*** (2 Wakorintho 8:1-5). Pata hamasa kutoka katika Luka 6:38, ***"Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa."***

**Lance Mosher anafanya kazi na kanisa la Bwana huko New Zealand.**

**I T A K U W A J E N I S I P O T O A ?**

Shadrack S. Msambaza

1. Utakuwa hujatimiza wajibu wako kama Mkristo (1 Kor. 16:1-2).
2. Hutofanikiwa kiuchumi (Matendo 20:35).
3. Utajiweka kwenye hatari ya kupotelea katika dhambi (Mw. 4:6-7).

# Imani na Kuona

**Joseph Ezenweze**

**Paulo** aliandika, ***"Basi siku zote tuna moyo mkuu; tena twajua ya kuwa, wakati tuwapo hapa katika mwili, tunakaa mbali na Bwana. (Maana twaenenda kwa imani, si kwa kuona.) Lakini tuna moyo mkuu; nasi tunaona ni afadhali kutokuwamo katika mwili na kukaa pamoja na Bwana"*** (2 Wakorintho 5:6-8). Paulo alisema kwamba Wakristo wanaoishi ulimwenguni hawapo kwa Bwana. Katika hali yao ya kibinadamu hawajaenda katika sehemu iliyoandaliwa kwa ajili ya watakatifu (Mathayo 25:46, Ufunuo 14:13).

Kwa vile hawapo kwa Bwana, sisi tuliopo katika ubinadamu tunatembea kwa imani, sio kwa kuona. Hiyo ina maana kwamba tunatakiwa kuamini katika Maandiko ya Bwana hata ingawa hatuna mawasiliano naye ya moja kwa moja. Hii haimaanishi kwamba tunatilia mashaka Neno la Mungu.

Paulo alijua kuwa Yesu ni Mkombozi hata ingawa hakumjua Kristo ***"katika mwili"*** (2 Wakorintho 5:16; 2 Timotheo 1:12). Yesu alikuwa mbinguni, haikumaanisha kuwa watu wa ulimwengu hawakujua kuwa yeye ni Kristo.

Kuna muda Imani na kuona vilienda sambamba. Watu walitembea kwa Imani kwa sababu ya kuona. Katika Yohana 20:29 tunapata kujua ***"Yesu akamwambia, Wewe, kwa kuwa umeniona, umesadiki; wa heri wale wasioona, wakasadiki".*** Tomaso aliamini ufufuo wa Bwana baada tu yeye binafsi kuonana ana kwa ana na Bwana (Yohana 4:39-42). Aliamini kwa sababu aliona.

Wengi kipindi cha huduma ya Bwana walimwamini kwa sababu ya vitu walivyoona na kusikia. Wengine, waliona wafu wakifufuliwa. Wengine, walishangazwa na mafundisho na mahubiri ya Bwana. Wengine, walivutiwa na miujiza iliyofanywa kipindi cha kanisa la mwanzo, na baadhi yao walitii Injili.

Leo hii, Mungu hafanyi miujiza yo yote kama alivyofanya katika siku za huduma ya Kristo na katika kipindi cha kanisa la awali (Waefeso 4:8-16; 1 Wakorimtho 13:13; Warumi 8:24). Leo hii, hatuwezi binafsi kushuhudia miujiza. Tunaweza kuwa na Imani kwa njia ya Neno la Mungu lililo rekodi miujiza (Yohana 20:30-31; Warumi 10: 17). Hivyo, ingawa Tomaso aliamini kwa kuona, sasa hivi tunaamini bila ya kuona (2 Wakorintho 5:7). Hata hivyo, siku inakuja ambapo Imani na kuona vitakuwa pamoja tena. Tunasoma katika 1 Yohana 3:2, ***"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo."***

Hatutaacha kuamini Maandiko ya Kristo mpaka pale tutakapo ***"…mwona kama alivyo"*** Imani haitatoweka mbinguni. Tutakuwa na Imani na kuona tukiwa mbinguni. Tomaso aliamini baada ya kuona. Sasa hivi tunaamini bila ya kuona. Mbinguni kutakuwa na kuona baada ya Imani yetu duniani na kuendelea na Imani. Mungu atusaidie!

**Joseph Ezenweze anaishi Nigeria, Afrika ya Magharibi.**

# Rubi za Robison

Mithali 16:3 inasema, ***"Mkabidhi Bwana kazi zako, Na mawazo yako yatathibitika."*** Wakati mwingine, nina staajabu kwa nini vitu haviendi katika njia ambayo naweza kuona kuwa ni bora, nahitaji kukumbuka vitu vichache. Hata kama jambo fulani linaonekana kuwa baya kwangu, Bwana anaweza kulifanya liwe na manufaa. Anaweza kutumia majaribu ili kuniimarisha. Anaweza kunifundisha kitu kupitia majaribu ili kwamba nije kuwa na uwezo wa kumsaidia mtu mwingine pindi atakapokuwa akipitia changamoto kama hiyo. Yakobo alisema, ***"Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali, mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi."*** (Yakobo 1:2-3). Paulo alisema, ***"Wala si hivyo tu, ila na mfurahi katika dhiki pia, mkijua ya kuwa dhiki, kazi yake ni kuleta saburi, na kazi ya saburi ni uthabiti wa moyo; na kazi ya uthabiti wa moyo ni tumaini;"*** (Warumi 5:3-4). Ingawa ni ngumu, kuna uwezekano nyakati ngumu hunisaidia kunifanya kuwa mtu bora zaidi.

# Maoni ya Haraka katika Aya Muhimu

## (Isaya 63:7-10)

**7** Nitautaja wema wa Bwana, sifa za Bwana kwa yote aliyotukirimia **Bwana**; na wingi wa wema wake kwa nyumba ya Israeli, aliowakirimia kwa rehema zake, na kwa wingi wa wema wake.
**8** Maana alisema, Hakika ndio watu wangu hawa, wana wasio na hila; akawa Mwokozi wao.
**9** Katika mateso yao yote yeye aliteswa, na **malaika wa uso wake** akawaokoa; kwa mapenzi yake, na huruma zake, aliwakomboa mwenyewe; akawainua, akawachukua siku zote za kale.
**10** Lakini wakaasi, wakamhuzunisha **Roho yake Mtakatifu**;..

Katika Isaya 48:16, neno "Mwanzo na Mwisho," "Mkombozi" kiunabii inazungumzia juu ya ujio Wake duniani, "na sasa Bwana MUNGU amenituma, na roho yake." Kifungu hiki kinaonesha Neno, aliweka kando mamlaka yake ili awe na umbo la mwanadamu (Wafilipi 2:5-7), chini ya uangalizi wa "Bwana Mungu" na "Roho Mtakatifu."

Katika Yohana 14:16 na 16:7 tunamwona Roho Mtakatifu akitumwa na Baba na Kristo, katika jukumu lake kama Msaidizi wa wazaliwa wa Mungu.

Kwa kuzingatia Maandiko ya Agano la Kale, tunatakiwa kuangalia mambo matatu ya Uungu ambayo yameoneshwa hapo yakifanya kazi pamoja katika ubinadamu. Katika kifungu hiki katika Isaya, tunasoma "Bwana" "malaika wa uso wake" na wa "Roho Mtakatifu."

Katika Kutoka 33:1-2 tunasoma juu ya "Bwana" akizungumza na Musa kuhusu safari ambayo wana wa Israeli waliyoitarajia kuianza, na akasema "nitamtuma malaika aende mbele yako;"

Katika Yoshua 5:13-15 maelezo yaliyotolewa "nili amiri wa jeshi la Bwana." Akimtokea Yoshua. Mazungumzo yalimalizika kwa Yoshua kumsujudia "Amiri" ambaye alidai kuwa uwepo wake ulisababisha mahali alipokuwa amesimama kuwa patakatifu.

Katika Agano la Kale lote tunamwona "malaika wa Bwana" akiwaongoza Waisraeli (Kutoka 13:21; 14:19) mchana kwa wingu la uvuli na usiku kwa nguzo ya moto. 1Wakorintho 10:4 inamtambua Kibinadamu kama mtu alyezaliwa kama Yesu Kristo.

Yohana 1:1 inatambulisha "Neno" aliyekuwako na Mungu hapo mwanzo, na alikuwa Mungu. Katika Agano la Kale lote tunasoma, "Neno la Bwana" lilimjia huyu na yule, "asema Bwana…" alikuwa mnenaji kwa niaba ya Uungu, Mpatanishi hata wakati huo.

# Mamajusi Walikuja Kumtafuta Yesu

**Sunny David**

Zaidi ya miaka elifu mbili imepita tangu kuzaliwa kwa Yesu katika Bethlehemu ya Yudea katika siku za mfalme Herode, Biblia inasema, ***" Yesu alipozaliwa katika Bethlehemu ya Uyahudi zamani za mfalme Herode, tazama, mamajusi wa mashariki walifika Yerusalemu, wakisema, Yuko wapi yeye aliyezaliwa mfalme wa Wayahudi? Kwa maana tuliiona nyota yake mashariki, nasi tumekuja kumsujudia"*** (Mathayo 2: 1-2). Kuzaliwa kwa Yesu katika Bethlehemu ilikuwa ni kutimia kwa unabii uliorekodiwa miaka zaidi ya mia moja iliyopita katika Agano la Kale la Biblia. Nabii Mika zaidi ya karne saba zilizopita kabla ya kuzaliwa Kristo alitabiri, ***"Bali wewe, Bethlehemu Efrata, uliye mdogo kuwa miongoni mwa elfu za Yuda; kutoka kwako wewe atanitokea mmoja atakayekuwa mtawala katika Israeli; ambaye matokeo yake yamekuwa tangu zamani za kale, tangu milele"*** (Mika 5:2). Isaya nabii mwingine wa Mungu alitangaza ***"Kwa hiyo Bwana mwenyewe atawapa ishara. Tazama, bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli"*** (isaya 7:14). Neno **Imanueli lina maana ya "Mungu Pamoja nasi**." Yesu alipozaliwa, Mungu aliingia katika daraja la ubinadamu, amekuwa mtu kupitia Mwanawe Yesu Kristo na amelipa adhabu ya dhambi zetu, zilizoangukia juu yake kupitia Mwanawe, kwa maovu yetu sisi (Yohana 1:1,14;3:16). Isaya alitabiri pia ya kwamba atakaye zaliwa atakuwa Mwana wa Mungu, atakuwa mfalme atakaye ongoza katika ufalme wake wa milele (Isaya 9:6-7). Isaya alitabiri kuhusu Yesu kuzaliwa na bikira, na Mika alitabiri kijiji atakachozaliwa Yesu, Bethlehemu.

Maandiko ya Agano la Kale, ambayo awali yaliandikwa kwa lugha ya Kiebrania, baadaye yalitafsiriwa kwa lugha ya Kigiriki mnamo miaka

ya 250 kabla ya Kristo. Mamajusi walikuja kutoka mashariki, (labda uarabuni, Mwanzo 25:6), kumwabudu Yesu. Walikuwa wasomi, wanafalsafa. Biblia ya Kigiriki inawaelezea kama Magia, aliyekuwa kuhani katika kipindi cha uongozi wa Kiajemi karne nyingi zilizopita kabla ya kuzaliwa kwa Kristo. Kwa sasa wameleta (dhahabu, ubani na tunu) zilizokuwa bithaa za Kiajemi. Mamajusi wakiwa katika nchi yao waliona nyota ya ajabu ambayo hawakuwahi kuiona mwanzoni. Waliichukulia kama ishara ya kuzaliwa kwa mtu wa ajabu katika ardhi ya Yuda, zaidi, ardhi ambayo nyota hii maalum ilionekana kutembea katika mtindo wa kimondo. Hii ilitofautiana sana na nyingine za kawaida hivyo walihitimisha kwamba hii inadhihirisha kitu fulani ambacho sicho cha kawaida na chenye umuhimu mkubwa. Wakajikita katika kujifunza Maandiko ya Agano la Kale, ambayo pia yalitabiri ***"…nyota itatokea katika Yakobo Na fimbo ya enzi itainuka katika Israeli;…"*** (Hesabu 24:17), walihitimisha kwamba mfalme wa Wayahudi, Imanueli, anayezungumziwa kwenye Maandiko amezaliwa. Kwa hivyo, walikwenda kukutana naye. Hatujui idadi yao. Kuna dhana kuwa walikuwa "watatu", dhana hii iliibuka kwenye aina tatu za zawadi zilitajwa, ambazo walitoa baada ya kumwona Yesu.

Hao watu hakika walikuwa wenye busara, kwa sababu haraka walipoiona nyota ya ajabu, hawakupoteza muda bali walitoka nje kumtafuta Mfalme mpya kwa kuifuata nyota. Lazima itakuwa imechukua muda mrefu kwa wao kusafiri wakiwa wamekaa juu ya Wanyama na wakienda kwa kupitia njia za misituni na barabara mbaya, na maeneo ya milima. Bado hawakukata tamaa. Walikuwa wenye busara, kwa sababu katika kumtafuta Yesu waliifuata nyota, ikiwaongoza, kwamba Mungu amewahakikishia wao. Ilikuwa ni mwanga uliowekwa na Mungu kuwaongoza kwa Kristo. Biblia inasema, ***"Nao waliposikia maneno ya mfalme, walishika njia; na tazama, ile nyota waliyoiona mashariki ikawatangulia, hata ikaenda ikasimama juu ya mahali alipokuwapo mtoto. Nao walipoiona ile nyota, walifurahi furaha kubwa mno"*** (Mathayo 2:9-10).

Hata leo hii njia ya busara ya kumtafuta Kristo na nini anachohitaji watu wajifunze kutoka kwake, na anachowafundisha wafanye, ni

kwenda moja kwa moja kwenye Agano lake Jipya katika Biblia na kusoma au kusikiliza isemavyo. Kuna mambo mengi ya uwongo yanayofundishwa katika jina la Kristo leo hii, ambayo hayapatikani katika Biblia na ambayo hayana lo lote la kufanya kwa Kristo na mafundisho yake. Kwa mfano unatakiwa kufanya nini ili uokoke? (Marko 16:16), ni kanisa lipi lazima uwe muumini wake? (Mathayo 16-18; Matendo 20:28;2:47) na jinsi gani utaabudu ili ukubalike? (Yohana 4:24; Mathayo 15:8-9). Katika Hotuba ya Mlimani, Yesu alifundisha:

***"Basi kila asikiaye hayo maneno yangu, na kuyafanya, atafananishwa na mtu mwenye akili, aliyejenga nyumba yake juu ya mwamba; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, isianguke; kwa maana misingi yake imewekwa juu ya mwamba. Na kila asikiaye hayo maneno yangu asiyafanye, atafananishwa na mtu mpumbavu, aliyejenga nyumba yake juu ya mchanga; mvua ikanyesha, mafuriko yakaja, pepo zikavuma, zikaipiga nyumba ile, ikaanguka; nalo anguko lake likawa kubwa."*** (Mathayo 7: 24-27)

Kuwa mwenye busara, haimpasi mtu kusikia tu au kujua kuhusu Kristo, lakini lazima afanye alichofundishwa. Mvua, mafuliko na upepo vinawakilisha usemi kuhusu ujio wa hukumu (Yohana 12:48). Mara nyingi watu wanapenda kwenda kwa watu na kwenye vitabu vilivyoandikwa na watu kwa ajili ya kujifunza kuhusu Kristo na mafundisho yake. Hata hivyo, wale wanaokwenda kwenye chanzo halisi, Biblia, Mungu ametupa mwongozo kwa ajili ya mambo yote ya kiroho. Hao wanaojifunza kuhusu Kristo na mafundisho yake hakika wana busara.

Kitu kingine kinachojulikana ambacho tunajifunza kwa wale Mamajusi ni kwamba, walipogundua kwamba, nyota waliyokuwa wakiifuata imesimama na haiendi kwingine bali imesimama mahali palipo na Mtoto mchanga, waliingia ndani ya nyumba ***"…wakamwona mtoto pamoja na mariamu mamaye, wakaanguka wakamsujudia"*** (Mathayo 2:11). Kumbuka, hawakumsujudia Mariamu. Mamajusi walijua Mariamu ni kama binadamu mwingine ambaye ametumiwa na

Mungu kumleta Mwanawe wa pekee ulimwenguni (Mathayo 1:18-25). Hakuna wasiwasi, Mariamu alikuwa mtu mwenye hofu ya Mungu na mtu aliyempenda Mungu, na hiyo ndiyo sababu Mungu alimtumia katika kazi hiyo kubwa na ya ajabu. Bado kwa hakika, hakuwa ***"mama wa Mungu"*** au kama mtakatifu asiye na dhambi kama Kristo alivyo. Mamajusi, hata hivyo, walimsujudia Yesu, Mwana wa Mungu, na wakamtolea zawadi. Mtume Paulo katika Waefeso 5: 15-17 alisema, "***Basi angalieni sana jinsi mnavyoenenda; si kama watu wasio na hekima bali kama watu wenye hekima; mkiukomboa wakati kwa maana zamani hizi ni za uovu. Kwa sababu hiyo msiwe wajinga, bali mfahamu ni nini yaliyo mapenzi ya Bwana".*** Mamajusi na wanawake wa leo hii wanamtafuta Yesu kama walivyofanya Mamajusi zaidi ya miaka elfu mbili iliyopita.

**Suuny David anaishi ndani ya New Delhi, India, na ni Mhubiri katika Hindi-speaking TV na ni mchungaji.**

## FUNDISHO LA MAMAJUSI

Shadrack S. Msambaza

**Waliifuata nyota kutoka mbali:** Ingawa walikuwa mbali na njia ilikuwa ngumu, lakini hawakujali hayo yote, waliendelea na safari. Ni wangapi wetu wana moyo kama huo, au tumekuwa watu wa visingizio na kukata tamaa?

**Walimsujudia Mtoto:** Katika macho ya kawaida walichokifanya ni kituko. Katika mazingira ya kifalme, hilo lilikuwa sahihi. Basi, kitendo hicho kilimaanisha kuwa Mtoto Yule alikuwa ni Mfalme wa ajabu. Dhihirisho la hilo walipuuza amri ya mfalme Herode na kutii agizo la malaika ili kumlinda Mtoto.

**Walikwenda na zawadi:** Katika safari yao walibeba zawadi nyingi na zenye thamani kubwa, jambo hilo lilihatarisha usalama wao pindi wakiwa njiani, lakini hayo yote hawakujali. Hii ilimaanisha kuwa Yesu alikuwa na thamani kuu kuliko wao. Je! Wewe na mimi huwa tunamwendea Yesu tukiwa mikono mitupu? Majibu unayo!

# Agizo Lake Ni Kazi Yetu

Darrell Surrette

Nimetumia zaidi ya miaka 22 ya maisha ya ujana wangu nikiwa jeshini. Katika miaka yote 22 nilijiandaa kuwa tayari kwa mapigano. Kila siku ililetwa kazi maalumu yenye “kipaumbele cha juu”. Hizo kazi maalumu hubadilika kutegemeana na hali halisi. Vivyo hivyo, ndani ya kanisa, tuna kazi kubwa. Tofauti moja kubwa kati ya kazi ya kidunia na kazi tuliyopewa na kanisa ni kwamba, kazi ya kanisa haibadiliki miaka na miaka, au hata karne na karne. Hii inapaswa kutimizwa kwa urahisi, ni sahihi?

Ndani ya Agano Jipya, Mathayo, Marko na Luka kila mtu amepewa jukumu kubwa (Mathayo 28: 18-20; Marko 16: 14-20; Luka 24:46-47)! Inaonekana yakipekee, hata jukumu la Mathayo ikisomeka ***“Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari***” (Mathayo 28: 18-20).

Kazi yetu inajulikana dunia nzima na katika kanisa kwamba imepata umaarufu kuwa ni “Agizo Kuu”. Kama ni kuu kiasi hicho kwetu huleta maswali, kwa nini hakuna ushahidi zaidi wa kazi hii hasa ndani ya sehemu ambamo tunakusanyika kuabudu? Tungeweza kutumia muda mwingi zaidi wa kujadili matokeo ya Agizo lenyewe, na tupo vizuri kwenye kuelezea mstari wa 19 nyuma ya mimbari. Hata hivyo, naweza kusema dunia inaonekana kuhitaji mstari wa 20 wote, msisitizo umejengwa kutoka katika mstari wa 18! Hususani, angalia hoja ya kwanza Yesu aliyoiweka. ***“Mamlaka yote nimepewa mimi.”*** Kinachosisitizwa kwa kina katika kauli hii ni kwamba Yesu kimsimgi

alisema **“sikilizeni ninachokwenda kusema, kwa sababu hicho ndicho kitakachowahusu.”** Hatupaswi kuthubutu kuchukulia kwa wepesi mwelekeo wa mwajiri wetu, kamanda au bosi vinginevyo tunaweza tusiwe na ajira tena. Kwa nini basi, inatendeka nje ya **“Agizo Kuu”** hatupati msisitizo zaidi kuliko ilivyo? Unaona, ujumbe leo hii unasikika kutoka katika mimbari, lakini kamwe haikumaanisha kuwa unaishia katika mimbari! Neno **“enendeni”** hasa linamaanisha kama kitenzi kilivyo.

Jambo moja nililojifunza katika kila kazi sikuwahi kuwa nalo ni kwamba **ama uimalize au ushindwe kufanya hivyo.** Kama ukishindwa, hasa matokeo yanakuwa mabaya sana, na hatia ni ngumu kuibeba. Lazima tujiulize wenyewe, “tupo katika nafasi ipi katika kuitii amri ya Kamanda wetu?” Hili si hukumu kwa mtu ye yote, bali ni wito wa kuamsha, ninasali, kwa ajili ya uvivu wetu. Tuna tabia ya kuvutiwa na viongozi ambao hawaogopi kufanya wao wenyewe kile wanachowaomba wasaidizi wao wafanye. Tuna tabia ya kuwa na heshima nyingi kwa wale ambao wamekuwepo pale tulipo, na ambao hawaogopi kuchafua mikono yao. Tuna tabia ya kutaka kuwafuata. Wapo wapi viongozi katika kanisa ambao wanaitii amri ya **“enendeni”?** Tuna Mkombozi na Kiongozi ambaye ametuonesha njia kwa kuiacha Mbingu na kuja ulimwenguni ili kuleta Injili. Agizo lake linapaswa kuwa kazi yetu! Tayari Yeye ni Mshindi, basi na tuchukue kazi yake, ileile ambayo ilikuokoa hata wewe! Waendee jamaa wa familia yako, majirani, marafiki, wafanya kazi wenzako kwenye mji ambapo kanisa la Kristo halipo au katika nchi ambayo Injili imefundishwa kidogo na kulihubiri Neno kwa ye yote aliye tayari kusikia ***kwamba Yesu ni Bwana!*** Kisha uwaambie jinsi tulivyokuwa wafanisi katika kufundisha nyuma ya mimbari kwa kila mmoja anayetuzunguka, ***“Mkiwabatiza katika jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu.”***

**Darrelll Surrete anahudumia katika ulinzi wa Taifa, na anaishi Ulaya, Misisipi , Marekani.**

# SERIKALI NA MKRISTO: MTAZAMO WA KANISA NA UTAMADUNI

Steve Higginbotham

Fikiria juu ya mtu ambaye hakuwa na makaazi, bali alikuwa akiishi mitaani. Hana uwezo kuwa wa kumiliki mahali pa kuishi, na hajawahi kuwa na kitu zaidi ya kile anachohitaji. Siku zote anapata vitu vya kumtosha kuishi tu. Basi siku moja kuna mtu akamhurumia kwa kumpatia nyumba ya kuishi pamoja na kupata huduma zote bure kabisa. Hatimaye yule mtu aliekuwa hana makaazi hapo mwanzo akajikuta anaishi maisha yenye faraja.

Lakini kadiri muda ulivyopita, yule mfadhili alibadili mawazo juu ya ukarimu wake. Mazingira yalimsababisha kufikiri upya matendo yote ya wema aliyokuwa amemuonyesha kwa yule mtu ambaye hakuwa na makazi mwanzoni. Dalili ya kwanza ya badiliko la mawazo yake ni kwamba aliondoa kiyoyozi kwenye nyumba. Miezi kadhaa baadaye, alikata maji. Hatimaye, alikata umeme. Ingawa huyu mtu ambaye mwanzo hakuwa na makazi hakupata tena baadhi ya huduma alizokuwa akizipata mara ya kwanza kwa mfadhili, lakini aliruhusiwa kuendelea kuishi ndani ya ile nyumba.

Sasa basi, swali langu ni kwamba, "Hali ya mtu huyu ambaye mwanzoni hakuwa na makazi itakuwa?" Je, anapaswa kunyoosha mikono kwa ajili ya kutaka huduma zilizoondolewa kwake?, au anapaswa kujawa na shukrani kwa ajili ya huduma alizozipata kipindi alichokuwa amepata kukifurahia?

Naamini kwamba wakati kuna kila namna ya kushituliwa ghafla kwa kuondolewa kwa baadhi ya huduma ambazo alikuwa amezizoea, bila shaka hakukosa kufikiri juu baraka alizokuwanazo kipindi cha nyuma, kwa maana hapakuwa na kitu hata kimoja alichokuwa na haki nacho. Hivi vitu vyote vilikuwa "zawadi" na anatakiwa kutoa shukurani kwa muda ambao alivitumia.

Kwa kusema hivyo, katika historia nzima, ukristo umepata upendeleo mara chache sana kwenye serikali. Ukristo ulipitia hali ngumu, mateso na kujitoa mhanga, lakini ulikuwepo. Sisi tumetokea tu kuzaliwa katika wakati na sehemu ambapo serikali yetu ilikuwa njema juu ya ukristo, hata kutoa nafasi ya upendeleo. Ila bado nyakati zinabadilika. Baraka zetu nyingi huondolewa kwetu. Marupurupu tuliyoyafurahia, sasa yameondolewa.Mtazamo wetu unatakiwa

kuwaje? Naamini jibu la swali hili ni sawa tu na lile lililotolewa kwenye swali la kwanza.

Ndugu zangu, ukristo hauhitaji upendeleo wa serikali ili uweze kudumu na kustawi katika baraka ambazo sisi na wazazi tumekuwa tukizifurahia, kesho zinaweza kondolewa kwetu. Hali hiyo inaweza kutuhuzunisha, lakini isiwe sababu ya kukata tamaa. Hakika, kiwango cha mateso tunayopata kinaweza kuwa ni kiwango tu cha dawa ambacho tabibu wetu mkuu amekiweka ili kiweze kuamsha ari zetu za kiroho inaweza kuwa ni "mateso ya kutosha" ni kile tu "tabibu mkuu" ameagiza kutuamsha kutoka kwenye uchovu wa kiroho na kuhuisha (kufanya upya) jitihada zetu na hali ya kujitoa kwa Mungu na ajenda yake. Dawa kama hiyo haivutii, ila inaweza ikawa nzuri kwetu, ebu ifikirie!

## ALAMA ZA MFUASI NI ZIPI?

Therman Hodge

Mfuasi ni mwanafunzi, anaejifunza na kufuatilia mambo. Kwa kawaida, mfuasi anatakiwa kuenda sawa na mawazo ya mtu anayemfuata, kwa maneno na maneno na vitendo kama mwalimu wake - Yesu (Luka 6:40). Yesu huishi ndani ya wafuasi wake ambao wanaendana naye (Wagalatia 2:40). Ni wajibu wa mfuasi kuwa kama Yesu. Kwa hiyo tunauliza, “Alama za mfuasi ni zip?"

Kwanza kabisa mfuasi wa kristo ni lazima awe ndani ya Neno (Yohana 8:31; 14:14,23). Kuna mambo matatu yanahusika katika kuwa ndani ya Neno: (1) Mtu ni lazima alipokee (Zaburi 1:2). (2) Mtu ni lazima alitafakari (Wagalatia 2:20). (3) Mtu ni lazima alitumie (Yakobo 1:22).

Pili wafuasi wa Kristo ni lazima wapendane (Yohana 13:34-35). Kwa nini hii ni amri mpya? (1) Ni amri mpya kwa sababu ni kitu kipya (Yohana 4:20). (2) Ni mpya katika kipimo (Mathayo 5:43-45). (3) Ni mpya katika kusudi (Yohana 13:35). Ni upendo huu ambao kila mtu anatakiwa kuwa nao kwa mwenzake ili kuwavuti wengine wapate kufanyika kuwa wafuasi wa Yesu pia.

Tatu, wafuasi wake Kristo ni lazima wazae matunda (Yohana 15:5-10; 1 Wakorintho 3:6-9). Kuna vitu vitatu vinafundishwa kwenye injili ya Yohana 15. (1) Mtu ni lazima awe ndani ya upendo wa Baba (Yohana 15:10). (2) Mtu ni lazima aziishi amri za Baba (Yohana 15:16). (3) Mfuasi ni lazima azae matunda (Yohana 15:16). Hizi tatu ni kama kiti cha miguu mitatu. Miguu yote husaidiana. Katika kuhitimisha, tunauliza, "Je unazo alama za mfuasi?" "Je Yesu anaishi ndani yako ili kuwafanya wengine kuwa wafuasi wake? "Je wewe kweli ni mfuasi wa Yesu?".

# Ukumbusho Wa Bwana

Gary C. Hampton

Ukumbusho, kama sanamu, mawe ya makaburini na mabamba hutumiwa duniani kote kwa heshima ya wanadamu, hasa wafu. Meza ya Bwana ni huduma ya ukumbusho. ***“Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa akisema, Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.’ Vivyo hivyo kikombe baada ya kula, akisema, ‘Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu”*** (Luka 22L:19-20). Kristo pia alisema, ***“Kwa maana kila mwulapo mkate huu na kukinywea kikombe hiki, mwaitangaza mauti ya Bwana hata ajapo”*** (1 Wakorintho 11:23-34, hasa 26). Kwa hiyo kila wakati Mkristo anaposhiriki Meza ya Bwana, anashiriki karamu ya ukumbusho.

Pasaka ilikuwa kivuli cha Meza ya Bwana. Sikukuu ya Pasaka ililiwa na Waisraeli mara moja kwa mwaka ili kuwakumbusha juu ya kukombolewa kwao kutoka katika utumwa wa Misri (Kutoka 11:1-8:1-8; 12:25-27, 46) Paulo alimshutumu Bwana kwa kusema, “*. . .kwa maana  Pasaka wetu amekwisha kutolewa kuwa dhabihu, yaani Kristo*” (1Wakorintho 5:7). Dhabihu ya Yesu ndiyo njia ya mkristo ya kuachiliwa kutoka katika utumwa wa dhambi (Waefeso 1:7). Kwa sababu Yeye ni Pasaka wetu, hakuna mfupa wake hata mmoja uliovunjwa (Yohana 19:31-36).

Sikukuu hii ya ukumbusho ina vitu viwili vinavyotumika, mkate na tunda (mzao) la mzabibu (Mathayo 26:26-28; Marko 14:23-25). Mkate unaotumka ni ule usiotiwa chachu, kwa vile agizo la Yesu lilikuja mara tu baada ya Yeye na wanafunzi wake kumaliza mlo wa pasaka ya kiyahudi (Kutoka 12:15). Mathayo anaiita sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu pale anaposema ***"siku ya kwanza ya mikate isiyotiwa chachu***" (Mathayo 26:17). Yesu alisema, ***“Huu ni mwili wangu.”*** Hilo limewafanya watu wengine kufundisha fundisho linalosema kwamba mkate na mzao wa mzabibu hubadilika kuwa mwili na damu halisi ya

Yesu. Kwa kuwa Yesu alikuwepo katika mwili wake wa kimwili sikukuu hii ilipokuwa ikianzishwa, inaonekana wazi kwamba alikuwa akitumia sitiari (lugha ya mfano). Sawa na aliposema, “Mtu akikupiga shavu la kuume,mgeuzie na pili” (Mathayo 5:39). Hapo hakuwa na maana kuwa ukipigwa na mtu umsogelee tena akupige mara ya pili kihalisia. Ila alimaanisha kwamba mtu akikutendea mabaya, wewe umtendee mema. Vivyo hivyo, Yesu hakumaanisha tule mwili wake na tunywe damu yake halisi, bali ni kwamba mkate na mzao wa mzabibu huwakilisha mwili wake na damu yake.

Meza ya Bwana inapaswa kuliwa siku ya kwanza ya kila juma. Luka aliandika, ***“Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane”*** (Matendo 20:7). Paulo alikuwa Troa siku saba (Mst 6), lakini wanafunzi walikusanyika kwa ajili ya Siku ya Bwana kwa kuwa Yesu alifufuka siku hiyo (Marko 16: 9; Matendo 2; Walawi 23: 15-16). Sasa, Mungu aliposema, “Ikumbuke siku ya Sabato uitakase” (Kutoka 20:8) Wayahudi walielewa kwamba alimaanisha kila Sabato. Kisha Paulo akasema, ***“Siku ya kwanza ya juma kila mtu kwenu na aweke akiba kwake, kwa kadiri ya kufanikiwa kwake, ili kwamba michango isifanyike hapo nitakapokuja”*** (1Wakorintho 16:2), tumeelewa kuwa ni kila siku ya kwanza ya juma. Katika kazi zetu za kimwili, bosi akisema siku ya malipo ni siku ya kwanza ya juma, tunaelewa kuwa ni kila siku ya kwanza ya kila juma. Kwa nini hatuelewi kwamba kanisa lilikusanyika kila siku ya kwanza ya juma kumega mkate? Sote tunapaswa kuishiriki kama ukumbusho wa kila juma wa dhabihu kuu ya Bwana wetu kwa ajili ya dhambi.

***“Akatwaa mkate, akashukuru, akaumega, akawapa akisema, Huu ndio mwili wangu unaotolewa kwa ajili yenu; fanyeni hivi kwa ukumbusho wangu.’ Vivyo hivyo kikombe baada ya kula, akisema, ‘Kikombe hiki ni agano jipya katika damu yangu, inayomwagika kwa ajili yenu”*** (Luka 22L:19-20).

# KUMWABUDU MUNGU KATIKA NYIMBO!

Mark N. Posey

Kibali cha kuimba katika Agano Jipya kimo katika Maandiko yafuatayo Mathayo 26:30; Matendo 16:25; Warumi 16:19; 1Wakorintho 14:15; Waefeso 5:19; Wakolosai 3:16; Waebrania 2:12; 13:15; Yakobo 5:13, Ufunuo 5:8-9; 14:1-3; 15:2-3. Kila kifungu katika maandiko haya kinaonyesha kuwa uimbaji katika Agano Jipya unahusisha sauti za midomo tu kama sehemu ya ibada ya Kanisa la Agano Jipya.

Vifungu vilivyotajwa hapo juu ni mamlaka yenye nguvu juu ya kutumia muziki wa sauti za midomo katika ibada ya kanisa la Kristo. Angalia uainishaji wa vifungu hivi.

- **Amri ya moja kwa moja:** Waebrania 13:15; Yakobo 5:3, Waefeso 5:19: Wakolosai 3:16
- **Mfano wa Mitume:** Mathayo 26:30, Matendo 16:25; I Wakorintho 14:15.

Mungu ametueleza wazi wazi jinsi anavyotaka kusifiwa. Kwa matunda ya midomo yetu tunamwimbia sifa na kuliinua Jina Lake Kuu na Takatifu. Mungu anastahili kupata sifa kutoka kwetu. Zingatia kwamba Mungu alikuwa wazi kuhusiana na jinsi ya kumwabudu kwa nyimbo. Aliagiza uimbaji wa sauti za midomo kwa wale wanaoishi chini ya Sheria ya Kristo. Kamwe tusiende mbali na shauku aliyokuwanayo, ni wajibu wetu kufuata maagizo yake!

Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, **mkifundishana** na **kuonyana** kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu. Wakolosai 3:16

# UTUHUISHE TENA: KUNA UHITAJI WA UAMSHO KATIKA KANISA LA LEO

Claude Thompson

Mama yake William P. Mackay alijaribu kumsisitiza mwanawe juu ya thamani ya Biblia, na alipoondoka nyumbani alimpa Biblia ndogo. Hata hivyo, William aliasi mafundisho ya mama yake, hata akauza Biblia. Kwa maelezo yake mwenyewe, kadiri umri wake ulivyoongezeka, alizidi kuwa "mwovu zaidi". Baadaye, Mackay akawa daktari kule Scotland, naye alikuwa akimtibu kibarua mmoja aliyekuwa amejeruhiwa vibaya sana ambaye ombi lake pekee lilikuwa kwamba mama mwenye nyumba wake ampelekee "Kitabu,"basi akapelekewa. Mara baada ya kukipata, alikisoma ama kukishika kitabu hicho kidogo kila mara katika siku zake za mwisho. Baada ya kifo cha mtu huyo, Mackay alikuwa na jukumu la kutoa vitu vyake. Kwa mshangao, Mackay akagundua kuwa kitabu cha yule mtu ilikuwa Biblia yake mwenyewe ikiwa na jina lake lililoandikwa kwa mwandiko wa mama yake. Ujumbe uleule ambao Mackay alikuwa ameukataa hapo awali kuwa haufai, hatimaye ulimletea hatia na hatimaye wokovu.

Alipohuishwa kiroho, Mackay aliandika maneno ya shairi, ambayo yaliwekwa katika muziki na John Husband kama wimbo mkuu ukisema, "Tuhuishe tena." Mwaka wa 2013 ulikuwa ukumbusho wa miaka 150 tangu kuchapishwa kwake, na hatua hiyo muhimu inatuhimiza kutazama kwa umakini jumbe za kiroho kwa kazi iliyo bora.

"Utuhuishe tena… kila nafsi iamshwe upya." Maneno yote mawili: Kiebrania 'khaw –yaw' na Kiyunani 'anazao' yanayotafsiriwa 'huisha' au 'uamsho' humaanisha 'kuishi tena'. Ingawaje yanatumiwa kuonyesha ufufuo halisi wa wafu kwa maisha ya kimwili (1Wafalme 17:22, 2 Wafalme 13:21; Warumi 14:9), mara nyingi hutumiwa kwa njia ya

sitiari kama :kustawi au kuwa hai tena'" ( Waamuzi 16:19: Nehemia 4:2) dhambi inaweza kuhuishwa ndani ya mwanadamu (Warumi 7:9), na imani pia lazima ihuishwe (Warumi 12:2; Wagalatia 6:1).

Imani ya mwanadamu lazima iendelee "kuhuishwa" na "kuamshwa upya" Tena na "tena"!Kwa kweli, uamsho ni muhimu zaidi kuliko utii wa kwanza." Kuhusu wale wanaotenda dhambi wangali wanajua, Petro anaonya kwamba "Ingekuwa heri kwao kama wasingeijua njia ya uadilifu kuliko kuijua na kugeuka kutoka katika utakatifu. ( 2 Petro 2:20-21) Uamsho wa kiroho ni chaguo la hiari la mwanadamu, lakini pia ni kazi ya Mungu, unahitaji "moto kutoka juu."

"Tunakusifu", Ee Mungu. Wimbo huu kwa hakika ni maombi ya sifa kwa Mungu kwa ajili ya kazi yake katika uamsho wa kiroho. Mstari wa ufunguzi wa beti zake nne tano huanza na tamko hili la sifa na baadhi ya nyimbo huitumia kama kichwa. Nafsi zote tatu za Uungu zimetajwa kuwa zinastahili sifa kwa sehemu yao katika uongofu wa kiroho na uamsho.

"**Mungu**" Baba ndiye chanzo cha baraka zote za kiroho (Waefeso 1: 3 .) Mwanadamu, mara nyingi sana, anaomba tu kwa ajili ya mahitaji yake ya kimwili, lakini maombi ya Mackay anamwoomba Mungu atulete karibu naye.

"**Mwana. Yesu, ambaye alikufa**." Yesu alitenda kazi katika uumbaji wa mwanadamu (Yohana 1:1-3), na pia ni "Mwana-Kondoo aliyechinjwa," kwa ajili ya kumkomboa mwanadamu arudi kutoka katika dhambi kwa damu yake mwenyewe (Tito 2:14). Sasa "amekwenda juu. " Kuwangoja wafuasi wake waaminifu waende kuungana naye (Ufunuo 5:5-6).

"**Roho wa nuru…ametuonyesha Mwokozi wetu**," ambaye hutuongoza kwenye imani ya awali na kutufundisha kwa njia nyingine kupitia Maandiko (2 Petro 1:20-21).

"**Ujaze kila moyo kwa upendo wako**." Upendo ni msukumo wa Mungu kwa kazi zake zote za neema. Yesu, "mwana wa upendo wako". Ni onyesho kuu la upendo huo (Yohana 3:16) Upendo kwa Mungu na kwa wanadamu wenzetu pia lazima kiwe kichocheo pekee cha kuitikia

upendo na amri zake (Mathayo 22:37-40). Upendo ndio neema kuu zaidi ya kudumu ( 1Wakorintho 13:13 ).

"Uamsho" si neno tunalolisikia sana leo. Labda hiyo ni kwa sababu tumesahau upendo wetu wa kwanza na sasa tunafuata dini yetu zaidi kwa mazoea au kwa mapokeo. Kuna haja kubwa ya kuwepo uamsho wa kweli wa imani na utendaji wa kiroho katika maisha ya wakristo leo. Maombi yetu na yawe kama yale ya William Mackay na mtunga Zaburi, “Tuhuishe tena” (85:6). “Haleluya”! Amina”

## Uzima Na Utauwa


Maisha ya mwanadamu, ya kiroho na ya kimwili yako mikononi mwa Mungu. Mtume Petro alisema*, “Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa…* (2 Petro 1:3). Hivyo, hakuna jambo jema lolote tunaloweza kulifanya pasipo msaada wake.

Katika uumbaji, Mungu alitangulia kutuandalia mazingira yanayostahili maisha yetu, ikiwa ni pamoja na majira na nyakati ili tuweze kuendesha maisha yetu kwayo, huku tukizingatia kanuni alizotuwekea. Kwa hiyo, maisha yetu ya kimwili yamepangwa na Mungu (Mathayo 5:44-45).

Kwa habari ya maisha ya kiroho, ambayo kwayo tuna tumaini la uzima wa milele, pia tumeelezwa namna uzima huo utakavyopatikana, kwani Roho wa Mungu ametufinulia yote (1 Wakorintho 2:10-11; 2 Timotheo 3:16, 17). Kwa hiyo, habari yote inayohusu maisha ya kiroho, hasa tukiwaza juu ya uzima wa milele, tutapata katika maandiko yaliyoandikwa kwa mwongozo wa Roho Mtakatifu. Paulo alisema tufikiri juu ya maisha ya milele (Wakolosai 3:1-4). Naye mtume Petro akihimiza juu ya kujifunza maandiko matakatifu, alisema, *“Kama watoto wachanga waliozaliwa sasa yatamanini maziwa ya akili yasiyoghoshiwa, ili kwa hayo mpate kuukulia wakovu*” (1 Petro 2:2).

Pamoja na kwamba Mungu ametukirimia vitu vyote juu ya maisha ya kimwili na ya kiroho, lakini Yesu anatusihi tuyape kipaumbele zaidi maisha ya kiroho, ya kimwili yafuate nyuma (Mathayo 6:31-34).

**Peter O. A. Kamatula**



# Je, Unapima Vipi?

Umtumaini Bwana ukatende mema, Ukae katika nchi,
upendezwe na uaminifu. Nawe utajifurahisha kwa Bwana,
Naye atakupa haja za moyo wako. mkabidhi Bwana njia
yako, Pia umtumaini, naye atafanya.
6 Ataitokeza haki yako kama nuru, Na hukumu
yako kama adhuhuri.
7 Ukae kimya mbele za Bwana, Nawe
umngojee kwa saburi; Usimkasirikie yeye
afanikiwaye katika njia yake, Wala mtu
afanyaye hila.
8 Ukomeshe hasira, uache ghadhabu,
Usikasirike, mwisho wake ni
kutenda mabaya.
9 Maana watenda mabaya
wataharibiwa, Bali wamngojao
Bwana ndio watakaoirithi nchi.
10 Maana bado kitambo
kidogo asiye haki
hatakuwapo, Utapaangalia
mahali pake wala
hatakuwapo.
11 Bali wenye upole
watairithi nchi,
Watajifurahisha kwa
wingi wa amani.

Zaburi 37:3-11

# MITHALI 17:22



Kijana mdogo alikuwa anamngoja mama yake atoke dukani. Alipokuwa akingoja, aliJiwa na mtu mmoja ambaye alimuuliza, “Mwanangu, unaweza kuniambia mahali posta ilipo?

Yule kijana mdogo akajibu, "Ndiyo, nenda tu moja kwa moja kwenye mtaa huu, utapita majengo kadhaa halafu ugeuke kulia kwako.”

Yule mtu alimshukuru kijana kwa upole na kusema, “Mimi ndiye mhubiri mpya mjini, ningependa uje kanisani Jumapili. Nitakuonyesha jinsi ya kufika Mbinguni.

Kijana akajibu huku akicheka, “Aaa! Wewe, wakati huijui hata njia ya kwenda posta?”

Wagombea wawili wa kisiasa walikuwa na mjadala mkali. Hatimaye, mmoja wao aliruka na kumwambia mwenzie, “vipi kuhusu shauku kuu inayokutawala?”
Na jamaa mwingine akajibu, “mwache mke wangu katika hili!”

Siku moja miaka kadhaa iliyopita nilikuwa nasoma gazeti mwanangu alipoingia na kusema, “Baba, utanipeleka kwenye mbuga ya wanyama kesho,” nikamwambia, “Hapana. Kama wanakutaka wanaweza kuja kukuchukua.”

Mke wa Mike alinunua aina mpya ya vipodozi vya bei ghali alivyohakikishiwa kuwa vitamfanya aonekane kijana kwa miaka mingi. Baada ya kukaa kwa muda mrefu mbele

ya kioo akitumia bidhaa za “miujiza,” aliuliza, “Mpenzi, kusema kweli, ungesema nina umri gani?”
Akimtazama kwa makini, Mike alijibu, “Kwa kuangalia ngozi yako, miaka 20; nywele zako, miaka 18; na umbo lako, miaka 25.”

Akalalamika, “Aa! we mpenzi,wewe! Mike akamkatisha, “Ebu subiri kidogo, sijajumlisha bado.”

Mwanafunzi mchanga wa darasa la Biblia aliombwa kuorodhesha Amri Kumi kwa mpangilio wowote. Alijibu: 3,6,18,4,5,9,2,10,7.

Kwenye uwanja wa ndege sehemu ya kukagulia wasafiri,nilimsikia mwanamke mmoja akiomba nafasi mbili za dirishani kwa ajili ya mumewe na yeye mwenyewe. Karani akamweleza kwamba hii ingewafanya washindwe kuketi pamoja.Yule mwanamke akajibu, "Sikiliza, mpenzi, "nimekaa siku 10 tu za wakati mzuri katika gari la kukodi na mwanaume huyu. Najua ninachokiomba!”

**Kama Mama tu**

Hakupenda bakuli, Na hakupenda keki yangu Biskuti zangu zilikuwa ngumu sana…. Sio kama mama yake alivyokuwa akitengeneza. Sikuinywa kahawa sawa, Hakupenda mchuzi.

Sikushona soksi zake kwa namna mama yake alivyokuwa akifanya. Nilikuwa natafakari jibu. Nilikuwa natafuta ishara. Kisha nikageuka na kumpiga, Kama mama yake alivyokuwa akifanya.

Little Johnny alifngua zawadi yake ya sikukuu ya kuzaliwa kwake kutoka kwa Gramma.
Muhtasari kutoka kwa Gramma, ilikuwa ni bastola ya maji! Alipiga kelele kwa furaha na
kuelelekea kwenye sinki la maji la karibu zaidi.

Mama yake hakufurahishwa sana. Akamgeukia Gramm na kusema, “Umenishangaza kumletea bastola ya maji. Je, hukumbuki jinsi tulivyokuwa tukikutia wazimu na hizo?” Gramma alitabasamu tu, "Ndiyo, nakumbuka."

Katika darasa la Biblia la Jumapili walikuwa wakijifunza jinsi Mungu alivyoumba kila kitu, wakiwemo wanadamu. Johnny alikuwa makini kusikiliza hasa pale mwalimu alipomweleza jinsi Hawa alivyoumbwa kutoka kwenye ubavu mmoja wa Adamu. Baadaye katika juma hilo hilo, mama yake akamwona akiwa amelala chini kana kwamba ni mgonjwa. Mama yake akamuuliza, “Johnny, una tatizo gani”? “Johnny alijibu, “Nasikia maumivu upande wangu mmoja. Nadhani nakaribia kupata mke.

Alama kubwa nyekundu ya “F” ilikuwa kwenye karatasi yake ya mtihani. Freddy akamtazama rafiki yake aliyekasirika na kumuuliza, "Kwa nini ulipata alama ya chini kwenye mtihani huo?"

Little Johnny akajibu, “ Kwa sababu ya kutokuwepo”. Akamuuliza, “Ina maana siku ya mtihani hukuwepo?”Little Johnny alijibu, "Hapana, ila mtoto anayeketi karibu nami hakuwepo."

**Mithali 17:22**

**Moyo uliochangamka ni dawa nzuri; Bali roho iliyopondeka huikausha mifupa.**

# UTAJIRI NA UMAARUFU WA DUNIANI HAUWEZI KUNIINGIA KAMWE

DON MYERS

Katika uandishi wake Mathayo wa hotuba ya mlimani, Yesu alikuwa na mambo mengi ya kusema kuhusu mahangaiko na mali za kidunia. Moja ya hatari kuu katika safari yetu ya kiroho ni jinsi tunavyoshughulika na pesa na mali. Kutokana na hotuba ya Yesu, mambo yanayopaswa kuzingatiwa ni: kuepuka kuwasaidia wengine ili kupata sifa kwa wanadamu (6:3), kusali kwa ajili ya mkate wetu wa kila siku (6:11), kujizoeza kufunga (6:18), kutojiwekea hazina duniani. (6:19), kumtumikia Mungu - si mali (6:24), kuacha kusumbukia maisha (6:25), tahadhari kuhusu kuzungukwa na watu wa dunia ambao wamejishughulisha na kutengeneza na kuwa na mali (6: 32) na kuishi maisha ya siku moja kwa wakati - kesho itajisumbukia yenyewe (6:34).

## Mawazo machache tu juu ya Maneno ya Yesu

**Kwanza**, kama vile viashirio katika magari yetu (kipimo cha mafuta, kipimo cha joto, onyo la mkanda wa kiti, n.k) kuna baadhi ya mambo (ikiwa tutaangalia dashibodi za mioyo yetu) ambayo hutuwezesha kuangalia kwa haraka mahali tulipo kiroho.... Je, tumewahi kujitathimini na kujiona kwamba mtu mwingine amejua kuwakulimtendea mtu jambo jema kwa kutumia nyenzo na mali ambavyo kiukweli ni vya Mungu - mali zote tulizopewa na Mungu? Tunaweza kuwa na njia za ujanja sana (lakini, bila kujua) za kuwasaidia watu ili tu tuonekane machoni pa wengine. Yesu alisema kwamba hatupaswi kamwe kutoa ili tupate sifa kwa watu kwa sababu hayo ndiyo yatakuwa malipo yetu pekee. Hatupaswi kamwe kutoa kwa watu ili kujionyesha kwa wengine. Kwa nini tunafanya hivyo? Tunapotoa ili tupate sifa kutoka kwa wengine, hatutoi kwa haki, bali tunanunua sifa kwa wanadamu.

**Pili**, je, leo ninaweza kujishughulisha na kile nitakachokula, kunywa au kuvaa kesho kiasi cha kusahau kuomba na kushukuru kweli kweli kwa ajili ya riziki ya kila siku? Mimi, mke wangu, na mjukuu wangu tunapokaa kula, huwa naizungumzia sahani yangu iliyojaa, “Haya ndiyo maisha yetu.”Naweza tu nikala sana siku moja tu- na si zaidi. Umewahi kununua gari (jipya au la zamani) na ukajikuta unatafuta au unazungumzia gari lingine ulilotaka kununua? Ama mkate wa kila siku? Au mahitaji ya kila siku? Kula kilichoko mbele yako bila kufikiria utakachokula kesho. Unakumbuka Waisraeli walikusanya mana zaidi ya walivyohitaji kwa siku? Mana iliyobokia iliharibika! Vaa mavazi uliyonayo pasipo kufikiria mavazi utakayokuwanayo baadaye kwenye kabati lako la nguo.

**Tatu**, Yesu hakusema “kama mkifunga”, bali alisema, “mnapofunga”. Yesu alidhani wanafunzi wake wangefunga. Kwa kweli, hatuwezi kuchunguza funga ya kila mmoja wetu au kutaarifu kwa wengine, “Ninafunga,” kwa sababu tunazingatia maonyo ya Yesu kwamba tusifunge ili tuonekane na watu. Wakati wa kufunga, tunajitenga kwa muda na mahitaji ya kidunia ili tujiweke wakfu kwa maombi ili tupate kukumbushwa jinsi tunavyotegemea upaji wa Mungu. Mtu mmoja alisema, “*Mungu yupo karibu na na kila mtu kupitia tumbo lake*.” Mungu huwanyeshea mvua wenye haki na wasio haki. Wenye haki wanapaswa kuinua macho yao Mbinguni na kusema kutoka moyoni, Asante, Bwana Mungu.

**Nne**, je, umewahi kuridhika kabisa, halafu muda mfupi tu baadaye ukaona tangazo kwenye runinga likiuliza kama uko tayari kustaafu na kisha, mara moja ukawa kutoridhika? Mabilioni ya dola hutumika kwa matangazo yaliyotengenezwa na wataalamu waliosoma vyuoni ambao wana ujuzi wa kuleta hali ya kutoridhika. Wako vizuri sana katika hilo! Je, inawezekana kwamba tunanunua vitu ambavyo hatuwezi kuvimudu ili kupatana na watu ambao hata hatuwapendi?

**Tano**, Je, una wasiwasi juu ya kukosa chakula au mavazi? Yesu alisema tuache kuwa na hofu juu ya mahitaji ya maisha. Je, tumekosa chakul? Mungu wetu aliyetuwezesha jana ni Mungu yule yule atupaye

chakula cha kila siku. Haja yetu kama wakristo ni kujisalimisha katika utawala wa Bwana wetu Yesu na Mungu Baba.

**Sita**, ni vigumu kuweka mambo ya kidunia na ya kimwili katika mtazamo sahihi tunapozama katika bahari ya uchoyo wa kitaifa na kimataifa.Tena, wale watu wanaotaka kupata zaidi na zaidi huwa na mashaka? Ndiyo wapo! Mambo hayawezi kutosheleza. Tuna mashujaa wasio sahihi. Je, haingekuwa vema kuwa huru mbali na minyororo ya kidunia inayotufunga? Vipi kama tungeridhika na chakula rahisi cha leo, mavazi na vinywaji?

**Mwisho**, je, tunataka kuiishi kesho kwa maana ya kwamba tunashindwa kukabiliana na changamoto za leo? Je, changamoto za leo hazitoshi bila kuiweka kesho mabegani mwetu? Umesikia habari ya mtu anayetembea barabarani mchana wa nyuzi joto 100, akitokwa na jasho, huku akiwa amebeba gunia la kilo hamsini mgongoni kwake? Mtu mmoja alikuja karibu naye akiwa katika gari la kukokotwa na farasi na kumuuliza, “Je, ninaweza kukubeba?” Kwa msaada huu, yule mbeba mzigo akashukuru kwa kujibu, “Ndiyo, eeh! Asante!” Yule mtu aliyelemewa na mzigo alipanda nyuma ya lile gari na yule mtoa msaada akamwamuru farasi wake aende. Kisha akamsikia mtu aliyekuwa nyuma ya lile gari akiguna. Alipogeuka, akamwona yule mtu aliyemchukua amesimama nyuma ya lile gari na gunia lake la kilo hamsini likiwa bado mgongoni kwake. Yule mtu akauliza, “Kwa nini hutui huo mzigo?” Akajibu, “Sikujua kuwa msaada ulionipa wa kunibeba unalihusu gunia langu pia.” Hivi, bado tunahangaika na mizigo ambayo Yesu alitualika muda mrefu tumpelekee atubebee? Petro alisema, “Mtwikeni fadhaa zenu zote kwa maana yeye hujishughulisha sana kwa mambo yenu.

Yesu anajua nini kuhusu maisha? Mungu aliuumba ulimwengu, kwa hiyo anaujua unavyokwenda! Mungu, katika mwili wa Yesu, alifanyika kuwa mmoja wetu! Mungu katika mwili wa binadamu hakuwahi kusafiri umbali wa maili mia moja kutoka mahali alipozaliwa. Alikuwa na aina moja tu ya mali za kidunia-nguo zake. Baada ya Kuanza huduma Yake ya kidunia, je, unakumbuka umewahi kusoma mahali

popote kwamba alikuwa na nyumba ambayo alikuwa anailipia kila mwezi? Haja yake ilikuwa nini, na alizama hasa kwenye nini? Hapa kuna siri ya kuishi duniani - amani na kuridhika! Ni wapi tena ambapo tumewahi kufikiria kupata amani ya nafsi isipokuwa kupitia na kuwa ndani ya Yesu?

Maneno haya ya Yesu si ya kukariri tu, bali ya kuyaishi. Tumwombe Mungu tujifunze kuyaishi kiuhalisia.

**Don Myers profesa msaidizi wa Biblia katika Chuo Kikuu chaFaulkner na ni mhubiri wa kanisa la Elmore, Alabama, Marekani.**

# Tafakuli Ya 2 Timotheo 3:16, 17

***"Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."*** Maneno haya "*andiko lenye pumzi ya Mungu*" yana maana "Kila andiko lililoandikwa kwa uwezo wa Roho Mtakatifu." Katika fungu hili la maandiko, Paulo ameanisha mambo manne ambayo yanayopaswa kuzingatiwa na mtu ye yote mwenye shauku ya kwenda mbinguni. Mambo hayo ni:

1. **Mafundisho**- hapo maana yake ni kwa maandiko yanafaa kutuonyesha mema yote ambayo Mungu anataka tuyajue kwa ajili ya uzima wetu wa milele.
2. **Maonyo-** maandiko yanafaa kutuonyesha mabaya yote ya ulimwengu huu ili tupate kuyaepuka.
3. **Kuongoza-** maandino yanafaa kutuonyesha njia namna ya kuyaacha mabaya ya ulimwengu na kuingia kwenye mambo mema ya kiroho [Ndiyo maana kuna hatua tano za wokovu].
4. **Kuadibisha-** maandiko yanafaa kutufunya tuishi kwa adabu baada ya kuyakimbia mabaya na kuingia kwenye mambo mema ya kiroho.
   - Maandiko matakatifu yanatukamilisha.

**Peter O. A. Kamatula**

# BIBLIA INAFUNDISHA NINI KUHUSU KUFUNGA? JE, KUFUNGA NI KWA AJILI YA WAKRISTO?

ERICK OBENG ASANT

Kufunga, kwa muujibu wa Biblia ni hali ya kuacha kula na kunywa kwa sababu za kiroho. Katika historia ya Agano La Kale, Wayahudi walifunga mara kwa mara, ingawaje kulikuwa na aina moja tu ya funga iliyoamriwa katika Torati! Mara moja kila mwaka siku ya upatanisho, waebrania walipaswa kuzitesa roho zao (Law. 16:31), kwa maana ya kufunga (Linganisha na Isaya 58:3).

Pamoja na kwamba hakuna shuruti ya kufunga kwa wakristo leo, Agano Jipya linaonyesha kuwa wana wa Mungu wanapaswa kuona umuhimu wa kufunga katika matukio fulani fulani. Wanafunzi wa Yesu walipolaumiwa kwa kutokufunga kwao, Yesu alijibu kuwa hapakuwa na haja kwao kufunga alipokuwa angali pamoja nao.

Hata hivyo, wakati ungefika baada ya Yesu kuchukuliwa kutoka kwao ambapo wangefunga (Luka 5:35).

Pia, katika kuonya dhidi ya hamasa zisizofaa ibadani, Kristo alisema, "*Tena mfungapo msiwe kama wanafiki*." Hapo inafaa tutambue kwamba Yesu hakusema "**kama mnafunga**" bali alisema "**mfungapo**" akiwa na mategemeo kwamba watafanya hivyo.

Kufunga, kwa upande wa wakristo, ni jambo la hiari. Linatakiwa litokane na hisia na kusudi la ndani ya moyo wa mtu, isiwe kama matokeo ya utaratibu wa kawaida.

## KUFUNGA KUNA THAMANI GANI

Ni wakati gani basi kufunga kunakuwa na thamani? Kufunga kunaweza kuwa na manufaa ya kiroho wakati wa huzuni binafsi. Daudi na watu wake waliomboleza na kufunga baada ya kusikia habari ya kifo

cha Sauli (2 sam. 12:16). Pia Nehemia alifanya vivyo hivyo alipopewa taarifa ya hali ya maangamizi ya Yerusalemu (Nehemia 1:4).

Kufunga na kuomba inaonekana kunafaa sana pale mpendwa anapokuwa mgonjwa sana (2 Samweli 12:16). Mara nyingi kunaenda sambamba na toba kama mwonekano halisi wa utu wa nje kuonyesha majuto kwa ajili ya mambo ya uasi wa kiroho. (1 Samweli 7:6). Watu wa Ninawi walitangaza kufunga walipotambua dhambi zao (Yona 3:5).

Kufunga kuliambatana na matukio makuu na muhimu ya kidini. Musa alifunga kipindi cha muda aliokuwa anapokea Torati (Kutoka 34:28). Kristo alifunga kipindi alichokuwa anaelekea kukabiliana na shetani kule jangwani (mt. 4:2).

Kanisa lilifunga kabla ya kuwatuma Barnaba na Sauli kwenye safari ya kwanza ngumu sana ya kimisionari (Matendo 13:2-3). Kwa kweli kufunga lilikuwa jambo muhimu sana katika huduma ya Paulo iliyokuwa ngumu kwake pamoja na hali ya kusafiri (2 Wakorintho 6:5, 11:27).

## MAONYO KWA WALE WANAOFUNGA

Lakini, kwa kukiri wazi; funga inaweza kufanyika visivyo. Zoezi la kufunga lisiwe badala ya maisha binafsi ya utauwa.

Isaya aliwakemea kwa ukali waliokuwa wanafunga na huku wakiendekeza tamaa zao za kidunia (Isa. 58).

Zaidi ya hayo, kufunga lisiwe tukio la mtu kujionyesha kuwa yeye ameishika sana dini. Mafarisayo walikuwa na hatia juu ya jambo hilo (Mathayo 6:16-18).

Mwisho, msimamo wa kufunga usipewe nafasi ya kuanzisha hali ya kujisikia au kuridhisha nafsi ama kujipa haki kiroho katika mambo ya dini. Hali hiyo inawezekana kuwa jaribu (Luka.18:9-14).

## FAIDA ZA KUFUNGA.

Katika mchanganuo wa mwisho, kinachoonekana ni kwamba kufunga ni kwa hiari. Kwa nyakati fulani kufunga kuna faida kama ifuatavyo:

- Maandiko yanaonyesha kuwa Mungu anathamini funga ya mtu inapofanyika kuonyesha ishara ya kujiweka wakfu katika dhamiri safi.
- Wataalam wa afya wanaeleza kuwa kufunga katika hali ya wastani kuna faida ya kuifanya mifumo ya mwili ipate nafasi ya kujisafisha.
- Akili inapata nafasi ya kutafakari na kupambanua mambo kwa kina wakati wa kufunga.
- Kufunga kunaweza kumfanya mtu ajiweke katika hali ya nidhamu zaidi.
- Kufunga kunaweza kuchochea hali Yetu kuimarisha ari ya shukurani kwa yale mambo ambayo hatujiwezi kwayo vipindi ambavyo hatuna uhuru wa kuchagua.

## Marejeleo Ya Maandiko

Walawi 16:31; Isaya 58:3; Luka 5:35; Mathayo 6:16; 2 Samweli 1:12; Nehemia 1:4; 2 Samweli 12:16; 1 Samweli 7:6; Yona 3:5; Kutoka 34:28; Mathayo 4:2; Matendo 13:2-3; 2 Wakorintho 6:5; 11:27; Isaya 58; Mathayo 6:16-18; Luka 18:9-14.

# Kiasi

Ed Benesh

***"Lakini ikiwa Roho wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake aliyekaa ndani yenu"*** (Warumi 8:11).

Mwaka 1920, mabadiliko ya katiba ya 18 yaliazimia kukataza unywaji wa pombe. Kwa hiyo hii ikaonekana ni "marufuku." Lakini, miaka 13 baadaye mabadiliko ya katiba ya 21 yakaitangua ile ya kumi na nane, ikitufunulia uhalali wa kirai (maneno) "huwezi kuutungia sheria uadilifu." Wakati kwa sehemu tu ni kweli, hata hivyo ni kweli. Kwa nini? Ni kwamba, katazo lilithibitika kuwa shida si pombe, sawa tu na bunduki, ngono na kamali namna visivyokuwa na shida. Kama msemo wa zamani usemavyo, "Bunduki haziui watu, watu wanaua watu."

Tatizo ni sisi kutokuwa na kiasi, kitu ambacho pia ni vigumu kukitungia sheria. Hatuhitaji udhibiti wa bunduki au sheria kali zaidi juu ya uwepo wa ngono na kamali. Tunahitaji kuwa na kiasi zaidi.

# BWANA ANAWAITA WAPIGANAJI WOTE KUFANYA VITA NA SHETANI, NJOENI NYOTE TUVAE SILAHA NA TWENDE VITANI

(Waefeso 6:11)

Mpango mkuu wa shetani
Dave Hart

Ni jambo la kutisha!!!!! Fikiria juu ya hilo. Shetani aliitisha kikao cha mazungumzo cha dunia nzima. Katika hotuba yake ya wazi kwa malaika zake waovu alisema, "Hatuwezi kuwazuia wakristo kwenda kanisani. Hatuwezi kuwazuia kusoma Biblia na kuujua ukweli, hatuwezi hata kuwazuia kujenga ushirika wa karibu na uhusiano mwema ndani ya kristo. Pindi wanapopata hayo mahusiano na Yesu, nguvu yetu inavunjika juu yao. Kwa hiyo, waacheni waende kwenye makanisa yao; waacheni waishi maisha ya kihafidhina (ya ufuasi makini), lakini ibeni muda wao, ili washindwe kupata ule uhusiano wao na Yesu Kristo. Hivi ndivyo ninavyotaka mfanye nyie malaika: watingeni ili wasipate nafasi ya kushikamana na mwokozi wao wasije wakadumisha uhusiano wao siku nzima. Malaika wakajibu, “tunawezaje kuyafanya hayo”?

"Tutawezaje kufanya hivi?" Walijibu kwa sauti malaika zake.

"Wafanyeni watingwe na mambo yasiyo muhimu maishani na kuwatengenezea mipango isiyohesabika ili kuchukua akili zao." Wajaribuni kwa kuwafanya wawe watu wa kutumia sana na kukopa kopa.”

"Washawishini wake zao waende kazini kwa masaa mengi na waume kufanya kazi siku 6-7 kila wiki, masaa 10-12 kwa siku, ili waweze kumudu mitindo yao ya maisha isiyokuwa na maana. Wazuieni kuwa na muda wa kukaa na watoto wao kutokana na kutokupata nafasi kwa sababu ya kazi na shughuli nyingi! Tieni msisimko katika akili zao ili wasiweze kuisikiliza ile sauti ndogo ya kuwaokoa.

Washawishini wasikilize redio au kanda za muziki wakati wowote wanapoendesha vyombo vya moto ili kuwepo mwendelezo wa kushulika na vitu kama: TV, VCR, CD na kompyuta majumbani mwao kama ilivyo kwenye maduka, mahoteli n.k ambako nyimbo za kweli za Mungu hazina nafasi.

Meza za sebuleni zijazwe majarida na magazeti. Zijaze akili zao habari saa 24 kwa siku. Teka muda wao wa kuendesha magari kwa kuweka mabango ya matangazo. Jaza masanduku yao ya barua kwa "Malundo ya barua, maagizo ununuzi wa bidhaa kwa njia ya posta, "bahati nasibu", na kila aina za majarida ya kuwatumainisha kuwapa bidhaa bure, ambazo ni huduma na matumaini ya uongo.

Weka wanamitindo wembamba na wazuri kwenye majarida ili waume zao waamini kwamba uzuri wa nje ndo kilicho muhimu na kuwafanya wote wasiridhike na wake zao. Hali hiyo itazifarakanisha familia zao haraka! Hata wasione umuhimu wa kurejeana.

Msiwaache waviendee viumbe vya asili kutafakari maajabu ya Mungu. Badala yake watumeni kwenye hifadhi za vichekesho, matukio ya michezo, matamasha na sinema.

Wafanyeni wawe na shughuli nyingi! Halafu wanapokutana katika ushirika wa kiroho, wahusishe kwenye mambo ya umbeya na kusemana ili waondoke na dhamira tata na hisia zisizotulia. Endeleeni, waacheni washughulike na kuokoa roho, lakini jazeni maisha yao kwa kutoa sababu nzuri sana za kushughulika na maisha ya kimwili hata wasiwe na muda kutafuta nguvu kutoka kwa Yesu. Punde, watakuwa wanafanya kazi kwa nguvu zao wenyewe wakitoa kafara afya na familia zao kwa ajili ya maisha yao. Hiyo itafaa.

Yalikuwa ni mazungumzo tu. Malaika waovu wakaenda kwa shauku kwenye kazi zao, ili kusababisha Wakristo kila mahali wawe na shughuli nyingi zaidi za kwenda huku na kule. Nadhani swali ni: Je, shetani kafanikiwa katika mpango wake? Wewe uwe mwamuzi!

**Dave Hart anafanya kazi na kanisa la Kristo kule Winslow, Arizona, nchini Marekani.**

# WAUME, TAFADHALI SOMENI!

Samuel Matthews

"***Enyi waume, wapendeni wake zenu, kama Kristo naye alivyolipenda Kanisa, akajitoa kwa ajili yake*** " (Waefeso 5:25). Wapendwa, kwa wanaume waliooa, hakuna changamoto kubwa zaidi ya ile iliyotolewa kwa nabii alieongozwa katika kuandika maandindishi haya. Kuwapenda wake zetu ni rahisi, lakini kuwapenda "kama kristo naye alivyolipenda kanisa" hicho ni kiwango cha juu mno. Ndoa zetu haziwezi kuwa namna zilivyotakiwa kuwa kama hatujafuata kielelezo cha upendo wa Yesu kwa Kanisa lake. Hivyo basi, katika makala hii, tutaona tu jinsi Kristo alivyolipenda kanisa. Halafu, kwa smaada wa Bwana, sisi waume inatakiwa tuwatendee wake zetu jinsi ipasavyo.

Kristo alilipenda kanisa kidhabihu. Maandiko yanasema, "*alijitoa kwaajili yake*". Alilipenda kanisa, si kwa vile ambavyo kanisa lilivyomtendea, bali Yeye alivyolitendea kanisa. Yesu alisema, "lakini mimi kati yenu ni kama atumikaye" (Luka 22:27). Pia alisema "*kama vile mwana wa Adamu asivyokuja kutumikiwa bali kutumika, na kutoa nafsi yake iwe fidia ya wengi*" (mathayo 20:28). Mtu Kufanikiwa kumpenda mke wake kama kristo alivyolipenda kanisa kunahitaji hali ya kujitoa sana kwake. Si kwamba tunatakiwa tufe kwa ajili ya wake zetu, lah! Bali tunatakiwa tuwe tayari kuwahudumia katika kukidhi mahitaji yao. Kwa hakika, upendo wa kweli "hautafuti mambo yake" (1 Wakorintho 13:5)

Kama waume, tunatakiwa tuelewe kwamba wake zetu wana mahitaji yanayotofautiana na ya kwetu, na ni wajibu wetu kuyatimiza hayo mahitaji yao. Pamoja na kwamba mahitaji ya wake zetu yanatofautiana, utafiti uliofanyika kwa miongoni mwa washiriki wa madarasa ya Biblia ya wanawake, walipoulizwa mambo ambayo wangependa watendewe zaidi na waume zao, majibu yalikuwa kama ifuatavyo:

**1.** Hitaji la kwanza lililoelezwa ni kwamba waume zao watekeleze uongozi wa kiroho. Kwa kweli 91% ya wanawake waliofanyiwa utafiti waliorodhesha hili kama hitaji linalotakiwa kutiliwa mkazo zaidi. Ewe mume, mke wako anataka ushike hatamu ya uongozikatika kuiandaa familia yako kwa ajili ya maisha ya milele, ikiwa ni pamoja na kutumia mamlaka katika utekelezaji mwenendo ya haki, adabu na ushiriki wa ibada na mafundisho ya Biblia.

**2**. Hitaji lililofuatia kwa umuhimu kama lilivyotajwa nawashiriki wa madarasa lilikuwa kujituma katika familia. Kama mume, mkeo anakuhitaji uweke nguvu zako kumsaidia anapojishughulisha katika kuiimarisha nyumba dhidi ya mambo yoyote yanayoweza kuweka vitisho kwenye familia.

**3.** Pia jambo linguine muhimu katika orodha yao ya mahitaji ni mazungumzo na mawasiliano. Mke anaumia mume anapokuwa hazungumzi naye kama rafiki yake. Ingawa inaweza kuwa mume hakuwa na nia ya kumchukulia mke wake kama si wa muhimu, lakini mara nyingi kwa mtazamo wa mke ataona kama mume hamjali. Kumbuka mkeo ni mwenzi wako, anstahili kushiriki kwenye mawazo na mipango yako.

**4.** Hitaji lengine lililotajwa ni kuonyesha mapenzi ya dhati kwa wake zetu. Ingawa hili ni hitaji muhimu sana kwa waume pia, lakini kwa kawaida jinsi wake wanavyotarajia upendo uonyeshwe kwao ni tofauti. Kama waume, tunahitaji kutumia ufahamu wetu kubuni njia mpya za kuonyesha mapenzi ya kweli kwa wake zetu.

**5.** Pia kwenye orodha yao ulitajwa usalama wa kifedha. Hili lisitafsiriwe kama hitaji kwa ajili ya matajiri, la! Badala yake litafsiriwe kama hitaji la mume kuwajibika katika kuisaidia familia. Kuna mambo mawili ya kuyaepuka. Mume ambaye anaacha jukumu lake la kuihudumia familia atakuwa ameshindwa kuitunza kwa kutoyakabili mahitaji halisi. Kwa upande mwingine, wapo waume wanaotumia kigezo cha kutimiza majukumu ya kawaida katika familia zao kama sababu ya kutokutoa hela za matumizi, huko nako ni kushindwa kuitunza familia.

Kristo alilipenda kanisa upendo wa namna ya pekee. Ingawa Yesu aliupenda ulimwengu mzima kama Baba yake alivyoupenda (Yohana 3:16), alilitakasa kanisa kama bibi arusi wake (waefeso 5:26-27). Hii ina maana alilitenga kanisa lake mbali na mambo ya ulimwengu. Vivyo hivyo, mahusiano ya ndoa yanadai utakaso. Mume ametengwa kuwa wa mke wake, na mke ametengwa kuwa wa mume wake- mume ni wa mke, mke ni wa mume. Muingiliano wowote ule katika mpangilio huu uliotolewa na Mungu ni dhambi.

Hekima inadai kwamba, kwa kadiri iwezavyo, mume ajiepushe na hali inayomwonyesha kuwa anategemewa kufanya kazi kwa karibu na mwanamke zaidi ya mke wake. Kama kazi ya mtu inalazimu kuwa na mwanamke ambaye si mke wake, basi anatakiwa ahakikishe kuna watu wengine kwenye eneo la kazi hiyo ili kuepuka tuhuma zisizosahihi zinazoweza kujitokeza na kumtia fikra mbaya mke wake.

Hitaji la kuridhishana katika ndoa ni la wanandoa wote wawili (1Wakorintho 7:2-5), kwa pamoja "**wana*ikimbia zinaa***" (1 Wakorintho 6:18) "***na mambo kama hayo***" (Wagalatia 5:19-21). Hali hii peke yake inakataza kutazama picha za ngono.

Kristo alilipenda kanisa kwa kulijali sana. Andiko linasema, "*vivyo hivyo imewapasa waume nao kuwapenda wake zao kama miili yao wenyewe. Ampendaye mkewe hujipenda mwenyewe*" (waefeso 5:28). Mtu anapomtendea jambo jema mke wake, anajitendea mwenyewe. Mtume Paulo alisema, "*Maana hakuma mtu anaeuchukia mwili wake popote; bali huulisha na kuutunza, kama kristo naye alivyolitendea kanisa*" (aya 29). Kuutunza mwili ni kuulisha. Kristo anamlisha bibi arusi wake kwa "chakula cha uzima (Yohana 6:48-51).

Tunalinda na kujali kwa upendo vitu au mtu tunayemthamini. Mume mwenye upendo kwa mke wake atamtunza na kumjali. Mume mwenye hekima atamtunza mke wake kwa kuweka wazi kwake na kwa watu wengine kwamba anamthamini.

Kristo alilipenda kanisa kwa uvumilivu unaodumu. Yesu amelifanya kanisa lake "*viungo vya mwili wake, na vya mifupa yake*" (Waefeso 5:30).

Hali kadhalika, "*…mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja*" (Waefeso 5:31). Yesu alinukuu andiko kutoka katika kitabu cha Mwanzo 2:24 kufundisha hali ya kutotengana katika ndoa(Math 19:5-6). Mungu anawaunganisha mwanaume na mwanamke (katika mpango wa ndoa na kuwa "mwili mmoja". Mwili mmoja. Mwanadamu hatakiwi kutenganisha kilichounganishwa na Mungu (Mathayo 19:6). Wakristo Katika Agano jipya, wazo la talaka linatakiwa kuwa mbali sawa na mtu kufikiria kuutenganisha mwili wake mwenyewe.

Jinsi Yesu alivyolipenda kanisa inatosha kabisa kumfanya mtu kutoa shukrani nyingi kwa mke wake. Mume anatakiwa amwone mke kama zawadi yenye thamani kubwa (iliyofungwa vizuri) kutoka kwa Muumba wake ambaye alijua hitaji lake.

Mtu mwenye hekima aliandika, "*Ajipatiaye mke apata kitu chema, naye apata kibali kwa Bwana*" (Mithali 18:22).

**Samuel Matthews anafanya kazi na kanisa la Kristo la Mtakatifu Thomas kwenye visiwa vya Virgin, Marekani.**

## Upendo na Heshima Kwa Mke

Kwa habaria ya maisha ya mke na mume, mtume Paulo aliandika juu ya waume kuwapenda wake zao mithili ya upendo wa Kristo kwa Kanisa (Waefeso 5:25). Upendo huo ni ule usiokuwa na masharti, mume anatakiwa kumpenda mke pasipo kuangalia mema au mapungufu anayotendewa na huyo mke. Huo ni upendo wa *agape*.

Mtume Petro amezungumzia swala la mume kumpa heshima mke. Katika waraka wake wa kwanza anasema, "*Kadhalika ninyi waume, kaeni na wake zenu kwa akili; na kumpa mke heshima, kama chombo kisicho na nguvu, na kama warithi wa neema ya uzima, kusudi kuomba kwenu kusizuiliwe*." (1 Petro 3:7).

Mtume Paulo, pia alisema, "*Vivyo hivyo na wazee wa kike wawe na mwenendo wa utakatifu, . . . ili wawatie wanawake vijana akili, wawatie, wawapende waume zao na kuwapenda watoto wao*. . . kufanya kazi nyumbani mwao. . . (Tito 2:3-5).

**Peter O. A. Kamatula**



# WAKE!

**Betty Burton Choate**

Uchafuzi wa ajabu alioufanya shetani kwenye utamaduni wetu! Tumemruhusu kufunga fikra za watu (hata nimesoma kwamba zile za kimaadili kwa sasa zimepitwa na wakati; hatuzihitaji katika ulimwengu wa kisasa, kwa sababu utaratibu wao wa awali ulikuwa kupambana na- chanzo cha vita vyote), juu ya wanawake, juu ya familia, juu ya talaka, juu ya ushoga, juu ya kujiua, juu ya kutoa mimba, juu ya ndoa, juu ya uzinzi- juu ya uumbaji na Mungu na dini. Fikira za watu wengi kuhusu masomo yote haya ni kinyume na jinsi ilivyokuwa na ni kinyume na Maandiko yanavyofundisha.

Je, dunia imekuwa sehemu nzuri zaidi kwa sababu ya jaribio letu katika uasi? Ni Dhahiri, hapana. Uhalifu, kujiua, talaka, magonjwa ya akili na kila aina ya ukatili vimejitokeza kwenye miaka hamsini iliyopita. Utafiti uliofanyika huko nyuma kuhusu hofu kuu zaidi kwenye moyo wa mtoto uliorodhesha hofu ya giza, ya dhoruba na kufanya vibaya shuleni. Ni hofu gani, watoto wa leo wanakumbana nazo? Unyanyasaji, talaka na ugaidi. Ulimwengu umekuwa tofauti mno!

Nadharia ya "*Ubinadamu*" ndio mzizi mkuu wa migogoro hii, dunia ikiwa iko kwenye mteremko mkali unaoteleza wa kujiharibu yenyewe. Moja ya zana zenye ufanisi ambazo nadharia ya“*ubinadamu*”

Imezitumia kutufikisha kwenye hatua hii tuliopo ni kumvamia Hawa wa kisasa. Ndiyo, amekuwa akimsikiliza tena yule nyoka wa zamani, na ameuamini uwongo wake. Tena, Adamu alikuwa naye, lakini hajatimiza jukumu lake la kumlinda mke wake na nyumba yake kutoka kwenye kifo ambacho hakika kinakuja kutokana na kula tunda lililokatazwa.

## UTAJE UONGO

- Kuwa mwanamke anayefanya kazi ni vizuri**.**

Miaka sitini iliyopita, shetani alianza kuwashawishi waume na wake kwamba, mke anatakiwa na analazimika wakati mwingine kufanya kazi nje mbali nyumbani. Kibali kikatolewa, maana kuna hali ambazo kiuhalisia hakuna chaguo: anatakiwa kufanya hivyo ili ajipatie kipato, vinginevyo familia yake itakosa chakula. Ingawaje mara nyingi mke anafanya kazi za ziada kwa sababu ya kutamani kufanya zaidi mambo ya kiduniani,ili angalau sehemu ya malipo hayo ya ziada yasaidie kwenye gharama zamahusiano ya mume/mke, mama/mtoto,maisha ya nyumbani na maisha ya kiroho ya familia.

Inachukua muda kukuza mahusiano yoyote, na hicho ndicho kinachotokea pale mke anapofanya kazi muda wote nje na mazingira ya nyumbani. La kusikitisha, sehemu ya kazi, pia inakuwa eneo la mahusiano ya kirafiki inayoweza kusababisha talaka na maumivu ya moyo yasiyokwisha.

- **Uhuru wa mwanamke ni mzuri.**

Kwa kweli,udhalilishaji uliofanikiwa zaidi ni ule uliokuja kwa njia ya uongo wa "*usawa*". Wanawake si binadamu wa kiwango cha chini katika kuumbwa, lakini wengi wamejitengenezea wenyewe kiwango cha chini kwa kufuata hii sehemu ya utamaduni wa binadamu. Wanawake sasa wapo katika "*usawa*" wanaweza hata kuajiriwa kufanya kazi ngumu na nzito ambazo waliachiwa wanaume. Katika “*usawa*” wao na kwa kupenda kwao kukubali mambo ya uzinzi kama njia ya kuendeshea maisha, Mara nyingi wamekuwa wakijikuta kwenye changamoto za maisha za utoaji mimba au ukosefu wa fedha, majukumu ya kihisia na kiroho na namna ya kulea watoto peke yao.

- **Kuvaa “kiwanamitindo” ni vizuri.**

Katika upumbavu wao, wanawake wengi wamejifanya bidhaa kwa kuonyesha miili yao matangazo ya kuwaridhisha watu wengi kwenye maisha yao ya kila siku, wakitembea duniani wakiwa nusu uchi, halafu wanapiga kelele pindi wanaume wanapojibu ujumbe wao wakisema, “*nipo hapa kwa ajili ya kuchukuliwa*.”

- **Kuwa na watoto wa mtu kwenye kituo cha kulelea watoto ni vizuri.**

Akina mama wameacha malezi ya watoto wao---miliki zao zenye thamani zaidi---kwa wageni. Ni sawa, kunapokuwa hakuna namna nyingine ya kufanya, hitaji hili ni la kuumiza moyo---lakini kuna akina mama ambao hawawezi kusubiri Jumatatu ili warudi ofisini na kwenda kuwachukua wale watoto wao.

- **"Kuishi ndani ya nyumba" pamoja na rafiki yako wa kiume (mchumba) ni vizuri.**

Lakini pindi mwanaume mvivu, ambaye hakutarajiwa kufanya majukumu yoyote, wakati wowote anakuwa tayari kuondoka.Huyu Hawa wa kisasa atakuwa ameingia gharama kiasi gani?

- **"Talaka ni bora kukiko kuishi na mwanaume ambaye simpendi tena"**

Ni kawaida leo kwa wanaume na wanawake kuingia katika ndoa na mtazamo kwamba, "*Ndoa hii ikileta shida, tutapeana talaka tu*." Kwa msingi huo, ni ndoa ngapi zitastahimili changamoto na dhoruba? Kwa kawaida ni nani anayekuwa na maisha magumu zaidi baada ya talaka? Mungu anakataza talaka (Marko 10:4-9).

# Tiba ni ipi?

Kwa kweli ni rahisi. Kwanza kabisa, inatakiwa kutathiminiwa upya kwa mombo haya yote ambayo yamekuwa yakipotoshwa na utamaduni wetu wa “*ubinadamu*”. Njia itakayomwezesha mwanamke kufanya tathimini upya ni kuzama kwenye Neno la Mungu, akitafuta funguo zote zilizotolewa pale. Mungu aliwaumba wanawake; aliumba ndoa; aliumba nyumba (familia). Ni jambo la kimantiki kuhitimisha

kwamba maelekezo katika kitabu chake yatatujenga ili tuweze kuishi kwa usalama na kwa furaha katika dunia hii.

- **Kitu "cha kwanza" cha muhimu ni kujitoa jumla kwa Mungu.**

Mungu yupo kwa ajili ya wanawake watauwa, ndoa imara na nyumba zenye furaha. Mke akijitoa kwa ajili ya kumcha Mungu atapata uhakika kwamba hawezi kukiuka kanuni au kuyaacha malengo.

- **Hitaji la pili ni kujitoa kwa ajili ya mume wake.**

Mpango ya Mungu, kulingana na Mwanzo 2:23-24 na Waefeso 5:22-31, ni mwanamke kumtii mume wake mtauwa, ambaye anamjali na kumlinda.

- **Anatakiwa awe tayari kujitoa kwa ajili ya familia yake.**

Mke mwaminifu atatanguliza mahitaji na furaha ya mumewe na ya familia yake kabla ya mambo yake, na matokeo yatakuwa maisha yenye furaha ambayo ni faida kwake.

- **Anatakiwa alipe nafasi Neno la Mungu liongoze tabia yake, hali yakena na uvaaji wake.**

Mke mwangalifu, mwenye fikra nzuri, mwenye huruma na upendo kwa mume ambaye anaendelea kumuombea atakuwa tajiri.

**Betty Burton Choate ni mjane wa J.C. Choate, mwanzilishi wa Sauti Ya Kweli Ya Kimataifa, anaeishi Winona, Mississippi, Marekani.**

## Mke Mwema

***“Mke mwema ni nani awezae kumwona? Maana kima chake chapita kima cha marijani. Moyo wa mume wake humwamini wakla hatakosa kumpa mapato. Humtendea mume wake si mabaya, siku zote za maisha yake. Hutafuta sufu na kitani; Hufanya kazi yake ya mikono kwa moyo. Anafanana na merikebu za biashara; Huleta chakula chake kutoka mbali. Tna huamka kabla haujaisha usiku; Huwapa watu wa nyumbani mwake chakula; Na wajakazi wake sehemu zao. Huangalia shamba akalinunua; Kwa mapato ya mikono yake hupanda mizabibu. Hujifunga nguvu viunoni kama mshpi; Hutia mikono nguvu”***

(Mithali 31:10-17).

# JE, TUNALEA WANAMICHEZO AU WAKRISTO?

Wes McAdams

Kama unanijua mimi na familia yangu vizuri, bila shaka utakuwa unajua kuwa mwanangu mwenye umri wa miaka 9 anapenda mchezo wa **baseball**. Huwa anaangalia karibu kila mechi ya michezo ya TEXAS RANGERS kwenye runinga (au anajilaza kitandani akisikiliza redio), anaweka ligi yake ndogo, anaweza akakaa na kuuzungumzia mchezo wa baseball kwa masaa, na ni mara chache kumwona hana aina yo yote ya vimpira vidogo mkononi mwake (hata ndani ya nyumba). Hivyo, naamini kabisa kwamba familia za kikristo zinahitaji kuweka tahadhari kwa watoto wao wanapokuwa na vipaji vya mapenzi ya michezo.

## Ibada Sanamu Ya Michezo

Naamini kitu chochote kinaweza kufanyika kuwa sanamu ya kuabudiwa, na pia ninafikiri maana nzuri ya ibada ya sanamu ni "**Kuwa na hisia juu ya kitu kama vile mtu anavyokuwa na hisia juu ya Mungu**." Ibada ya sanamu ni hali ya kuamini katika moyo wa ndani ambayo mtu hawezi kukamilika asipokuwa katika hali hiyo katika maisha yake. Kwa maneno mengine, jambo hili linayafanya maisha ya mtu yawe na thamani. Kwa hiyo, si ajabubu kuona watu wakiabudu michezo.

- Je, viwanja vikubwa sana vya michezo tunavyojenga vinatofautiana sana na mahekalu ya kale?
- Je, aina ya wataalam wa michezo si kama makuhani wanaotuombea dua?
- Je, watu hawaangalii, hawasikilizi na kusoma kuhusu michezo katika mfumo wa kidini?

- ❖ Je, timu yetu pendwa inayocheza haionyeshi kutawala kila jambo katika maisha yetu?
- ❖ Si kila hali ya hisia zetu inategemea namna timu inavyofanya katika michezo?
- ❖ Je, watu wengi hawaamini kwamba michezo inafanya tuishi maisha tunayostahili?

Sitaki mwanangu aiabudu baseball. Sitaki afikiri kwamba baseball inafanya maisha yawe na thamani. Sitaki aamini kwamba hawezi kukamilika bila baseball. Nataka ajue kwamba baseball inaweza kupotea kwa usiku mmoja na kila kitu kikabaki sawa tu.

Usinielewe vibaya. Nataka acheze baseball na aifurahie kwa namna anavyotaka, lakini hatimaye nataka akumbuke kwamba huo ni mchezo-sio mungu.

## Kipaumbele Cha Yesu



Nilipokuwa mtoto mdogo, mama yangu alikuwa ananiambia, "*Unaweza ukawa na kipaumbele kimoja tu*." Kunaweza kuwa na jambo moja tu ambalo ni la muhimu zaidi katika maisha ya mtu. Kunaweza kuwa na jambo moja tu linalochukua nafasi ya kwanza kuliko jumbo linguine lolote. Kama baba, nimeamua kwamba baseball haitakuwa kipaumbele cha familia yetu.

Katika Mathayo 10:37-39, Yesu aliyasema haya kwa habari ya

kuwa mfuasi wake, "***Apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili. Wala mtu asiyechukua msalaba wake akanifuata, hanistahili. Mwenye kuiona nafsi yake ataipoteza; naye mwenye kuipoteza nafsi yake kwa ajili yangu ataiona."***

Kama Yesu angezungumza nasi leo, je, asingesema, "*Ye yote anayependa baseball au soka kuliko mimi hanistahili"*? Yesu na ufalme wake kinapaswa kuwa kipaumbele chetu, kitu kingine chochote kionekane ni takataka tunapojaribu kufananisha.

## Mstari wa Mwisho

Kila familia ya kikristo inapaswa kuamua namna itakavyofanya kuhakikisha michezo kamwe haitakuwa miungu sanamu katika nyumba yao. Wote ni lazima tuhakikishe kwamba ndani ya mioyo yetu, na ndani ya mioyo ya watoto wetu, mambo yasiyostahili hayaeti kwenye kiti cha enzi anapotakiwa kuketi Kristo. Hatutakiwi kuiruhusu michezo itawale maisha yetu, itupangie ratiba zetu na ituamrie hali ya hisia zetu. Tutaifunga baadhi ya michezo na kutangaza, "*Michezo si jambo la mwisho (la muhimu Zaidi) katika nyumba yetu*."

Kwa makusudi kabisa tutatumia muda, fedha na nguvu kwa ajili ya mambo ya Yesu Kristo kuliko tunavyotumia kwenye michezo. Kwa weledi mkubwa watoto wajue jambo lililo la muhimu zaidi nyumbani mwao. Watangaze kwa njia ya maneno au pasipo maneno juu ya jambo linalotakiwa kuchua nafasi ya kwanza katika maisha. Wanaweza kuona kama michezo na mazoezi ya michezo ni muhimu zaidi kwetu kuliko ibada, madarasa ya Biblia, uinjilisti na huduma kwa wengine. Si hotuba tu tunazohubiri kwa midomo yetu, bali hotuba tunazohubiri kwa njia ya pochi zetu na kalenda zinazowashawishi watoto wetu.

Kwa kadiri wanangu wanavyokua, napaswa kuendelea kujiuliza swali, "Je, nalea wanamichezo au Wkristo?"

**Wes McAdams ni mtumishi anayehubiri katika kanisa la Kristo McDermott Road kule Plano, Texas, Marekani.**

# Tubu Au Angamia

Dennis Gulledge

Wahubiri wa Injili wameyatumia maneno haya mara nyingi pasipo idadi katika hotuba zao kama mamlaka kwa ajili ya kuwasihi watu wajue ulazima wa toba. Hakuna swali kwamba kugeuka na kuacha dhambi (kutubu) ni lazima katika kuongoka (Matendo 17:30-31). Tena, hakuna shaka kwamba tunapaswa kuwasihi watu juu ya ujumbe wa Neno la Mungu kwa yale yote tunayoamini na kutenda (1 Thessalonians 5:21). Leo uhubiri wa uthibitisho wa maandiko unakosolewa sana, tunahitaji daima kutumia mamlaka ya Agano Jipya la Mungu katika yote tunayotenda na kufundisha (2 Timothy 4:2).

Angalia Luka 13:1-5 katika mtazamo wa namna ilivyokuwa kimazingira. ***"Na wakati uo huo walikuwapo watu waliompasha habari ya Wagalilaya wale ambao Pilato alichanganya damu yao na dhabihu zao. Akawajibu akawaambia, Je! Mwadhani ya kwamba Wagalilaya hao walikuwa wenye dhambi kuliko Wagalilaya wote, hata wakapatwa na mambo hayo? Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo. Au wale kumi na wanane, walioangukiwa na mnara huko Siloamu, ukawaua, mwadhani ya kwamba wao walikuwa wakosaji kuliko watu wote waliokaa Yerusalemu? Nawaambia, Sivyo; lakini msipotubu, ninyi nyote mtaangamia vivyo hivyo."*** (Luka 13:1-5).

Fungu hili na mengine yote, yanatakiwa kunukuliwa, kutajwa au kutumika kwa kuzingatia muktadha (mazingira) wao. Je, Yesu alikuwa anatupa hoja kwamba iingizwe kwenye mpango wa wokovu wa Injili? Kama ni hivyo, basi hivi ndivyo ninavyohitaji kulitumia fungu hili. Kama sivyo, na ninalitumia kwa namna hiyo, je, sitakuwa na hatia ya kulitumia andiko tofauti na muktadha wake, hata kama hoja inayojengwa ni nzuri?

Muktadha wa fungu hili unamwelezea Yesu akiwafundisha makutano (Luka 12:1-13:9). Tumejulishwa katika sehemu hii ya maandiko fundisho la Yesu juu ya unafiki (Luka 12:1-12), kupenda mali au tamaa (aya 13-34), kuwa makini (aya 35-48), maafa yaliyotarajiwa (aya 49-59) na toba (Luka 13:1-9). Katika aya ya 1, Luka alitaja tukio ambalo halikunukuliwa katika maandiko. Machafuko na uasi yalikuwa mambo ya kawaida miongoni mwa Wayahudi. Ukatili wa Pilato unatolewa kama mfano hapa. Jambo la lililokuwa akilini kwa wale walioleta taarifa ya tukio hili ni kwamba iliaminika kuwa lilikuwa tendo la adhabu ya Mungu kwa wale waliokuwa waovu zaidi yao.

Kitabu cha Ayubu kiliweka msingi wa mambo hayo kwenye vitabu vilivyofuata. Yesu aliwafundisha mapema wanafunzi wake juu ya mawazo yasiyokuwa sahihi (Yohana 9:3). Bwana akaongezea tukio lingine la maafa-vifo vya watu kumi na wanane katika kuanguka kwa mnara wa Siloamu (aya 4). Yesu aliyatumia matukio haya mawili kuwafundisha somo watu wa Israeli (aya 3,5). Matukio haya yaliongeza nguvu kwenye wito wa Yesu kwa ajili ya toba katika Israeli (Mathayo 4:17). Israeli ilikuwa ndiyo kusudi la adhabu ya Mungu katika maangamizi ya Yerusalemu miaka arubaini baadaye. Kwa nini lingekuwa jambo geni kufikiri kwamba Yesu aliwasihi watu wake kwa wakati huo kwamba watubu, au la wataangamia "vivyo hivyo" katika nguvu ambayo ingekuwa ni hukumu ya Mungu dhidi ya Yerusalemu? Ule ukweli wa kihistoriahauondoi kitu chochote katika hitaji la msingi la watu kutubu dhambi zao au la wataangamia "vivyo hivyo" katika jehanamu milele.

**Dennis Gulledge anahubiri katika kanisa la Kristo kule Mabelvale, Akansas, Marekani.**

**Mamla Ya Neno**

Mungu humaanisha anachosema, pia husema anachomaanisha. Mtume Petro alisema, "*Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu; mtu akihudumu na ahudumu kwa nguvu anazojaliwa na Mungu; ili Mungu atukuzwe katika mambo yote kwa Yesu Kristo. . .*(1 Petro 4:11).

Peter O. A. Kamatula

### Uchunguzi wa Kifungu

# Kristo Anakuja Na Watakatifu Wake Wote

Kevin L. Moore



Tunasoma katika 1 Wathesalonike 3:13, ***"apate kuifanya imara mioyo yenu iwe bila lawama katika utakatifu mbele za Mungu, Baba yetu, wakati wa kuja kwake Bwana wetu Yesu pamoja na watakatifu wake wote."*** Halafu Yuda aya 14 anasema, ***"Na Henoko, mtu wa saba baada ya Adamu, alitoa maneno ya unabii juu ya hao, akisema, Angalia, Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu,"***

Kwa kuwa Bwana atakuja kwa ajili ya watakatifu wake, siyo na watakatifu wake (1 Wathesalonike 4:16-18), mwachano huu ulio dhahiri unahitaji maelezo zaidi. Neno la Kiyunani *hagioi* lina maana "watakatifu". Katika tafsiri fulani, neno *hagioi* lina maana "watakatifu" tofauti na watakatifu waliotajwa kwa Wathesalonike. Kuna watakatifu watakaokuja pamoja na Bwana katika utukufu siku ya hukumu. Watakatifu hao ni nani? Biblia inatoa jibu sahihi: "***Hapo atakapokuja Mwana wa Adamu katika utukufu wake na malaika watakatifu wote pomoja naye…"*** (Mathayo 25:41). Watakatifu watakaokuja pamoja na Yesu wakati wa kurudi kwake ni malaika (Mathayo 13:39; 1 Wathesalonike 1:7), sio wanadamu watakatifu walio hai na watakaofufuliwa, maana hao watamlaki Bwana mawinguni (1 Wathesalonike 4:16-17).

**Kevin L. Moore anatumika kama Mkurugenzi wa masomo katika Chuo Kikuu cha Feed-Hardman kule Henderson, Tennessee, nchini Marekani.**

# Msaka Tonge

**Kitabu Luka**
Rebeka Rushmore

(Majibu yako yanapatikana kwenye ganda la nyuma kwa ndani)

1. Luka alimwandikia nani kitabu chake?
2. Wataje watu wawili waliotajwa kama makuhani wakuu Yohana alipoanza kuhubiri.
3. Yesu alianzia huduma yake ya hadharani katika mkoa gani?
4. Wataje wavuvi watatu ambao walikuwa shirika wakaziacha nyavu zao kwa ajili ya kwenda kuvua watu.
5. Yesu alifanya nini usiku kabla ya kuwachagua mitume kumi na wawili?
6. Ni nani ambaye Yesu alisema kwamba alikuwa na imani kubwa kuliko mtu ye yote aliyemwona katika Israeli?
7. Wataje watu wawili waliotokea wakawa pamoja na Yesu wakati wa mabadiliko yake.
8. Mkoma aliyerejea kumshukuru Yesu alitoka mkoa gani?
9. Yesu alikuwa wapi akiomba kabla ya kukamatwa kwake?
10. Yesu alikuwa wapi alipopaa kwenda mbinguni?

# AGIZO LA DAUDI KWA SULEMANI

Therman Hodge

"***Nawe, Sulemani mwanangu, mjue Mungu wa baba yako, ukamtumikie kwa moyo mkamilifu, na kwa nia ya kumkubali; kwa kuwa Bwana hutafuta-tafuta mioyo yote, na kuyatambua mawazo yote ya fikira; ukimtafuta, ataonekana nawe; ukimwacha, atakutupa milele. Jihadhari basi; kwani Bwana amekuchagua wewe ili ujenge nyumba itakayokuwa mahali patakatifu; uwe hodari ukatende hivyo."*** (1Nyakati 28:9-10). Daudi aliwasihi watu wamche Mungu. Kumbukumbu nyingine ya maagizo inaonekana katika 1 Wafalme 2:1-4, ambayo inasomeka: ***"Basi siku ya kufa kwake Daudi ikakaribia, akamwusia Sulemani mwanawe, akasema, Mimi naenda njia ya ulimwengu wote; basi uwe hodari, ujionyeshe kuwa mwanamume; uyashike mausia ya Bwana, Mungu wako, uende katika njia zake, uzishike sheria zake, na amri zake, na hukumu zake, na shuhuda zake, sawasawa na ilivyoandikwa katika torati ya Musa, upate kufanikiwa katika kila ufanyalo, na kila utazamako; ili Bwana afanye imara neno lake alilonena kwa habari yangu, akisema, Ikiwa watoto wako wataiangalia njia yao, wakienda mbele zangu kwa kweli, kwa moyo wao wote, na kwa roho yao yote, (akasema), hutakosa mtu katika kiti cha enzi cha Israeli."***

Mtumishi wa Mungu anapaswa kumjua Mungu, "Sulemani aliagizwa amjuea Mungu wa baba yake" (2 Nyakati 8;9). Mtume Yohana aliandika kwa uvuvio namna mtu anavyoweza kujuaa kwamba anamjua Mungu- kwa kushika amri zake (1 Yohana 2:4-5). Kushika amri za Mungu ni ushahidi wa kumjua Mungu.

Pia, Sulemni alipaswa kumtumikia Mungu. "*Alipaswa kumtumikia kwa moyo mkamilifu* (aya 9-10) na vivyo hivyo wakristo wana wajibu wa kumtumikia Mungu (Matendo 11:23). Zaidi ya hayo, Sulemani

alitakiwa kumtumikia Mungu kwa "*moyo wa kupenda*." Hakuna aina nyingine ya huduma inayokubalika kwa Mungu. Huduma ya mtu inatakiwa itolewe kwa unyenyekevu-"*kwa kicho mbele za Mungu*" (Zaburi 2:11; Waebrania 12:28). Sasa je,sisi ni watumishi wa nani (Warumi 6:16-18)? Kwa kuwa Wakristo ni watumishi wa Mungu, wanatakiwa watumike namna gani- "kwa moyo" (Wakolosai 3:23).

**Sulemani alipaswa "kuzingatia".** Wosia wa Daudi kwa mwanawe ulikuwa, "*Usicheleweshe*". Nasi pia tuna wajibu wa kumtafuta Bwana mapema tena pasipo kikomo. ***"naye akatoka ili amlaki Asa, akamwambia, Nisikieni, Ee Asa, na Yuda wote na Benyamini; Bwana yu pamoja nanyi, mkiwa pamoja naye; nanyi mkimtafuta ataonekana kwenu; lakini mkimwacha atawaacha ninyi."*** (2 Nyakati 15:2"). Kadhalika, sisi nasi tunapaswa "*kuzingatia*" na "*kuendelea*" na Mungu. ***"Jitunze nafsi yako, na mafundisho yako. Dumu katika mambo hayo; maana kwa kufanya hivyo utajiokoa nafsi yako na wale wakusikiao pia."*** (1 Timotheo 4:16). Sisi wakristo tunahitaji kuzingatia sana tusije tukaanguka (1 Wakorintho 10:12-13).

**Daudi alimwambia Sulemani "***awe imara na atende*". Nguvu zinahitajika-kimaadili na kiroho. Watoto wa Mungu wanatakiwa "*kuwa imara katika Bwana"* (Waefeso 6:10). Sehemu ya utendaji ya dini iliyotolewa na Mungu haipaswi kuachwa. Utendaji ni jambo la msingi (Yakobo 1:27). Wakristo wanatakiwa kufanya kazi kwa ajili ya Bwana wetu (1 Wakorintho 15:58); Mungu anawaita watu wanaofanya kazi, kwa mfano, Musa alikuwa na makundi ya kondoo ya Yethro, Gideoni alikuwa anapura ngano, Daudi alikuwa na kondoo wa baba yake, Nehemia alikuwa anashika kikombe cha mfalme, Petro na Andrea walikuwa wanatupa nyavu zao baharini, Yakobo na Yohana walikua wanashona nyavu zao, na Paulo alikuwa anawatesa wakristo. Hakuna nafasi kwa watu wavivu au wakaa bure katika huduma ya Bwana.

**Themani Hodge ni mhubiri wa Injili na mmisionari muda mfupi katika nchi kadhaa. Anaishi Meridian, Mississippi, nchini Marekani.**

# STEFANO: SHAHIDI MWAMINIFU HADI MWISHO

BRIAN R. KENYON

Siku ya Kumbukumbu inahusu kuwakumbuka wale Wamarekani waliopoteza maisha yao katika vita. Miongoni mwetu sisi ambao tuko upande huu wa maisha tunaweza tu kusema, "*Asante*" kwa wale waliotoa sadaka yao ya mwisho kwa ajili ya kunusuru na kudumisha uhuru tunaoufurahia. Ilihitaji uaminifu ili kufanya uhuru upatikane kwa kujitolea maisha yao. Hata hivyo, kuna sababu kubwa zaidi kuliko ile ya uhuru wa kisiasa---sababu ya Kristo! Sote tunaweza kutiwa moyo na wale tunaowapata katika Maandiko ambao walilipa gharama ya mwishokwa kwa ajili ya jambo hilo, Stefano ni mfano mmojawapo. Sifa alizoonyesha zitatuwezesha pia kuishi kwa ajili ya Bwana, hata kama hilo linamaanisha kulipa gharama ya mwisho katika maisha haya kutokana na uaminifu wetu, tunapaswa kuishi kama Stefano.

## Utayari wa kuhudumu mezani

Stefano anaonekana kwa mara ya kwanza katika Matendo 6. Kanisa la Yerusalemu lilipata jukumu la kuwahudumia watu wenye uhitaji, kama Wakristo wote wanavyopaswa kufanya (Yakobo 1:27; Wagalatia 6:10). Kulingana na hali iliyokuwepo, kanisa hili halikuweza kuona mahitaji ya wajane wa Kiyunani (Matendo 6:1). Mitume wasingeweza kuacha kazi yao katika “Neno la Mungu” ili “kuhudumia meza” (Matendo 6:2). Hivyo, waliliambia kusanyiko, ***“Basi ndugu, chagueni watu saba miongoni mwenu, walioshuhudiwa kuwa wema, wenye kujawa na Roho, na hekima, ili tuwaweke juu ya jambo hili; na sisi tutadumu katika kuomba na kulihudumia lile Neno.”*** (Matendo 6:3-4).

Stefano alikuwa miongoni mwa wanaume saba ambao mkutano uliowachagua (Matendo 6:5). Alikidhi vigezo. Kwanza, alikuwa na "*sifa*

*nzuri*," ambayo inamaanisha kwamba wenzake walifikiri vyema juu ya uadilifu wake. Pili, alikuwa "*amejaa Roho Mtakatifu*." Tunajua kwamba kwa Stefano hili lilihusisha nguvu za miujiza (Matendo 6:8). Tatu, alikuwa "*amejaa...hekima*" (Matendo 6:3). Stefano alikuwa tayari kufanya yale ambayo watu wengi katika siku zetu wangefikiri ni utumwa---kuhudumu mezani! Je, tungekuwa tayari kuyafanya haya kwa sababu ya Kristo? Tutakuwa tayari tukiwa na sifa zile zile za Stefano. Ni lazima tuwe na "*sifa nzuri*" (3 Yohana 12). Ingawaje wakristo leo hawajajazwa Roho Mtakatifu kimuujiza, bado tumeamriwa kujawa na **Roho**, si kimuujiza (Waefeso 5:18). Stefano anaweza kuwa alikuwa na hekima ya aina ya kimiujiza (linganisha na 1 Wakorintho 12:8), lakini sisi tunapokea hekima kwa kumwomba Mungu (Yakobo 1:5). Je, sifa zetu zinaweza kutupa nafasi ya kuhudumia meza kama hilo ndilo angelihitaji Bwana?

## Mwalimu asiye na Woga wa Neno la Mungu

Ingawa alichaguliwa kuhudumia meza, Stefano hakusita kutumia fursa aliyokuwa nayo kuwafundisha wengine Neno la Mungu. Huenda ikawa kwamba kazi yake ya kuhudumia meza ilimpeleka katikati ya watu na hiyo kazi usambazaji wa huduma ikampa fursa ya kufundisha. Mafundisho yake yalikuwa wazi, ya kueleweka na yasiyoweza kukanushwa. Hata wale watu waliosoma sana katika sinagogi ***"lakini hawakuweza kushindana na hiyo hekima na huyo Roho aliyesema naye."*** (Matendo 6:10). Kama matokeo ya mafundisho yake yasiyopingika, alikabiliana na upinzani kutoka kwa wale ambao hawakuipenda kweli. Alishtakiwa kwa uwongo na kunenewa mambo ya uzushi.

Hata wakawashawishi watu aliosema, ***"Hata wakashawishi watu waliosema, Tumemsikia mtu huyu akinena maneno ya kumtukana Musa na Mungu. Wakawataharakisha watu na wazee na waandishi, wakamwendea, wakamkamata, wakampeleka mbele ya baraza. Wakasimamisha mashahidi wa uongo waliosema, Mtu huyu haachi kusema maneno ya kufuru juu ya mahali hapa patakatifu na juu ya***

***torati; maana tumemsikia akisema kwamba Yesu huyo Mnazareti atapaharibu mahali hapa, na kuzibadili desturi tulizopewa na Musa."*** (Matendo 6:11-14).

Hata hivyo, Stefano alikuwa tayari kujibu (Matendo 6:15), na jibu alilotoa! Alitoa historia fupi ya watu wa Mungu (Matendo 6:2-36 ); alionyesha kwamba Kristo ndiye yule Nabii ambaye Musa alisema atakuja (Matendo 6:37-38). Zaidi ya hayo, alionyesha jinsi Wayahudi wa siku zake, kama mababu zao, ambavyo hawakuishika sheria (Matendo 6:39-53). Wakristo leo lazima pia wawe walimu wasio na woga wa Neno la Mungu. Tunaweza tusihubiri hadharani na tunaweza tusiwe wasomi, lakini sisi sote tunapaswa kutumia fursa tulizonazo kufundisha Neno Lake. Kama wazazi, lazima tuwafundishe watoto wetu Neno la Mungu (Waefeso 6:4). Hii ina maana kwamba tunapaswa kujua maandiko (2 Timotheo 2:15). Haijalishi tuna cheo gani katika maisha, ujasiri unahitajika kulifundisha na kuliishi Neno la Mungu. Tunao ujasiri huo?

## Mwaminifu hata kufa

Stefano alikuwa amesema kweli, lakini badala ya wasikilizaji wake 'kuchomwa mioyoni' na kutafuta msamaha kama wale wa Pentekoste walivyofanya (Matendo 2:37), ***"Basi waliposikia maneno haya, wakachomwa mioyo, wakamsagia meno."*** (Matendo 7:54). Kifo cha Stefano kilikuwa matokeo ya moja kwa moja ya mahubiri yake. Mahubiri mengine yanawalaza wasikilizaji usingizi, lakini kwa mahubiri ya Stefano, wasikilizaji walimlaza usingizini wa kudumu (mpaka Yesu atakapokuja tena, 1 Wathesalonike 4:15-17). Mahubiri ya Stefano yalimdhuru yeye mwenyewe. Alisingiziwa na mashahidi wa uongo (Matendo 6:13), aliletwa mbele ya Kuhani Mkuu (Mdo. 7:1), na akafa kifo cha kikatili tena kisicho na huruma (Matendo 7:54-60). Kifo cha Stefano kiliathiri kanisa. kilileta huzuni kubwa (Matendo 8:2), na ikasababisha kanisa "*kutawanyika*" (Matendo 8:3-4; ling, 11:19).

Kifo cha Stefano kiliathiri mpango wa Kristo. Wote waliondoka Yerusamu, isipokuwa mitume, na kile ambacho kingeonekana kama

mwisho wa kanisa kikaleta matokeo ya upanuzi wake; Wakristo walienda kila mahali wakihubiri, kufundisha na kulieneza kanisa (Matendo 8:4). Katika kifo chake Stefano, kuna mambo muhimu sana aliyoyaona na aiyoyasema. Aliona ***"Akasema, Tazama! Naona mbingu zimefunguka, na Mwana wa Adamu amesimama mkono wa kuume wa Mungu."*** (Matendo 7:56), ambayo yaliyoonyesha kujali na kujihusisha kwake Yesu na wanafunzi wake wanapopata mateso ya kifo. Stefano alisema, ***"Wakampiga kwa mawe Stefano, naye akiomba, akisema, Bwana Yesu, pokea roho yangu."*** (Matendo 7:59), kitu ambacho kilionyesha ujasiri wake kamili katika Kristo, na ***"Akapiga magoti, akalia kwa sauti kuu, Bwana, usiwahesabie dhambi hii. Akiisha kusema haya akalala. Na Sauli alikuwa akiona vema kwa kuuawa kwake."*** (Matendo 7:60), kitu ambacho kilionyesha tabia ya kufanana na Kristo (linganisha L23:34).

Kifo cha Stefano kinatoa mwanga juu ya kauli ya Yesu, ***"Usiogope mambo yatakayokupata; tazama, huyo Ibilisi atawatupa baadhi yenu gerezani ili mjaribiwe, nanyi mtakuwa na dhiki siku kumi. Uwe mwaminifu hata kufa, nami nitakupa taji ya uzima."*** (Ufunuo 2:10). Hii haimaanishi tu tuwe waaminifu hadi siku tutakapokufa, lakini inamaanisha kuwa waminifu, hata ikiwa uaminifu wetu unatugharimu maisha yetu! Yesu alisema, ***"Msiwaogope wauuao mwili, wasiweze kuiua na roho; afadhali mwogopeni yule awezaye kuangamiza mwili na roho pia katika jehanum."*** (Mathayo 10:28 ).

## Hitimisho

Stefano alitoa uhai wake kwa ajili ya Kristo. Anasimama kama mfano kwetu. Je, tunayo tabia kwamba tungehudumu mezani ikiwa ndivyo Bwana alivyotutaka? Je, hatuna woga katika kufundisha Neno la Mungu? Je, sisi ni waaminifu hata kufa? Bwana na atupe nguvu za kutoa maisha yetu kwake, tuwe tayari kufanya kile anachosema na "tusichoke katika kutenda mema" (Wagalatia 6:9).

**Brian R. Kenyon ni Mkurugenzi wa Shule ya uhubiri ya Florida huko Lakeland, Florida, Marekani.**

# Je, Sisi ni Watetezi?

Mike Riley

*Merriam-Webster mtandaoni* inafafanua neno "*utetezi*" kwa kiingereza “apology” linatokana na neno la Kiyunani(Kigiriki) "apologia" ambalo linamaanisha, "kuzungumza kwa kujitetea." Neno hili la Kiyunani halionyeshi kukubali hatia au majuto, bali ni shauku ya kuweka wazi misingi ya jambo, imani au nafasi fulani (yaani, "**hotuba yake ilikuwa kuomba msamaha kwa ajili ya sera yake ya kigeni**"). Mtume Paulo alitumia neno la Kiyunani lililo hapo juu katika Wafilipi 1:7, 17 (vile vile katika 1 Wakorintho 9:3; 2 Wakorintho 7:11; 2 Timotheo 4:16) alipoweka wazi “*utetezi*” wake wa Injili.



Kwa hiyo, mtume Paulo aliyevuviwa alikuwa kweli “*mtetezi*” katika “*ulinzi*” wa Injili ya Kristo. Hivyo, watetezi wa imani ni wa lazima na mafunzo ya "*utetezi wa imani*" (tawi la theolojia linalojitolea katika kulinda asili ya kiroho na mamlaka ya Ukristo) ni ya lazima pia. Kwa kumtumia Paulo kama kielelezo kwetu (1 Wakorintho 11:1; Wafilipi 3:17), sisi kama Wakristo, tunapaswa kuwa tayari kila wakati kufanya "*ulinzi*" au "*utetezi*" kwa ye yote anayetuuliza habari ya tumaini lililomo ndani yetu (1 Petro 3:15).

# KWA NINI YESU ALIBATIZWA?

Jerry A. Jenkins

Kuna sababu nyingi kwanini watu wanabatizwa, kama vile (1) Wazazi wao waliwabatiza walipokuwa watoto wachanga, (2) Wale waliokaribu nao wanabatizwa, na mtu anajiunga kuwa zehemu ya kundi, (3) Wanaamini itawasaidia katika juhudi zao za kibiashara kupata ridhaa kutoka kwa wale wanaoamini kuwa ubatizo ni wa muhimu. (4) Wanaamini ni uthibitisho kwa umma kuwa kwa neema yake Mungu tayari wamekwisha okolewa, (5) Wanaamini ni sharti la wokovu. Labda kuna sababu nyingine nyingi ambazo zinawafanya watu wabatizwe.

Kwa nini Yesu alibatizwa? Bila shaka aliona ni muhimu kwa maana alisafiri umbali wa maili 70 au 80 kwenda mahali ulipokuwepo Mto Yordani ambako Yohana alikuwa akibatiza. Yesu hakubatizwa kwa sababu zilizomfanya Yohana abatize. Kwa jambo hili, ina maana Yohana alikuwa akibatiza ili mtu asamehewe dhambi zake. Mwandishi aliyevuviwa katika Agani Jipya anasema, ***" ikawa alipokuwa akipanda, mbegu nyingine ilianguka kando ya njia, wakaja ndege wakaila."*** (Marko 1:4).

Yohana alielewa kuwa Yesu hakuhitaji kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zake. Alisema, ***"Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu?"*** (Mathayo 3:13-14). Yohana alielewa kuwa yeye ni mwenye dhambi, na alielewa kuwa Yesu hakuwa na dhambi.

Sasa kwa nini Yesu alibatizwa, ikiwa si kwa sababu iliyomfanya Yohana awabatize wale waliotoka Yerusalemu, Uyahudi yote na mkoa mzima wa Yordan, walivyokuja wakiziungama dhambi zao? Bwana alitoa sababu hii, ***"Yesu akajibu akamwambia, Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote. Basi akamkubali."*** (Mathayo 3:15). Msomi mkubwa wa kimethodisti akitoa mawazo juu ya kirai hiki (maneno haya), "*kuitimiza haki yote,"* alisema, "Hilo ni agizo la kila mwenye haki…"

Yesu angekataa kutii amri ya ubatizo, angekuwa katika kambi moja na Mafarisayo na wataalam wa sheria, kama Luka alivyosema kuwa kwa kukataa kwao ***"Lakini, Mafarisayo na wana-sheria walilipinga shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye."*** (Luka 7:30). Ubatizo haukuhitajika katika Sheria ya Musa, lakini Mungu alimtuma Yohana Mbatizaji kuhubiri juu ya ukaribu wa ufalme uliotarajiwa na kuwabatiza wate kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao.

Kwanini watu katika karne ya 21 wabatizwe? Hapa kuna sababu chache: (1) kwa sababu Yesu aliamuru (Marko 16:16; Mathayo 28:18-20). (2) Kwasababu ubatizo umeunganishwa na imani na pia umeambatanishwa na wakovu katika mafundisho ya Yesu (Marko 16:16).(3) Kwa sababu ubatizo umeunganushwa pamoja na toba na msamaha wa dhambi katika fundisho la mitume (Matendo 2:28). (4) Kwa sababu katika ubatizo mtu huliitia jina lake Bwana. "*simama ubatizwe ukiliitia jina lake*" (Matendo 22:16). (5) Kwa sababu katika ubatizo mtu huletwa katika mawasiliano ya kiroho kwa damu ya Yesu (Warumi 6:3) (6) Kwasababu katika ubatizo tunatekeleza mfano wa kifo mazishi na ufufuo wa Yesu (Warumi 6;3-4).

**Jerry Jenkins (1936-2010) alikuwa mhubiri kwa miaka mingi katika Kanisa la Kristo Roebuck Parkway huko Birmingham, Alabama, Marekani.**

[**Ujumbe wa Mhariri**: Ingawa Yesu na watu leo wanabatizwa kwasababu tofauti, hata hivyo ubatizo ni wa lazima kwa watu sasa kuliko ulivyokuwa kipindi cha Yesu Kristo___ Louis Rushmore, Mhariri]

# Ukweli wa Msingi Kuhusu Ubatizo wa Agano Jipya

Ronald D. Reeves.

I. **Ubatizo unaungwa mkono na mamlaka ya Mungu.**
   A. Kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho mtakatifu (Mathayo 28:19).
   B. Kwa jina la Yesu Kristo (Matendo 2:38;8:12).
   C. Kwa jina la Bwana (Matendo 10:48).
   D. Kwa jina la Bwana Yesu (Matedo 8:16;19:5).

II. **Ubatizo ni amri ya Munguinayotakiwa kuitii.**
   A. Iliamriwa na Yesu kwa mitume (Mathayo 28:19, Mk16:15-16).
   B. Iliamriwa na Mitume kwa Wayahudi (matendo 2:38).
   C. Iliamriwa na Petro kwa mataifa (Matendo 10:48).
   D. Iliamriwa na Filipo, Mwinjisti, kwa wasamaria (Matendo 8:12).
   E. Iliamriwa na Anania kwa Sauli wa Tarso, Myahudi (Matendo 22:16).

III. **Ubatizo ni amri ya Mungu inayotumika kwa watu wote wenye uwezo wa kupambanua.**
   A. Uhusishwaji wa jumla
      1. Ulimwenguni mwote (Mark 16:15-16).
      2. Kwa mataifa yote (Mathayo 28:19).
   B. Ombi Maalum.
      1. Kwa kila kiumbe (Marko 16:15-16).
      2. Kila mmoja wenu (Matendo 2:38).

IV. **Ubatizo unatanguliwa na mambo mengine ya kiroho yanyohitajika:**
   A. Imani ya mtu binafsi katika Yesu kuwa ni Mwana wa Mungu (Markok 16:16, Yohana 3:16; 8:24).

B. Toba ya matendo ya zamani, dhambi za mtu (Matendo 2:38;17:30-31).
C. Mtu kumkiri Yesu (Warumi 10:9-10;Mdo 8:37).

**V. Ubatizo unakamilika katika maji.**

A. Watu walibatizwa katika Mto Yordani (Mathayo 3:6,13; Marko 1:5,9; Yohana 1:28).
B. Mtu alibatizwa kwa kutelemka majini (Matendo 8:38).
C. Watu walibatizwa kwa maji (Mathayo 3:11, 16; Marko 1:8; Luka 3:16; Yohana 1:26,31,33, Matendo 1:5;8:36,38; 10:47; 11:16).
D. Watu walibatizwa kwa maji mengi (Yohana 3:23).
E. Tunabatizwa kwa kuzikwa (Warumi 6:4; Kol 2:12).

**VI. Ubatizo huleta baraka za Mungu.**

A. Kuhusiana na dhambi:
   1. Mtu anaokolewa (Marko 16:16; 1Pet 3:21).
   2. Mtu anapata ondoleo la dhambi (Matendo 2:38).
   3. Dhambi za mtu zinaoshwa (Matendo 22:16).

B. Katika muunganiko na Yesu Kristo.
   1. Mtu anabatizwa katika Yesu Kristo (Warumi 6:3; Wagalatia 3:27).
   2. Mtu anabatizwa katika mauti ya Yesu Kristo (Warumi 6:3-4).
   3. Mtu anakuwa pamoja na Yesu Kristo katika ubatizo (Warumi 6:4; Wakolosai 2:12).
   4. Mtu anamvaa Kristo (Wagalatia 3:27).

C. Katika muunganiko na Kanisa la Agano Jipya.
   1. Mtu anakuwa katika mwili mmoja (1 Wakorintho 12:13).
   2. Mtu anaongezwa ndani ya Kanisa (Mdo 2:41,47).

**VII. Ubatizo unafuatiwa na maisha yaliyobadilika (Rum 6:3-4).**

**Ronald D. Reeves anahubiri katika kanisa la Kristo la College Avenue kule DeFuniak Spring, Florida, Marekani.**

# Ni Changamoto Gani Ambazo Kanisa La Karne Ya Kwanza Lilikabiliana Nazo? Mapambano Dhidi Ya Serikali na Desturi za Kidini

Jeremy W. Barrier

Kutokana na mafunzo ya kitabu cha Matendo Ya Mitume na nyaraka kwa makanisa, tunaweza kuona kuwa kanisa la awali lilikabiliana na desturi za mahali husika na za kidini, na huenda hali hii ndiyo iliyozuia lisikue miaka ya mwanzoni.

## Walikabiliana na Desturi za Kidini

***"Wakashuka watu waliotoka Uyahudi wakawafundisha wale ndugu ya kwamba, Msipotahiriwa kama desturi ya Musa hamwezi kuokoka. Basi baada ya Paulo na Barnaba kushindana na watu hawa na kuhojiana nao sana, ndugu wakaamuru kwamba Paulo na Barnaba na wengine miongoni mwao wapande kwenda Yerusalemu kwa mitume na wazee kwa habari ya swali hilo."*** (Matendo 15:1-2).

Katika Matendo 15, tunasoma kuhusu "*kutokukubaliana*" kulikotokea kati ya baadhi ya wakristo waliotokea Uyahudi, walioitwa "*ndugu*" katika fungu hili, na wale waliotoka Antiokia, mji uliopo pwani ya mashariki ya Bahari ya Mediterrania. Kiini, kilikuwa ni kutoelewana kulikoibuka kati ya watu walioishi katika ulimwengu wa desturi tofauti tofauti. Kweli, walikuwa wote pamoja kama kundi la wakristo, lakini walikuwa na tamaduni na desturi tofauti tofauti za kidini. Jambo lililokuwa linabishaniwa hasa lilihusiana na wakristo kwamba lazima watimize desturi ya kiyahudi ya tohara. Tohara kwa Wayahudi ilikuwa ishara ya agano kati yao na Mungu kwa mujibu wa torati.

Kipindi cha karne ya kwanza, katika desturi yao, Wayahudi walioishi Palestina waliwatahiri watoto wachanga na hata watu wazima walioongokea dini ya kiyahudi. Lakini, wayahudi walioishi nje

ya Palestina, walioitwa wayahudi waliotawanyika [Wayahudi wa kiyunani], mara nyingi tohara haikuhitajika kwao ili waongolewe katika imani yao. Hivyo, hali hii ilileta mvutano miongoni mwa wayahudi na desturi za imani zao. Jambo la kufurahisha ni kwamba, wayahudi wengi waliongoka na kufanyika kuwa wakristo. Lakini katika kuongoka kwao waliingia na desturi zao za dini ya kiyahudi ndani ya kanisa, jambo ambalo lilileta mtafaruku mkubwa. Basi, Wayahudi wa kundi la Wanazarayo, ambao tayari walishafanyika kuwa Wakristo walikuwa wanapambana na hali ya kuwataka waongofu wapya watahiriwe kama ilivyokuwa desturi ya Musa. Kama tunavyosoma katika Matendo 15, tukimalizia mpaka mwisho wa sura, tunaona jinsi wale wakristo wa awali walivyoendelea kujadiliana juu ya jambo hilo kule Antiokia, halafu baadaye Yerusalemu---Yerusalemu kikiwa kitovu kwa makundi yote mawili, kundi lenye asili ya dini ya kiyahudi na watu wa mataifa. Wanaume katika mkutano wa Yerusalemu walipoachana na swala la “maafikiano”, walikuwa wanakubaliana ingawa maelekezo ya uongozi uliovuviwa yalikuwa kwamba wazingatie ukweli kwamba ibada za sanamu zizuiliwe kwa wakristo, lisiwepo swala la kula damu, na kwamba uasherati ukomeshwe. Pia tangazo likatolewa kwamba wale watu wa mataifa wako huru mbali na sharia ya kiyahudi ya tohara.

Hata hivyo, makubaliano haya yalidumu kwa kipindi fulani tu. Mara tu ukristo ulipoanza koenea maeneo mengine yenye desturi mpya na tofauti tofautis, tohara iliendelea kujitokeza na ikaonekana kama suala linalowagawa. Jambo hilo lilijitokeza kule Galatia, kama tunavyosoma katika waraka wa mtume Paulo kwa Wagalatia kwamba kundi la wapenyezaji lilikuwa likiwashinikiza Wagalatia wawatahiri waongofu wao wapya katika Kristo. Paulo alipinga kwa nguvu zote uamuzi kama huo akiwatia moyo Wagalatia wadumishe uhuru wao kutokana na vitendo vya ibada, na kwa maana hiyo alipinga mienendo yao. Kwa kumnukuu Paulo, alisema katika Wagalatia 5:1-2, ***"Katika ungwana huo Kristo alituandika huru; kwa hiyo simameni, wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa. Tazama, mimi Paulo***

***nawaambia ninyi ya kwamba, mkitahiriwa, Kristo hatawafaidia neno."***

Jambo la kufurahisha kuhusu uamuzi huu ni kwamba Paulo, kwa sababu mbalimbali, aliona kwamba lazima apinge tohara kwa sababu ilikuwa inakiuka uadilifu katika injili. Katika sura ya kwanza ya waraka wake kwa Wagalatia, aliwaonya Wgalatia akiwaambia waikatae injili yoyote ambayo si ile ya kweli iliyohubiriwa kwao kwanza. Maelezo muhimu ya kukumbuka hapa ni kwamba Paulo hakupinga zoezi la kiutamaduni la tohara yenyewe. Alipinga tohara kama kwa namna yoyote ilifanyika kwa kusudi la kuashiria injili. Katika Matendo 16:1-4, tunasoma kuhusu Paulo akimwomba kijana Timotheo ambaye aliambatana naye katika safari atahiriwe, Timotheo akatahiriwa. Jambo la kufurahisha katika tukio hili ni kwamba Timotheo alikuwa mtoto wa baba wa kiyunani na mama wa kiyahudi. Kwa sababu ya baba yake myunani, Timotheo alikuwa hajatahiriwa. Lakini kwa kuwa Paulo alimwomba asafiri naye, akamtahiri "kwa sababu ya wayahudi waliokuwepo sehemu zile" ambazo Paulo na Timotheo walitaka kuziendea. Kinachothbitishwa kwetu hapa ni kwamba Paulo alikuwa tayari kutahiri au kuacha wengine watahiriwe, ili asiwakwaze watu kwa sababu za kiutamaduni, lakini pale tu alipoona kwamba haitaleta mkanganyo katika ukweli wa injili.

## Mipango ya kutunza majira:

Suala lingine ambalo tunaliona linajitokeza kama jambo gumu kwa wakristo wa kwanza, lilikuwa ni kuamua kalenda gani waitumie. Hili ni jambo ambalo wengi wetu tunatumia muda kidogo kulifikiria leo, hasa kwa vile nchi nyingi na watu wengi wamepitisha kalenda ya aina moja. Lakini, jambo hili lilikuwa gumu sana kuwaongoza wakristo wa kwanza, kwa maana wakristo wa mwanzo waliokuwa wanaishi katika ulimwengu wa eneo la Mediterrania kulikuwa na kalenda kuu mbili walizokuwa wamezizoea. Kwanza, kulikuwa na kalenda ya kirumi iliyotengenezwa kulingana na miendo ya Jua huku siku nyingi za juma zikitajwa kwa kuiheshimu miungu ya Wayunani na Warumi, na misimu minne ya mwaka ikiwa imewekwa katika msingi wa elimu ya visasili ya

kiyunani. Mwaka ulijawa na sherehe nyingi za kidini na pia ulijaa kila ilivyowezekana na imani za kidini za kipagani.

Kalenda nyingine muhimu ilikuwa kalenda ya kuyahudi, iliyotengenezwa kukingana na miendo ya Mwezi na kulingana kabisa na mtazamo wa ulimwengu wa kiyahudi na siku moja tu ya juma, *Sabato*. Hakuna siku nyingine yoyote iliyojulikana kwa jina isipokuwa *Sabato.* Kama kulitokea ulazima wa kuitaja siku nyingine yoyote, basi iliitwa: siku moja kutoka Sabato, siku mbili kutoka Sabato, nk. Hiki ndicho tunachokiona hata kwa mtume Paulo akikisema katika 1 Wakorintho 16:2 au Luka alipoandika katika Matendo 20:7, "siku ya kwanza ya juma [kutoka Sabato], tulipokutana kumega mkate..." kalenda hii pia ilijawa na matukio, sherehe za mwandamo wa mwezi na vipengele vingine vya misimu ya kushika nyakati, lakini yote yalitegemea kalenda ya mwezi wa kiyahudi. Tunaona kalenda hizi zikijadiliwa kama sehemu mbili katika Agano Jipya (Gal 4:10, Kol 2:16). Wakolosai 2:16 inasema, ***"Basi, mtu asiwahukumu ninyi katika vyakula au vinywaji, au kwa sababu ya sikukuu au mwandamo wa mwezi, au sabato;"*** Wagalatia 4:10 inasema, ***"Mnashika siku, na miezi, na nyakati, na miaka."***

Jambo la kufurahisha kuhusu sehemu zote mbili a maandiko ni kwamba zinataja mawazo yanayohusiana na imani ya kikristo na mipango ya kushika nyakati. Kwanza, katika Wakolosai, Paulo anawatia moyo waumini wasiruhusu mtu awahukumu kwa sababu walikuwa wakitumia mipango ya kushika siku ambayo kwa asili ilikuwa katika mfumo wa kiyahudi na kipagani. Wakati Paulo hakuwa akipendekeza kwamba Wakolosai wakiri au waheshimu imani ya kipagani, kwa upande mwingine alikuwa akinasema Ukristo ni mkuu zaidi ya hili, na kushauri kuwa si lazima kwa Wakristo kuunda kalenda yao wenyewe. Hata hivyo, Paulo alitambua kuwa hizi kalenda za kipagani zilikuwa zimejengwa juu ya imanj ambayo si ya kweli, bali sanamu tu (angalia 1 Wakorintho 8:4, ambapo Paulo alisema, ***" Basi kwa habari ya kuvila vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu; twajua ya kuwa sanamu si kitu katika ulimwengu, na ya kuwa hakuna Mungu ila mmoja tu."***

Kwa upande wa Wagalatia mambo yalikuwa kinyume kabisa. Wagalatia walikuwa wamekubali kalenda (hasa ya kipagani) ya kidini, na ilikuwa imeingia kati yao na Mungu wao! Baadaye katika jambo hili tunaona mambo mengine yaliyokithiri inawezekana yalitoa nafasi kwa desturi za mahali husika. Basi katika hali hii, mpango wa kushika nyakati au hata tohara ulifika hatua ya kumtenga mtu na Mungu wake. Ukweli ni kwamba, mtu anachotakiwa kuwa mwangalifu kukifanya ni kuepuka kujichanganya juu ya mambo mawili na kutokutoa hukumu haraka.

## Hitimisho:

Kwa kuhitimisha, nataka kusema mambo kadhaa kwa mara moja. Kwanza, Injili ya Kristo haibadiliki, na ukweli wa Injili unapaswa kudumishwa kwa lolote tunalolifanya. Pili, kanisa la kwanza wakati mwengine lilikuwa na matatizo ya kutofautisha kati ya Injili na tamaduni za kidini za mahali husika. Desturi tuliyoitazama hapa ni tohara, na kwa ufupi sana, tuliifikiria juu ya kalenda ya Kiyunani-Kirumi dhidi ya kalenda ya Kiyahudi. Katika kila jambo, tulichokiona ni Wakristo kufanya jitihada ili kujua lini na wapi desturi za mahali husika zinaweza kudumishwa, na ni wakati gani destruri hizo zinapaswa kutoa njia kwa ajili ya injili.

Hata hivyo, tunachotaka kutambua ni kwamba Wakristo wa kwanza walikuwa kwenye hatari ya kutoendelea kama kundi la imani mpya kwa sababu walikuwa hawawezi kutofautisha kati ya desturi za kidini na Injili, jambo ambalo lilipelekea wakati mwingine kuingiza desturi zao za kienyeji kwa watu wengine. Mwisho, lakini si kwa umuhimu, tunaona kuwa Paulo hakuwa na tatizo na desturi za mahali, hata desturi za kipagani za mahali fulani kama vile kula baadhi ya vyakula kwa jina la miungu au pia mipango ya kushika nyakati, kama kalenda. Hakuwa na tatizo na hivyo, isipokuwa kama vinahatarisha Injili.

Inachukua uvumilivu mwingi na hekima kutofautisha, na mtu anapaswa awe mwangalifu wakati wa kufanya tofauti hizi ndani ya nchi ya mtu mwingine. Hatimaye, tunachokiona ni kwamba Paulo, ambaye mara nyingi alipenda kutoa “uhuru” kwa Mkristo alikuwa mwakilishi

wa Injili ambayo tunaiona leo. Alikuwa halazimishi mambo ya Imani yaliyowazidi waliomzunguka, na wakati mwingine hali hii ilimletea ugumu. Hata maisha yake yalipofika mwishoni, ni injili aliyoibeba iliyoushinda ulimwengu. Kama tunataka Injili kiwe kitu chenye nguvu, tunatakiwa tusiingize kwenye mikanganyo ya desturi za kijamii na za kidini.

**Jeremy W. Barrer ni mwinjilisti mmisionari na mkuu wa prgramu ya wahitimu katika Chuo Kikuu cha Florence, Albama, Marekani.**

## Tusimame Katika Kweli

Yesu alitoa tahadhari juu ya mafundisho ya uongo. Katika Mathayo 7:15 alisema, "*Jihadharini na manbii wa uongo, watu wanaowajia wamevaa mavazi ya kondoo, walakini kwa ndani ni mbwa mwitu wakali*." Pia, Yesu aliwatahadharisha wanafunzi kuwa makini na makristo na manabii wa uongo wakati wa maangamizi ya Yerusalemu, akasema, "*Kwa maana watatokea makristo wa uongo, na manabii wa uongo, nao watatoa ishara kubwa na maajabu; wapate kuwapoteza, kama yamkini hata walio wateule* (Mathayo 24:24).

Yesu anataka tumwamini kupitia neno la mitume. Alipokuwa akituombea umoja alisema, "*Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja...* (Yohana 17:20-21). Neno la Kristo lilikabidhiwa kwa watakatifu wote kupitia kwa mitume kama alivyosema Yuda katika waraka wake, "*Wapenzi, nilipokuwa nikifanya bidii sana kuwaandikia habari ya wokovu ambao ni wetu sisi sote, naliona imenilazimu kuwaandikia, ili niwaonye kwamba mwishindanie imani waliokabidhiwa watakatifu mara moja tu*." (Yuda 3). Pia Yuda alito tahadhali kwa watakatifu juu ya maadui wa Injili aliposema, "*Bali ninyi wapenzi, yakumbukeni maneno yaliyonenwa zamani na mitume wa Bwana wetu Yesu Kristo, . . . .*" (Yuda 17-19).

**Peter O. A. Kamatula**

# Wote Wanakubali

Guy caskey

Watu walioanzisha harakati za kidini, kama vile harakati za matengenezo, walikubaliana wao kwa wao, kisha na Biblia katika ya kwanza wakifundisha yale yanayotakiwa ili kufanyika kuwa wkristo na kumuabudu Mungu.

1. **Anataka tuwe na umoja:** *"Wala si hao tu ninaowaombea; lakini na wale watakaoniamini kwa sababu ya neno lao. Wote wawe na umoja; kama wewe, Baba, ulivyo ndani yangu, nami ndani yako; hao nao wawe ndani yetu; ili ulimwengu upate kusadiki ya kwamba wewe ndiwe uliyenituma."* (Yohana 17: 20-21).
2. **Anataka tuenende kwa kanuni moja:** *"Lakini, hapo tulipofika na tuenende katika lilo hilo."* (Wafilipi 3:16).
3. **Anataka tuwe na malengo sawa:** *"Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioitiwa; kwa unyenyekevu wote na upole, kwa uvumilivu, mkichukuliana katika upendo; na kujitahidi kuuhifadhi umoja wa Roho katika kifungo cha amani."* (Waefeso 4:1-3).
4. **Anataka tunene mamoja:** *" Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.."* (1 Wakorintho 1:10).
5. **Anataka tutambue mamlaka yake:** *"Yesu akaja kwao, akasema nao, akawaambia, Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani.."* (Mathayo 28:18). *"aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka, na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu*

*vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa; ambalo"* (Waefeso 1:20-22).

6. **Anataka tufuate kiwango kimoja cha mwenendo maishani mwetu kwa ajili ya kanisa na Injili:** *"Mtu akisema, na aseme kama mausia ya Mungu;.."* (1Petro 4:11). *“Kila apitaye cheo, wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia.”* (2 Yohana 1:9).

## Wasikilize Watu Hawa kwenye Mambo ya Msingi ya Injili:

**John Calvin** (presbyterian): Marko 16:15-16: "aliwaamuru wote wanaoamini kubatizwa kwa ajili ya ondoleo la dhambi zao. Kwa hiyo, wale wanaofikiria kuwa ubatizo hauna kitu chochote zaidi ya alama au ishara ambayo tunakiri dini yetu mbele za watu, kama askari anayevaa ishara ya mkuu wao kama alama ya taaluma yao, haijazingatia kitu cha kanuni katika ubatizo, ambayo inatupasa kuipokea pamoja na ahadi, "aaminie na kubatizwa ataokoka." Neno ubatizo maana yake "zamisha" na ni hakika kwamba kuzamishwa kulionekana katika kanisa la kwanza (Institute, Book IV, sura 13)

**John Wesley** (Methodist) alisema juu ya Warumi 6:3 na Yoh 3:5: "tunazikwa pamoja naye, inahusu njia ya zamani ya ubatizo kwa kuzamisha… Kwa maji halafu, kama njia ya ubatizo wa maji, tunazaliwa upya; ambapo tendo hilo pia linaitwa na mtume, ‘kuosha kwa kuzaliwa upya’ (Tito3:5)” (*Notes on the New Testament, 1825*).

**Martin Luther** (Lutheran) alisema juu ya ubatizo: “kwa maelezo haya ningependa wale wanaobatizwa wazamishwe kabisa ndani ya maji kulingana na neno lenyewe, na umuhimu wa agizo, bila shaka ulianzishwa na Kristo” (*Works Volume 11, 76*).

**Timothy Dwight** (Mwanakusanyiko; raisi wa zamani wa Chuo Kikuu cha Yale) alisema juu ya Yohana 3:5 : Kuzaliwa kwa maji hapa maana yake ubatizo, na kwa mtazamo wangu, ni muhimu kwa kukiri kwetu kwa kanisa linaloonekana."

**Adam Clarke** (Methodist), juu ya Warumi 6:4 na Wakolosai 2:12: "kuna uwezekano kwamba, hapa mtume alikuwa anataja hali ya kusimamia ubatizo kwa kuzamisha, mwili mzima kwa kuuweka ndani ya maji".

**Clarke** anaendelea: anataja kuzamisha ambapo jambo hilo linafanyika kwa watu wazima kitendo ambacho mtu anaoneka kuzikwa ndani ya maji, kama Kristo alivyozikwa chini ya ardhi, akafufuka tena siku ya tatu. Basi kuibuka kwao kutoka majini, ilikuwa nembo ya ufufuo wa mwili; na ndani yao, kunakuwa na mabadiliko ya maisha kwa jumla".

**Lenski (Lutheran):** "ubatizo huu---kama ulivyoagizwa kwa mataifa yote kwani kwa ajili ya ondoleo la dhambi. Kuukataa ubatizo itakuwa ni kumkataa Kristo na zawadi zote zilizomo katika jina lake. Ubatizo ni Injili safi inayotoa neema na wokovu toka kwa Mungu kupitia kwa Kristo; haitakiwi kubadilishwa kuwa ya kisheria au mahitaji ya kisheria. Kihusishi hiki (ndani) huunganisha msamaha kwa karibu sana na ubatizo kwamba hakuna mtu anayeza kuvitenganisha hivi vitu viwili.

**Barnes** (Presbyterian): "Ubatizo ni utayari wa kusamehewa kwa njia hiyo na ni tamko zito la imani yetu kwamba hakuna njia nyingine ya ondoleo. Anayekuja kubatizwa anakuja na imani kubwa kwamba yeye ni mwenye dhambi, na kwamba hakuna njia nyingine ya rehema bali ni Injili, na kwa utayari mkubwa wa kufuata masharti ya wokovu, na kuipokea kama inavyotolewa kupitia Yesu kristo".

**Expository Greek New Testament:** "kama kila mtu alivyopaswa kubatizwa, kwa kufanya hivyo kila mmoja angepata msamaha wa dhambi zake".

**Pulpit commentary:** "Petro anahubiri neno kwa nguvu, wasikilizaji wanachomwa mioyo yao, na kwa maelekezo yake wanabatizwa, na hivyo kuupata wokovu ulioahidiwa. Paulo anafundisha kuwa tulibatizwa katika mauti ya Kristo, na tumewekwa huru mbali na dhambi. Kama mazishi yetu, kuzamishwa kabisa ndani ya maji kulifuatiwa na kuibuka kutoka majini, kwa hivyo kifo chetu na

Kristo katika katika kuifia dhambi, ambapo kuzamishwa ni ishara ya kuzikwa, kunakiwa kufuatiwe na ufufuo wetu pamoja naye kwa maisha mapya.

## Kushiriki Chakula cha Bwana kila Juma.

**John Calvin** (Presbyterian): "Kila juma meza ya Bwana ilipaswa kupelekwa kwenye mikusanyiko yote na ahadi ilitangazwa, ambayo, katika kushiriki, tunaweza kulishwa kiroho (*Institute*,Book VI,chapter 18).

**John Wesley** (Methodist): "Pia nawashauri wazee wasimamie chakula cha Bwana kila siku ya Bwana. Kwa heshima hii au amri nyingine yoyote, yeye ambaye anaweza kutii, kama hatatii hatakuwa na sehemu katika ufalme wa mbinguni". (*Letters to America*,1784).

**August Neander** (Lutheran church historian): "chakula cha Bwana kilikuwa bado ni sehemu ya ibada ya Mungu kila Jumapili. Kanisa zima lilishiriki baada ya amina ya maombi yaliyotangulia. Mashemasi walipeleka mkate na mvinyo kwa kila mtu aliekuwepo (*Church history*, Volume 1,332).

**Charles Spurgeon** (Baptist): Alishiriki chakula cha Bwana kila juma na kusanyiko lake katika Hema kuu ya London.

**Ignatius.** Alieishi kutoka mwaka 30 B.K mpaka 107 B.K, alisema: "Hakuna kushika Sabato tena, ila kuishi katika kuishika siku ya Bwana, ambayo katika hiyo uzima wetu ulileta tena na Yeye kwa njia ya kifo chake.

## Jina Mkristo

**Martin Luther:** "nawasihi, mwachane na jina langu; msijiite kwa jina hilo, bali jiiteni wakristo" (*Life of Luther* by strork, 289).

**John Wesley** (Methodist): "Nataka sana jina methodist lisitajwe tena, lizikwe katika usahaulifu milele. Ila kwa Mungu majina hayo yote ya chama na misemo isiyo kimaandiko na mifumo ambayo imewagawa Wakristo huenda ikasahaulika". (*Universal Knowledge*, Volume IX, 540).

**Charles Spurgeon** (Baptist): "Natarajia jina Baptisti litapotea hivi karibuni lakini acha jina la Kristo liishi milele."

**Adam Clarke** (Methodist): "Sasa kwa kuwa walikuwa na majina yao kutoka kwa wale mabwana mkubwamao waliohudhuria na kuyaamini mafundisho yao, kwa hiyo wanafunzi waliitwa Waktisto kwa sababu walimchukulia Kristo kuwa mwalimu wao, wakayakubali mafundisho yake, na kufuata kanuni ya maisha iliyowekwa na Yeye.

**Clement** (Mwana Historia wa zamani wa Alexandria): "Tunakushukuru kwa kuwa tunaitwa kwa jina la Kristo, na hivyo tunahesabiwa kuwa wako.

Maneno ya **Polycarp** alipokuwa anakufa: "Sasa ni mkristo".

## Kuimba bila ala za muziki:

**John Calvin** (presbyterian):"Vyombo vya muziki katika kusherehekea kwa kumsifu Mungu haitafaa tena kuliko kufukiza uvumba, kuwasha taa na marejesho ya vivuli vingine vya sheria. Wabaptisti, kwa hiyo kwa ujinga pamoja na vitu vingine vingi, wameazima kutoka kwa wayahudi (*Commentary on psalm* 33).

**Charles Spurgeon** (Baptist): "Israel alikuwa shuleni na alitumia mambo ya kitoto kumsaidia kujifunza. Lakini siku hizi, wakati Yesu anatupa utu uzima wa kiroho, mtu anaweza kuimba nyimbo bila nyuzi na vinubi. Hatuvihitaji, vinaweza kuzuia badala ya kusaidia sifa" (Zaburi 33:2). "Tunaweza pia kuomba kwa mashine kama tunavyoweza kutumia kusifu kwayo". (*Girardeau instrumental music*, 176)

**John Wesley** (Methodist): "Sina pingamizi juu ya ogani [vyombo vya muziki] katika ibada zetu, isipokuwa hazionekani wala kusikika (*Adam Clarke's commentary*).

**Wakristo hawakutumia vyombo vya muziki katika karne ya kwanza.**

## Watu hawa Walikubaliana na Biblia juu ya Masomo Haya

Suala juu ya kuzamisha kwa ondoleo la dhambi, hivi ndivyo Biblia inavyosema: *"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa*

jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea *kipawa cha Roho Mtakatifu*. "(Matendo ya Mitume 2:38). "*Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima*." (Warumi 6:4).

Juu ya somo la kushiriki chakula cha Bwana kila juma: "*Hata siku ya kwanza ya juma, tulipokuwa tumekutana ili kumega mkate, Paulo akawahutubu, akiazimu kusafiri siku ya pili yake, naye akafuliza maneno yake hata usiku wa manane*." (Matendo 20:7). "*Wakawa wakidumu katika fundisho la mitume, na katika ushirika, na katika kuumega mkate, na katika kusali*." (Matendo ya Mitume 2:42).

Somo juu ya jina wakristo: ***"Na wanafunzi waliitwa wakristo kwanza hapo antiokia"*** (Matendo ya mitume 11:26). ***"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo."*** (Matendo ya Mitume 4:12). ***"Na kila mfanyalo, kwa neno au kwa tendo, fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu"*** (Wakolosai 3:17).

Somo juu ya muziki wa vyombo: ***"Neno la Kristo na likae kwa wingi ndani yenu katika hekima yote, mkifundishana na kuonyana kwa zaburi, na nyimbo, na tenzi za rohoni; huku mkimwimbia Mungu kwa neema mioyoni mwenu."(***Wakolosai 3:16). ***"mkisemezana kwa zaburi na tenzi na nyimbo za rohoni, huku mkiimba na kumshangilia Bwana mioyoni mwenu;"*** (Waefeso 5:19).

**Maelezo ya Mwandishi: Guy Caskey (mwanzishi wa uchapishaji wa kazi) aliandika makala hii ambayo mwanzoni ilichapishwa mwez Agosti 1994 juu ya swala la *Mpaka Miisho ya Dunia*.**

## Nyimbo Katika Ibada

Kila mkristo anapoketi katika sehemu ya kuabudia anakuwa na vitu vitatu: **Mwili**, **roho**, **kweli** (Neno). Katika hivyo vitu vitatu anatakiwa avitumie viwili kumwabudu Mungu: **roho** na **kweli** (Yohana 4:24). Mwili haukupewa juku la kuabudu, bali ni chombo tu cha kuisaidia roho itekeleze majukumu yake. Halafu roho haijaagizwa iimbe na kucheza.

**Peter O. A. Kamatula**